ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/ Waziri wa Afya/ /Jimbo la Ziwani.
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Miundombinu n Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.

21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Said Hassan Said	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani

49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	Jimbo la Jang'ombe

79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake

81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Thelathini na Moja - Tarehe 26 Juni, 2014

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mahmoud Muhammed Mussa) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba kuweka mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2014/2015. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo naomba kuweka hati mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2014/2015. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Hoja za Serikali

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 - Wizara ya Fedha

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujamkaribisha Mhe. Waziri wa Fedha, kwanza kuna matangazo hapa. Waheshimiwa Wajumbe, kwa siku ya leo tumepata wageni ambao ni wanafunzi wa Skuli ya Msingi Mtoni, jumla yao ni 30, wamefuatana na walimu wao wanne. Naomba wanyanyuke ili tuwatambue. Ahsanteni kaeni kitako.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu sasa likae kama Kamati ili kupokea, kuzingatia, kujadili na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijaalia kwa mara nyengine tena kusimama mbele ya kikao cha Baraza lako Tukufu kwa ajili ya kuwasilisha mapendekezo ya Bajeti ya Wizara ya Fedha, tukiwa wazima na wenye afya njema.

Mhe. Mwenyekiti, pili, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kutuongoza na kutuelekeza kwa busara na hekima katika kuwaongoza watendaji wa Wizara hii na wananchi kwa ujumla. Aidha, nawashukuru pia wasaidizi wake wakuu, Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais na Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais kwa ushirikiano wao mzuri wanaonipa katika kufanikisha kazi zangu.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kukupongeza wewe mwenyewe binafsi, Mhe. Spika, Naibu Spika na Mwenyekiti wa Baraza kwa kuongoza vyema majadiliano ya bajeti. Kupitia kwako, naomba nitumie nafasi hii kuishukuru kwa namna ya pekee Kamati ya kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni) kwa maoni, ushauri na mapendekezo waliyoyatoa kwa Wizara wakati wa kuchambua mapendekezo ya Bajeti ya Wizara ya Fedha. Katika uandaaji wa hotuba hii, Wizara imezingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati hiyo pamoja na ushauri na maoni ya hoja mbali mbali zilizotolewa na Wajumbe wa Kamati wakati wa mjadala wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2013/14.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda sasa kuchukua fursa hii kueleza majukumu makuu ya Wizara ya Fedha, mapitio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2013/14, na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2013/14 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2014/15.

MAJUKUMU YA WIZARA YA FEDHA

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya Bajeti ya Serikali tarehe 14 Mei, 2014, Wizara yangu ni moja ya Wizara zilizoguswa na marekebisho ya muundo wa Serikali yaliyofanywa na Mhe. Rais mwezi Agosti, 2013. Chini ya marekebisho hayo jukumu la uratibu wa kazi za Tume ya Mipango

limehamishiwa Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora. Kwa msingi huo kwa sasa Wizara ya Fedha ina majukumu makuu yafuatayo:

i. Kusimamia Mapato ya Serikali ikiwemo ya ndani na kutoka nje ya nchi;

ii. Kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za umma ikiwemo uratibu wa deni la Taifa;

iii. Kusimamia mali za Serikali pamoja na Mashirika ya Umma;

iv. Kutoa huduma za kiuhasibu Serikalini;

v. Kusimamia Sekta ya Fedha nchini na maendeleo yake; na

vi. Kutoa huduma za utawala na kiutumishi kwa idara zake.

MAPITIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2013/14

Mhe. Mwenyekiti, uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa Bajeti ya Wizara ya Fedha umezingatia malengo ya Mpango Mkakati wa Wizara wa mwaka 2011/12 - 2013/14 ambao utaiwezesha wizara kufikia Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2020; MKUZA II; Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015. Aidha, utekelezaji wa Bajeti ulizingatia pia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2010.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kutoa tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kwa kufanya Mapitio ya Mapato na Matumizi ya Wizara.

MAPATO YA MWAKA 2013/14

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuwa wizara hii ndio msimamizi mkuu wa ukusanyaji mapato kutoka vianzio vya ndani na nje ya nchi kama nilivyoeleza katika Bajeti ya Serikali ambayo niliisoma mwanzoni mwa kikao hiki, Wizara hii pia ina wajibu wa kukusanya mapato ya ndani na baadae kuingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kama ilivyo kwa Wizara nyengine. Katika kipindi cha mwaka 2013/14, Wizara ya Fedha ilikadiria kukusanya jumla ya TZS 5,997.269 milioni kutoka vyanzo mbali mbali vya ndani katika Maidara na Taasisi. Mpaka kufikia Mei 31, 2014 Wizara imeweza kukusanya jumla ya TZS 3,285.6 milioni, sawa na asilimia 55 ya makadirio ya mwaka.

MATUMIZI YA MWAKA 2013/14

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2013/14 Wizara ilitengewa kutumia jumla ya TZS 154,320.40 milioni, ambapo TZS 45,767.0 milioni ni kwa ajili ya kazi za kawaida, TZS 42,438.40 milioni kwa ajili ya kazi za maendeleo na TZS 66,065.0 milioni kwa ajili ya matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali. Katika fedha za maendeleo jumla ya TZS 8,000.0 milioni ni mchango wa Serikali, TZS 17,488.40 milioni ikiwa ni misaada na mikopo kutoka nje na TZS 17,000.0 milioni kwa ajili ya ununuzi wa meli.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwishoni mwa Mei, 2014 wizara imeweza kutumia jumla ya TZS 124,633.58 milioni sawa na asilimia 81 ya makadirio, ambapo TZS 40,023.9 milioni zilitumika kwa kazi za kawaida, sawa na asilimia 87 ya makadirio, TZS 23,509.68 milioni kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 55 na TZS 61,100 milioni kwa matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali sawa na asilimia 93 ya makadirio.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo ya jumla kuhusu mapato na matumizi ya fedha za wizara kwa mwaka 2013/14, naomba sasa kuwasilisha taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya wizara kwa mwaka wa fedha 2013/14.

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014 NA MAKADIRIO YA MWAKA 2014/2015

USIMAMIZI NA UTUNZAJI WA MAPATO NA UDHIBITI WA RASILIMALI ZA UMMA

Mhe. Mwenyekiti, jukumu la kusimamia, kutunza na kudhibiti rasilimali za umma ndani ya Wizara ya Fedha linatekelezwa na Idara ya Bajeti, Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Idara ya Fedha za Nje na Idara ya Uhakikimali na Mitaji ya Umma.

IDARA YA BAJETI

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ina jukumu la kugawa rasilimali fedha kwa ajili ya Bajeti ya Serikali na kutoa mwongozo wa matayarisho ya Bajeti kwa kila mwaka. Aidha, Idara hii ndio inayosimamia malipo ya mishahara ya wafanyakazi wa Serikalini. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ilitengewa jumla ya TZS 35,534.21 milioni. Kati ya fedha hizo, TZS 17,500 milioni ni kwa ajili ya marekebisho ya mishahara Serikalini, TZS 17,363.00 milioni kwa ajili ya ruzuku kwa taasisi zilizo chini ya wizara na TZS 671.1 milioni ni kwa matumizi ya kazi za kawaida ya Idara.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Mei, 2014, Idara imetumia jumla ya TZS 31,884.87 milioni sawa na asilimia 90 ya makadirio, ambapo TZS 17,500 milioni sawa na asilimia 100 zimetumika kwa ajili ya marekebisho ya mshahara, TZS 13,908.45 milioni sawa na asilimia 80 kwa ajili ya ruzuku na TZS 476.42 milioni sawa na asilimia 71 kwa kazi za kawaida za idara.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza kazi zake za kawaida, idara imeweza kutekeleza majukumu yafuatayo:

i) Kuratibu shughuli za kibajeti na uandaaji wa mwongozo wa Bajeti na kusambazwa katika mawizara na idara zinazojitegemea katika mwezi Disemba, 2013;

ii) Kuandaa na kuchapisha vitabu vya makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali ya mwaka 2014/15 katika utaratibu wa vifungu pamoja na programu kwa ajili ya mjadala wa Bajeti unaoendelea wa Baraza la Wawakilishi;

iii) Kuwajengea uwezo katika kuandaa Bajeti zenye kuzingatia programu kwa maafisa wanaoandaa Bajeti kutoka Wizara na Idara zinazojitegemea. Aidha, Maafisa Wadhamini wote wameshiriki katika mafunzo haya;

iv) Kuifanyia marekebisho *Data base* ya mishahara ili iweze kutumika kwa wafanyakazi wa Taasisi za Serikali zinazopata ruzuku za mishahara. Aidha, marekebisho haya yanajumuisha kutoa ripoti ya mshahara kwa kila mfanyakazi;

v) Kuziwezesha taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha kutekeleza majukumu yao kwa kuzipatia ruzuku kwa wakati;

vi) Kuhakikisha marekebisho ya mishahara ya watumishi wa Serikali yanafanyika kwa ukamilifu na kwa mujibu wa Bajeti Kuu ya Serikali; na

vii) Kuandaa bajeti ya programu na viashiria vya kupima utekelezaji kabla ya mfumo kuanza kutumika rasmi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara inaombewa jumla ya TZS 26,724.870 milioni, zikiwemo TZS 8,500 milioni kwa ajili ya marekebisho ya mishahara Serikalini, TZS 17,452.30 milioni kwa ajili ya ruzuku kwa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na TZS 772.572 milioni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya idara.

Mhe. Mwenyekiti, mambo yaliyopangwa kutekelezwa na idara hii katika mwaka 2014/15 ni yafuatayo:

i) Kutayarisha na kutoa mwongozo wa bajeti kwa wizara na taasisi husika za Serikali hadi kufikia Disemba, 2014 kwa ajili ya matayarisho ya bajeti ya mwaka 2015/16;

ii) Kuwajengea uwezo juu ya Mfumo wa Bajeti unaozingatia Programu *(PBB)* Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi, Baraza la Wawakilishi, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Maidara ya SMZ na Wakuu wa Taasisi za Kijamii *(CSO);*

iii) Kuandaa vitabu vya bajeti ya mwaka 2015/16 kwa ajili ya mjadala wa Baraza la Wawakilishi;

iv) Kuziwezesha taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha kutekeleza majukumu yao kwa kuzipatia ruzuku kwa wakati;

v) Kuendelea kufanya marekebisho ya mishahara ya watumishi wa Serikali kwa mujibu wa mwongozo wa Utumishi;

vi) Kufanya tathmini ya usimamizi na utekelezaji wa malipo ya mishahara ya watumishi wa umma;

vii) Kufuatilia matumizi ya fedha za umma zikiwemo fedha za matumizi ya kazi za kawaida na kazi za maendeleo;

viii) Kutathmini uandaaji na uwasilishaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2014/15; na

ix) Kutayarisha taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali.

IDARA YA MHASIBU MKUU WA SERIKALI

Mhe. Mwenyekiti, jukumu la idara hii ni utunzaji wa mapato, udhibiti wa matumizi pamoja na kusimamia shughuli za Wahasibu na Wakaguzi wa ndani. Kwa mwaka 2013/2014, Idara ilitengewa jumla ya TZS 3,183.57 milioni kwa kazi za kawaida. Aidha, matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali ilitengewa jumla ya TZS 66,056.00 milioni.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Mei, 2014, Idara imetumia jumla ya TZS 2,825.23 milioni sawa na asilimia 89 ya makadirio kwa kazi za kawaida. Aidha, matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali yamefikia jumla ya TZS 61,100 milioni sawa na asilimia 93 ya makadirio.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2013/2014, Idara ilitekeleza mambo yafuatayo:

i) Kusimamia na kudhibiti ukusanyaji wa mapato ikiwemo kuchapisha vitabu 20,000 vya risiti za Serikali ambavyo vimewekewa alama maalumu;

ii) Kudhibiti matumizi ya Serikali ikiwemo kuratibu vikao kumi na moja (11) vya Kamati ya ukomo kwa lengo la kugawa rasilimali fedha kwa wizara na idara zinazojitegemea bila ya kuathiri hali ya fedha za Serikali;

iii) Kuwajengea uwezo wa usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi 51 wa kada ya Uhasibu na Ukaguzi wa Ndani wa Mawizara na Maidara;

iv) Kufunga hesabu za Serikali za mwaka 2012/13 kwa kuzingatia viwango vya Kimataifa vya uandaaji wa taarifa za hesabu katika sekta ya umma na taarifa mjumuisho kuwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

v) Kusimamia Deni la Taifa kwa kutoa kipaumbele katika ulipaji wa madeni kwa wakati ili kuepuka malimbikizo ya riba. Katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Mei, 2014 malipo ya riba yamefikia TZS 2,679.884 milioni;na

vi) Kusimamia marekebisho ya awali ya Sheria ya Fedha za Umma kwa kuratibu shughuli za Mshauri Elekezi wa kuandaa rasimu ya Sheria hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/2015, Idara inaombewa jumla ya TZS 3,297.457 milioni kwa kazi za kawaida na jumla ya TZS 69,825.10 milioni kwa ajili ya kusimamia matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali. Fedha hizo zinaombwa kwa ajili ya kutekeleza mambo yafuatayo:

i) Kusimamia na kudhibiti mapato kwa kuendelea kuchapisha vitabu 22,000 vya Risiti za Serikali zenye alama maalumu;

ii) Kusimamia, kudhibiti matumizi na hali ya Fedha za Serikali. Aidha, Idara itaratibu vikao vya kila mwezi vya kamati ya ukomo wa matumizi ili kufikia lengo;

iii) Kusimamia Deni la Taifa kwa kuendelea kulipa madeni ya ndani na nje kwa wakati na kushiriki vikao mbali mbali vya Kamati ya Wataalamu wa Deni la Taifa;

iv) Kuwajengea uwezo juu ya usimamizi na udhibiti wa fedha za umma kwa kuwadhamini katika mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi 80 wa kada ya uhasibu na ukaguzi wa ndani;

v) Kufunga hesabu za Serikali za mwaka 2013/14 kwa kuzingatia viwango vya Kimataifa vya uandaaji wa taarifa za hesabu katika sekta ya umma na majumuisho yake kuwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa wakati;

vi) Kukamilisha marekebisho ya Sheria ya Fedha za Umma na kuwasilishwa Baraza la Wawakilishi kwa mara ya kwanza;

vii) Kuzijengea uwezo Kamati za Ukaguzi za Wizara katika masuala ya ukaguzi na udhibiti wa ndani; na

viii) Kuwajengea uwezo wakaguzi wa ndani katika kufanya ukaguzi wa kiufundi kwa miradi inayotekelezwa katika taasisi zao; na kutayarisha miongozo ya udhibiti wa ndani, ukaguzi wa manunuzi na ukaguzi wa mikataba.

IDARA YA FEDHA ZA NJE

Mhe. Mwenyekiti, Idara Fedha za Nje ina jukumu la kutafuta misaada kutoka nje ya nchi na kuratibu mahusiano yetu na Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ilitarajiwa kuratibu na kusimamia upatikanaji wa misaada ya jumla ya TZS 275,411.0 milioni, zikiwemo TZS 86,797.0 milioni ni ruzuku, TZS 148,614.0 milioni ni mikopo na TZS 40,000 milioni za misaada ya kibajeti.

Mhe. Mwenyekiti, Katika kufanikisha upatikanaji wa fedha hizo, Idara katika mwaka 2013/2014, ilitengewa jumla ya TZS 173.90 milioni kwa kazi za kawaida. Hata hivyo, hadi kufikia Mei 2014, Idara imetumia jumla ya TZS 156.57 milioni sawa na asilimia 90 za makadirio kwa kazi za kawaida. Matumizi ya fedha hizo yanajumuisha ushiriki wa idara katika mikutano ya majadiliano ya Kimataifa na Kikanda yenye lengo la kutafuta misaada, mikopo nafuu na kuimarisha uhusiano uliopo. Aidha, idara iliandaa mikutano ya robo mwaka kwa Sekta ya Umma na Sekta binafsi kwa ajili ya kupata taarifa za misaada na mikopo na kuzifanyia uchambuzi.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Mei 2014, Idara imeweza kuratibu upatikanaji wa jumla ya TZS 187,551.0 milioni sawa na asilimia 68 ya makadirio kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa. Kati ya fedha hizo, TZS 42,713.0 milioni sawa na asilimia 49.21 ya makadirio kwa ajili ya misaada ya miradi, TZS 115,328 milioni sawa na asilimia 77.60 ya makadirio kwa ajili ya mikopo na TZS 29,510 milioni sawa na asilimia 73.77 ya makadirio ikiwa ni misaada ya kibajeti. Aidha, idara ilishiriki katika kutaarisha muongozo mpya wa ushirikiano wa maendeleo *(Development Co-operation Framework)* ambao utachukua nafasi ya Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania (MPAMITA) kwa lengo la kuleta ufanisi na kubainisha wajibu wa kila mdau wa maendeleo wakiwemo Raia.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Idara inaombewa jumla ya TZS 278.73 milioni kwa kazi za kawaida ili kutekeleza shughuli zifuatazo:

i) Kusimamia upatikanaji wa rasilimali kutoka nje inayotarajiwa kufikia TZS 306,040 milioni zikiwemo TZS 265,441.0 milioni kupitia programu na miradi mbali mbali ya maendeleo, TZS 40,000 milioni za misaada ya kibajeti (*GBS*) na TZS 600 milioni kutokana na msamaha wa madeni (*MDRI*). Kati ya fedha za *program* na miradi ya maendeleo, TZS 199,138.0 milioni ni mikopo na TZS 66,302 milioni ni ruzuku;

ii) Kuandaa mikutano ya robo mwaka kwa Sekta ya Umma na Sekta binafsi kwa ajili ya kupata taarifa za misaada na mikopo na kuzifanyia uchambuzi;

iii) Kushiriki mikutano ya Kimataifa na Kikanda kwa lengo la kuhakikisha kuwa rasilimali fedha zinapatikana kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, Mikutano hiyo husaidia katika kuimarisha uhusiano wetu na washirika wa Maendeleo;

iv) Kushiriki mikutano mbali mbali Tanzania Bara ikiwemo ya kazi za mtandao wa misaada (*APM*) na uimarishaji wa taarifa za misaada; na

v) Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa idara kwa kuwapatia mafunzo kazini.

IDARA YA UHAKIKIMALI NA MITAJI YA UMMA

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyoelewa idara ndio msimamizi wa mali zote za Serikali, manunuzi na uondoshwaji wa mali za umma na mitaji ya umma. Katika kutekeleza majukumu yake ya mwaka 2013/2014, Idara ilitengewa jumla ya TZS 502.70 milioni kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi Mei 2014, jumla ya TZS 401.51 milioni zilitumika sawa na asilimia 80 ya makadirio.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014 mambo yafuatayo yameweza kutekelezwa na idara:

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe, tumsikilize Mhe. Waziri ili tuweze kuchangia vizuri baadae. Mhe. Waziri, tuendelee.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti,

i) Kufanya uchambuzi wa tathmini ya kifedha kwa Mashirika manane yakiwemo Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*), Shirika la Bandari, Shirika la Bima, Benki ya watu wa Zanzibar, Shirika la Utalii, Shirika la Magari, Shirika la Umeme na Shirika la Meli;

ii) Kusimamia upatikanaji wa gawio kutokana na faida ya Mashirika ambapo jumla ya TZS 1,060 milioni zimekusanywa kama gawio kutoka Mashirika ya Bandari, Bima, *PBZ* na *ZSTC*. Gawio hilo ni ongezeko la asilimia 165 ikilinganishwa na TZS 400 milioni za mwaka 2012/13;

iii) Kuratibu na kusimamia ufufuaji wa Kiwanda cha Sukari Mahonda. Pamoja na matatizo kadhaa yaliyojitokeza, kwa mara ya kwanza tokea kusitisha uzalishaji mwaka 1997/98. Kiwanda katika mwaka wa fedha 2013/2014 kimeweza kuzalisha tani 150 za sukari kwa majaribio, wakati juhudi zaidi za kuimarisha zikiendelea;

iv) Kufanya ukaguzi wa manunuzi na uhakiki mali za Serikali katika Wizara 16 na Taasisi zake;

v) Kuondosha mali chakavu katika Wizara na Idara za Serikali ambapo hadi kufikia Mei 2014, jumla ya TZS 17.5 milioni zimekusanywa;

vi) Kuwajengea uwezo juu ya ukaguzi wa manunuzi na usimamizi wa mitaji ya umma kwa kuwadhamini watumishi wawili katika mafunzo ya muda mfupi;

vii) Kuwajengea uwezo juu ya uwekaji wa kumbukumbu katika daftari la mali za Serikali kwa kuwadhamini wafanyakazi 16 wa Wizara 5 ambazo tayari zimefanyiwa tathmini;

viii) Kufanya tathmini na hatimae kushauri Serikali kuyafunga Shirika la Magari na Shirika la Utalii. Serikali imeridhia kufungwa mashirika hayo na tayari Mheshimiwa Rais ametoa rasmi amri ya kuyafunga mashirika hayo kama sheria inavyoelekeza;

ix) Kusimamia majadiliano ya kurejesha mali za Kampuni ya *ZAPOCO* ambapo Serikali imeshakubaliana na wabia juu ya fidia ya kulipwa, ili mali hizo zirudi chini ya umiliki wa Serikali pekee. Kwa sasa, malipo ya fidia hiyo yanaendelea kwa mujibu wa mkataba na yanatarajiwa kukamilika ndani ya robo ya kwanza ya mwaka 2014/2015;

x) Kukusanya jumla ya TZS 328.0 milioni kutokana na ukodishwaji wa mitaji mbali mbali ya Serikali; na

xi) Kukamilisha hatua za awali za kuzitambua mali zitakazofanyiwa tathmini kwa wizara tatu (3); Wizara ya Kazi na Utumishi, Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa jamii, Wanawake na Watoto na Wizara ya Katiba na Sheria. Zoezi halikuweza kukamilika kutokana na kulazimika kulianza upya kulikosababishwa na mabadiliko ya muundo wa Wizara za Serikali yaliyofanywa Agost, 2013.

Mhe. Mwenyekiti, Idara itaendelea kusimamia, kudhibiti mali, mitaji na mashirika ya umma pamoja na kutoa muongozo wa ununuzi. Kwa mwaka 2014/2015, Idara inaombewa jumla ya TZS 535.558 milioni kwa kazi za kawaida. Fedha hizo ni kwa ajili ya kutekeleza mambo yafuatayo:

i) Kufanya uchambuzi na kutathmini masuala ya kifedha katika mashirika yote ya Serikali na mashirika ambayo Serikali imewekeza mitaji, ili kuhakikisha gawio la faida linapatikana;

ii) Kufanya ukaguzi wa utoaji wa zabuni na utekelezaji wa mikataba itokanayo na ununuzi wa mali za umma na kuhakiki mali za Serikali kwa Wizara 16 na Taasisi zake;

iii) Kuendelea kuondosha mali chakavu kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma;

iv) Kuwajengea uwezo juu ya utunzaji wa Daftari la Mali za Serikali kwa kuwadhamini katika mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi 30 wa Wizara na Idara zinazojitegemea;

v) Kufanya tathmini juu ya ufanisi wa ununuzi wa mali za umma;

vi) Kutoa mwongozo juu ya utaratibu wa kutoa taarifa ya ununuzi;

vii) Kuandaa Sera ya Mali za umma na utaratibu wa unnuzi wa mali za Umma;

viii) Kuimarisha usimamizi wa mashirika ya umma ili kuongeza mapato;na

ix) Kukamilisha urejeshaji wa mali za *ZAPOCO* Serikalini na ufungaji wa Shirika la Utalii na Shirika la Magari.

URATIBU WA MIPANGO NA UTAWALA

Mhe. Mwenyekiti, shughuli za Uratibu wa Mipango, Sera, Utafiti na Utawala katika Wizara yangu zinatekelezwa kupitia idara tatu (3) ambazo ni Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na Ofisi Kuu ya Pemba.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ndio yenye jukumu la kuhakikisha kuwepo kwa mazingira bora ya kazi na kusimamia huduma za *TEHAMA*, Sheria, Ununuzi na Ukaguzi wa ndani kwa Wizara ya Fedha.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara ilitengewa jumla ya TZS. 3,962.35 milioni kwa kazi za kawaida ambapo hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Mei, 2014, Idara imetumia jumla ya TZS 3,741.89 milioni sawa na asilimia 94 ya makadirio. Fedha hizo zimetumika katika kutekeleza shughuli mbali mbali zinazojumuisha mambo yafuatayo:

i) Kuwajengea uwezo wafanyakazi katika fani za Uhasibu, Fedha, Uchumi, *TEHAMA*, Rasilimali watu, Ununuzi na Ugavi kwa kuwadhamini watendaji wake 54 katika mafunzo ya muda mrefu na 20 mafunzo ya muda mfupi;

ii) Kuratibu shughuli za manunuzi kwa kuandaa vikao 12 vya Bodi ya Zabuni;

iii) Kusimamia maandalizi ya michoro ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Wizara Pemba, ambalo litashirikisha wizara tatu, ambazo ni Wizara ya Fedha, Wizara ya Uwezeshaji Ustawi wa Jamii, Wanawake na Watoto na Wizara nyengine itayopangwa na Serikali;

iv) Kuratibu vikao vya Wizara vya kupitia Sheria ya *ZIPA* na *ZSSF*. Aidha, idara ikishirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu iliandaa Mswada wa Sheria ya Fedha ya 2014/15 na mswada wa Sheria ya matumizi kwa mwaka 2013/14;

v) Kuratibu udhamini wa masomo kwa wanafunzi 1,366 katika vyuo mbali mbali nchini Tanzania katika fani za Uchumi, Fedha, Uhasibu, *TEHAMA*, Ununuzi na Ugavi;

vi) Kuhakiki madai mbali mbali ya Wwizara kabla ya kulipa; na

vii) Kuimarisha mazingiza ya kazi kwa kuajiri wafanyakazi 53 na kufanya ukarabati mdogo wa Ofisi na kununua vifaa vya ofisini.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Idara inaombewa jumla ya TZS 3,621.502 milioni kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yafuatayo:

i) Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Wizara kwa kuwapeleka katika mafunzo ya muda mrefu na mfupi;

ii) Kuwapatia likizo zao watendaji 90;

iii) Kuandaa mafunzo ya ndani kwa wafanyakazi 50 kwa lengo la kuelewa vizuri sheria mpya namba 2 ya Utumishi wa Umma;

iv) Kuwajengea mazingira bora ya kazi kwa kuwapatia watendaji maeneo mazuri ya kazi na vitendea kazi;

v) Kwa kushirikiana na Wizara ya Uwezeshaji Idara imeweza kukamilisha mchakato wa kumpata mkandarasi wa jengo la ofisi Pemba; na

vi) Kufanya Ukaguzi wa Mfumo wa ulipaji Mishahara.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ina jukumu la kuandaa sera na mipango inayohusu fedha na kodi na kusimamia utafiti katika sekta ya fedha. Kwa mwaka 2013/14, Idara ilitengewa jumla ya TZS 285.30 milioni kwa kazi za kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Mei 2014, Idara imetumia jumla ya TZS 201.81 milioni sawa na asilimia 71 ya makadirio kwa kutekeleza mambo yafuatayo:

i) Kuzifanyia mapitio Sheria ya *ZSSF* na *ZIPA* katika ngazi ya Wizara;

ii) Kuratibu utekelezaji wa majukumu ya Wizara na kuandaa ripoti za utekelezaji kwa vipindi vya robo mwaka, nusu mwaka na mwaka;

iii) Kuandaa mkutano mmoja wa masuala ya mtambuka kwa wafanyakazi wa wizara na taasisi zake;

iv) Kusimamia utendaji wa Bodi ya Rufaa ya Kodi kwa ajili ya kutatua migogoro ya walipa kodi, kesi nne zimesikilizwa ambapo kesi mbili zimetolewa maamuzi;

v) Kushiriki katika vikao sita vya majadiliano ya kikanda vikiwemo vya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*), Ukanda wa Bahari ya Hindi (*IOR*) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*), ili kutumia fursa za kiuchumi zilizopo na kulinda maslahi ya nchi;

vi) Kuratibu ujenzi wa meli mpya ya Serikali huko nchini Korea ya Kusini;

vii) Kukamilisha uandaaji wa Sera ya huduma za taasisi ndogo ndogo za kifedha (*Microfinance Policy)* katika ngazi ya Wizara; na

viii) Kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi na *programs* mbali mbali zinazotekelezwa na Wizara kwa lengo la kuhakikisha kuwa thamani ya fedha inapatikana katika miradi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/15, Idara inaombewa jumla ya TZS 463.464 milioni kwa kazi za kawaida kwa kutekeleza mambo yafuatayo:

i) Kuratibu utekelezaji wa bajeti na majukumu ya wizara na kuandaa ripoti mbali mbali za utekelezaji;

ii) Kuratibu uandaaji na kuzifanyia mapitio sera mbali mbali za wizara na taasisi zake;

iii) Kuratibu mapitio ya sheria ya udhibiti wa fedha haramu kwa kuandaa Kanuni na kushajihisha wadau juu ya udhibiti wa fedha hizo;

iv) Kuratibu uandaaji wa mfumo maalumu wa habari (*MIS*) utakaosimamia utunzaji wa taarifa za wizara, pamoja na utayarishaji wa ripoti za utekelezaji na bajeti ya wizara;

v) Kufanya utafiti wa kuangalia ukubwa wa Serikali na mashirika ya umma nchini;

vi) Kuratibu na kusimamia utendaji wa Bodi na Baraza la Rufaa ya kodi kwa ajili ya kutatua migogoro ya walipa kodi; na

vii) Kuandaa Sera ya uondowaji wa vifaa vichakavu Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia programu na miradi ya maendeleo ya wizara. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ilitengewa jumla ya TZS 25,000 milioni kama mchango wa Serikali katika kutekeleza programu tatu (3) na miradi sita (6) na TZS 17,448.403 milioni kama ruzuku na mikopo kutoka kwa washirika wa maendeleo. Mpaka kufikia mwezi Mei 2014, jumla ya TZS 12,069.043 milioni zilishapatikana kama mchango wa Serikali, sawa na asilimia 48 na TZS 11,143.926 milioni sawa na asilimia 64 kutoka kwa washirika wa maendeleo. Utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo ni kama ifuatavyo:

a) **Programu ya Usimamizi wa Fedha za Umma (*PFM*).**

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, programu hii ilitengewa jumla ya TZS 40.0 milioni ikiwa ni mchango wa Serikali. Hadi kufikia Mei 2014, programu imetumia jumla ya TZS 6.143 milioni sawa na asilimia 15 ya makadirio kwa shughuli za uratibu wa mradi na kutekeleza kazi zifuatazo:

i) Kuratibu vikao vya Kamati tendaji vya mradi;

ii) Kutayarisha ripoti za utekelezaji wa mradi na kuwasilisha kwa Washirika wa Maendeleo; na

iii) Kuhudhuria mikutano ya washirika wa Maendeleo Tanzania Bara.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa Fedha 2014/2015, programu hii inaombewa jumla ya TZS 20 milioni kama mchango wa Serikali ambazo zitatumika katika kuendeleza shughuli za uratibu wa mradi.

b) **Programu ya Mageuzi ya Msingi Usimamizi wa Fedha za Umma (*PFMRP*).**

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, programu hii ilipangiwa jumla ya TZS 500 milioni ikiwa ni mchango wa wafadhili. Hadi kufikia Mei 2014, Mradi umepatiwa TZS 29 milioni sawa na asilimi 6 ya makadirio na kukamilisha kazi zifuatazo:

(i) Kujenga uwezo kwa wakaguzi wa hesabu 46 kati ya hao 26 juu ya kutambua na kusimamia maeneo hatarishi *(Risk Based Management*) na 20 juu ya miongozo ya ukaguzi;

(ii) Ununuzi wa vitendea kazi vikiwemo Komputa 57 kwa ajili ya mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu (*CAG*) na Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuunganishwa na mtandao wa *IFMS*; na

(iii) Kusimamia na kuimarisha mfumo wa fedha wa *IFMS* kwa lengo la kuendana na mfumo wa *PBB* kwa kununua "*Server*" mpya ambayo itakuwa na uwezo wa kutoa taarifa za Bajeti kwa mfumo wa *PBB* .

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa Fedha 2014/2015, programu hii inaombewa jumla ya TZS 10 milioni kama mchango wa Serikali na TZS 2,630 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, ili kugharamia kazi zifuatazo:

i. Mafunzo ya uelewa juu ya sheria za fedha za umma, mfumo wa bajeti unaotumia programu (*PBB*) na Sheria ya Manunuzi kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi mipango, Wahasibu wakuu, Wakaguzi wa Ndani na maafisa Wadhamini;

ii. Kufanya tathmini ya mali za Serikali;

iii. Mapitio ya Sheria ya Mitaji ya Umma namba 4 ya mwaka 2002;na

iv. Kumtafuta mshauri elekezi atakaefanya kazi ya kuboresha mfumo wa Bajeti unaotumia Programu.

c) Programu ya Ujenzi wa Afisi za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 programu hii ilipangiwa jumla ya TZS 7,000 milioni ikiwa ni mchango wa Serikali. Hadi kufikia Mei 2014 programu imeweza kutumia jumla ya TZS 1,692.282 milioni sawa na asilimia 24 ya makadirio kwa ajili ya kusimamia malipo ya jengo la Katiba na Sheria lililopo Mazizini ambalo limefikia hatua za mwisho.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa Fedha 2014/2015, programu hii inaombewa jumla ya TZS 3,000 milioni ikiwa ni mchango wa Serikali kwa ajili ya usimamizi wa malipo ya ujenzi wa jengo la Wizara ya Fedha na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Wanawake na Watoto huko Pemba.

d) Mradi wa Uimarishaji wa Huduma za Mji (*ZUSP*).

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 50 milioni ikiwa ni mchango wa Serikali na TZS 15,200 milioni mkopo kutoka Benki ya Dunia. Hadi kufikia Mei 2014, mradi umeweza kutumia jumla ya TZS 38.62 milioni sawa na asilimia 77 kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kutayarisha nyaraka za mradi na kuwezesha kufanyika vikao sita (6) vya Bodi ya zabuni;

(ii) Kuratibu mikutano ya wadau ya kujadili ripoti za washauri elekezi;

(iii) Kufanya malipo ya ada ya TZS 3,216.02 milioni kwa washauri elekezi na wakandarasi kwa kazi mbali mbali za mradi;

(iv) Kuziwezesha taasisi (Manispaa na Baraza la Mji) zinazohusika na mradi kwa kuzipatia vifaa mbali mbali vikiwemo gari nane (8) za kuchukulia taka;na

(v) Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Baraza la Mji na Manispaa katika maeneo ya manunuzi, usimamizi wa Fedha, Miradi, sheria na Mipango miji.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa Fedha 2014/2015, mradi huu unaombewa jumla ya TZS 1,600 milioni kama mchango wa Serikali na TZS 10,611.176 milioni zinatarajiwa kutolewa na Benki ya Dunia kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:

i) Kufanya malipo ya fidia kwa waathirika wa mradi ya michirizi; na

ii) Kuendelea kufanya malipo kwa washauri elekezi pamoja na wakandarasi.

e) Mradi wa ujenzi wa Meli ya abiria ya Serikali:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa Fedha 2013/2014, Serikali ilitenga jumla ya TZS 17,000 milioni kwa ununuzi wa meli mpya ya abiria na mizigo ya Serikali ambapo hadi kufikia Mei 2014, Shilingi 10,048.392 milioni sawa na asilimia 59 zimeshatumika kulipia ujenzi wa meli awamu ya kwanza na ya pili.

f)Mradi wa ujenzi wa Meli ya Abiria ya Serikali

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali ilitenga jumla ya TZS 17,000 milioni kwa ununuzi wa meli mpya ya abiria na mizigo ya Serikali, ambapo hadi kufikia Mei 2014, Shilingi 10,048.392 milioni sawa na asilimia 59 zimeshatumika kulipia ujenzi wa meli awamu ya kwanza na ya pili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, idara inaombewa Serikali imetenga jumla ya TZS 20,000 milioni kwa ajili ya ujenzi wa meli mpya ya abiria.

g) **Ujenzi wa Maabara ya Kompyuta -*ZIFA***

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Chuo Cha Uongozi wa fedha (*ZIFA*) kilitengewa jumla ya TZS 200 milioni, ikiwa ni mchango wa Serikali kwa ajili kuendeleza ujenzi wa jengo ya maabara ya chuo. Hadi kufikia Mei 2014, mradi huu ulipatiwa kiasi cha TZS 100 milioni, sawa na aslimia 50 kwa ajili ya kufanya maandalizi ya awali ya ujenzi wa maabara. Hata hivyo, kutokana na eneo lililopatikana kwa ajili ya ujenzi kuwa dogo, mradi haujaweza kukamilika.

h) Mradi wa Kuimarisha Misaada Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, mradi huu ulipangiwa jumla ya TZS 5 milioni. Hadi kufikia Mei 2014, Mradi umepatiwa TZS 5.0 milioni sawa na asilimia 100 ambazo zilitumika kwa ajili ya kuwapatia mafunzo wafanyakazi wanane (8) katika fani ya ukusanyaji taarifa, ufuatiliaji na uchambuzi wa taarifa za misaada.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya TZS 10 milioni ikiwa ni mchango wa Serikali na TZS 326 milioni mchango wa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya kutekeleza yafuatayo:

(i) Kuimarisha utafutaji na utekelezaji wa misaada na kufanya uchambuzi wa taarifa za misaada;

(ii) Kuimarisha ushirikiano na uratibu wa misaada baina ya Washirika wa Maendeleo pamoja na Mashirika na Taasisi za Serikali;

(iii) Kushiriki mikutano na Wizara ya Fedha SMT juu ya kazi za mtandao wa misaada (*AMP*) na uimarishaji wa taarifa za misaada;

(iv) Kuendelea kusimamia malipo ya mshauri wa Uratibu wa Misaada; na

(v) Kujenga uwezo wa wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo kazini (*on job training*) na ya muda mfupi nje ya nchi kwa kuimarisha utendaji kazi wao.

i) Mradi wa Uimarishaji wa Utawala Bora Awamu ya Pili

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, mradi huu ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 55 milioni ikiwa ni mchango wa Serikali na TZS 1,088.403 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Mei 2014, mradi umeweza kutumia jumla ya TZS 55 milioni sawa na asilimia 100 mchango wa Serikali na jumla ya TZS 751.408 milioni sawa na asilimia 69 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kuratibu vikao vinne (4) vya Kamati tendaji ya mradi ambayo Wajumbe wake ni wakuu wa taasisi zinazofaidika na mradi; na

(ii) Kugharamia matangazo ya zabuni.

Kuendelea na mchakato wa zabuni wa kumpata mshauri elekezi ambae atafanya mapitio ya Sheria namba 9 ya Manunuzi ya mwaka 2005. Aidha, tathmini ya kiufundi imefanyika katika kumpata mshauri muelekezi;

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, mradi unaombewa jumla ya TZS 10 milioni kama mchango wa Serikali na jumla ya TZS 726.325 milioni kama mkopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:

(i) Kuomba fedha kwa ajili ya kumpata mshauri muelekezi wa kuifanyia marekebisho Sheria Namba 9 ya Manunuzi ya mwaka 2005;na

(ii) Kuwajengea uwezo wafanyakazi watano (5) katika fani ya uchumi na fedha kwa kudhamini mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

j) Mradi wa Kuimarisha Maeneo Huru Fumba

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, mradi ulipangiwa jumla ya TZS 150 milioni kwa lengo la kazi ifuatazo:

(i) Kukamilisha mpango wa matumizi ya ardhi kwa maeneo la Fumba. Katika mpango huo eneo hilo lenye ukubwa wa hekta 3,000 limegawanywa kama ifuatavyo:

a) Eneo la Vijiji vya makaazii – hekta 1,310;

b) Eneo la Uwekezaji – hekta 743.5; na

c) Eneo la akiba – hekta 946.5

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka fedha 2014/2015, mradi huu unaombewa kiasi cha TZS. 150 milioni ikiwa ni mchango wa Serikali, kwa ajili ya kutekeleza yafuatayo:

(i) Kuratibu shughui za Uwekaji njia kuu zenye urefu wa kilomita 10, kwa kiwango cha lami. na

(ii) Kuliendeleza eneo moja lenye ukubwa wa hekta 107 (*Industrial Parks*) kwa kuweka miundombinu ya maji na umeme, kwa ajili ya wawekezaji waliojitokeza ili kuwekeza miradi yao.

k) Mradi wa Kufanya tathmini ya mali za Serikali

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, mradi huu ulipangiwa jumla ya TZS 500 milioni. Hadi kufikia Mei 2014, Mradi umepatiwa TZS 123.599 milioni sawa na asilimia 25 ambazo zilitumika kwa kukamilisha hatua za awali za kuzitambua mali zitakazofanyiwa tathmini kwa wizara tatu (3); Wizara ya Kazi na Utumishi, Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto na Wizara ya Katiba na Sheria.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Miradi na Programu za Wizara ya Fedha kwa pamoja zinaombewa kiasi cha TZS 27,203 milioni ikiwa mchango wa Serikali na TZS 14,293.501milioni ni mchango kutoka Washirika wa Maendeleo.

B.3 OFISI KUU - PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi Kuu Pemba ndio inayotekeleza shughuli zote za wizara kwa upande wa Pemba. Kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014 Ofisi ilitengewa jumla ya TZS 825.10 milioni kwa kazi za kawaida, ambapo mpaka kufikia mwezi Mei 2014, Ofisi imepatiwa jumla ya TZS 812.0 milioni sawa na asilimia 98 ya makadirio. Shughuli zilizofanywa katika utekelezaji wa majukumu hayo ni kama zifuatazo:

i) Kuweka mazingira mazuri ya kazi na kuongeza ufanisi kwa kukarabati ofisi na kununua vifaa vya ofisi;

ii) Kuimarisha huduma za mtandao wa *IFMS*;

iii) Kuratibu upatikanaji wa mafunzo kwa wafanyakazi katika fani mbali mbali, ambapo jumla ya wafanyakazi 15 wakiwemo wanawake watano (5) na wanaume (10) walipatiwa mafunzo ikiwemo Shahada ya Pili ya usimamizi wa fedha (2): Shahada ya Pili ya Uchumi (1): Stashahada ya Uzamili ya Uhasibu (1); Shahada ya Kwanza ya Uhasibu (5): Shahada ya Kwanza ya Ununuzi na Ugavi (5); na Shahada ya Kwanza ya Utawala wa Biashara (1);

iv) Kufanya ukaguzi wa shughuli za manunuzi ya vifaa na huduma katika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano: Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko: Wizara ya Afya: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali: Mamalaka ya Maji (*ZAWA*): Baraza la Mji Chake Chake na Baraza la Mji Mkoani;

v) Kufanya ukaguzi juu ya Matumizi ya Daftari la kumbukumbu za mali za kudumu katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskszini (P), Wizara ya Kilimo na Maliasili, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Afya na Wizara ya Fedha, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) na Halmashauri ya Wilaya ya Wete;

vi) Kutoa mafunzo juu ya matumizi bora ya Daftari la kumbukumbu za mali za kudumu (*Fixed Assets Register*) kwa wizara tisa (9) kwa Maafisa wa Mipango na waangalizi wa Ofisi;

vii) Kutoa ushauri juu ya utendaji wa Bodi za zabuni za Mikoa ya Pemba na vitengo vya manunuzi kwa Wizara na Tasisi za Serikali;

viii) Kuratibu na kusimamia malipo ya viinua mgongo na pencheni kwa wastaafu wanaopokelea pencheni zao Ofisi kuu Pemba;

ix) Kufanya ukaguzi wa shughuli za kiuhasibu pamoja na kutoa ushauri wa mfumo wa ukusanyaji wa mapato yanayotokana na Wizara na Taasisi za Serikali;

x) Kuwapatia mafunzo na kuwaweka tayari watumiaji wapya wa mtandao wa *IFMs*, ambapo jumla ya watendaji kumi na tano (15) wa kada ya uhasibu walipatiwa mafunzo hayo;

xi) Ufuatiliaji wa hati za Serikali (*Counterfoil*) na kupatiwa Wizara na Taasisi za Serikali kwa mujibu wa taratibu;na

xii) Kuwapatia mafunzo wafanyakazi wote wa Ofisi kuu Pemba juu ya masuala ya Shughuli Mtambuka.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 Ofisi ya Fedha Pemba inaombewa jumla ya TZS 1,146.119 milioni ili kuweza kutekeleza majukumu yafuatayo:

i) Kuendelea kuandaa mazingira bora ya kazi na kuleta ufanisi na huduma bora katika kazi;

ii) Kuendelea kufanya uhakiki wa mali za Serikali na kufanya ukaguzi wa manunuzi katika Wizara na Taasisi zote za Serikali zilizopo Pemba;

iii) Kuendelea kusimamia na kuimarisha shughuli za uhasibu Serikalini kwa upande wa Pemba;

iv) Kuendelea kuratibu na kusimamia malipo ya viinua mgongo na pencheni kwa wastaafu wanaopokelea pencheni zao Wizara ya Fedha Ofisi kuu Pemba;

v) Kuendelea kuratibu upatikanaji wa nafasi zaidi za masomo kwa wafanyakazi wake katika ngazi na fani mbali mbali;

vi) Kuendelea kushirikiana na Idara ya Uendeshaji na Utumishi kuanza rasmi ujenzi wa Ofisi mpya Pemba;

vii) Kuendeleza kusimamia uthibiti wa fedha za umma kwenye mapato na matumizi na usimamizi wa mali za Serikali na Taasisi zake pamoja na kutoa huduma za Uhasibu na Ukaguzi;

viii) Kuwapatia mafunzo na kuwaweka tayari watumiaji wapya wa mtandao wa *IFMS* kwa Wizara na Taasisi za Serikali, pamoja na Ufuatiliaji na upatikanaji wa hati za Serikali (*Counterfoils*);

ix) Kupokea na kuziwasilisha taarifa za mgao wa fedha za Wizara na Idara za Serikali kupitia mtandao wa *IFIMs*;

x) Kuendelea kuwapatia mafunzo wafanyakazi wote wa Ofisi kuu Pemba pamoja na Taasisi zake kuhusiana masuala ya shughuli za mtambuka pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa;

xi) Kuratibu majadiliano ya bajeti kwa vikundi vya jamii na taasisi zisizo za kiserikali Pemba;

xii) Kuratibu upatikanaji wa mafunzo ya programu ya bajeti (*PBB*) kwa maafisa wadhamini, wakuu wa maidara na wakaguzi wa ndani wa hesabu; na

xiii) Kuratibu shughuli za kuandaa *MTEF* kulingana na bajeti itumiayo programu ya (*PBB*) kwa wizara na Taasisi za Serikali.

C. TAASISI ZA FEDHA ZINAZOJITEGEMEA

Mhe. Mwenyekiti, kwa muundo wa sasa wa Serikali, Wizara ya Fedha inasimamia taasisi nane (8) zinazojitegemea. Taasisi hizo ni Bodi ya Mapato Zanzibar, Mamlaka ya Mapato Tanzania - Zanzibar, Mfuko wa Barabara, Mamlaka ya Ukuzaji wa Vitega Uchumi, Chuo cha Uongozi wa Fedha, Shirika la Bima Zanzibar, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na Benki ya Watu wa Zanzibar.

C.1 BODI YA MAPATO ZANZIBAR (*ZRB*)

Mhe. Mwenyekiti, Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) ina jukumu la kukusanya mapato ya ndani ya Serikali Kuu Zanzibar. Kwa mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Bodi ya Mapato ilikadiriwa kukusanya jumla ya TZS 171,700 milioni, ambapo makusanyo halisi hadi Mei 2014, ni jumla ya TZS 165,887 milioni sawa na asilimia 97 ya lengo lililowekwa. Kati ya makusanyo hayo, jumla ya TZS 150,545 milioni zinatokana na vianzio vya kodi ambapo ni sawa na asilimia 90.7 ya makusanyo na jumla ya TZS 15,342 milioni zinazotokana na mapato ya mawizara sawa na asilimia 9.3 ya makusanyo. Makusanyo haya kwa kipindi hiki ni ziada ya TZS 33,320 milioni ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka 2012/2013 ya TZS 132,567 milioni sawa na ongezeko la asilimia 25. Aidha, hii inaonesha ukusanyaji wa wastani wa TZS 15,080 milioni kwa mwezi kwa mwaka 2013/14 ikilinganishwa na wastani wa TZS 12,051 milioni kwa mwezi kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Bodi ya Mapato ilipanga kutumia jumla ya TZS 8,693 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Mei 2014, Bodi ya Mapato ilitumia jumla ya TZS 7,703 milioni sawa na asilimia 88.61 ya makadirio. Katika kipindi hicho, *ZRB* imeweza kufanya yafuatayo:

i) Kuzipitia na kuzifanyia marekebisho sheria mbali mbali zinazohusika na usimamizi wa ukusanyaji wa mapato kupitia sheria namba 10 ya mwaka 2013. Sheria hizo ni Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*), Ushuru wa Stempu, Sheria ya usajili wa vyombo vya moto, Sheria ya Ada ya Bandari, Sheria ya kodi ya mafuta na kodi za ardhi;

ii) Kuwaelimisha na kuwahamasisha walipa kodi juu ya umuhimu wa kulipa kodi kwa wakati na umuhimu wa kudai risiti wanapofanya manunuzi. Jumla ya semina kumi na tano (15), mikutano sita (6), vipindi vya redio 21, vipindi vya *TV* 10 na matangazo sita (6) ya aina mbali mbali yalitolewa; na

iii) Kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu wafanyakazi katika fani mbali mbali kwa lengo la kukuza utaalamu utakaopelekea kuongeza ufanisi. Jumla ya wafanyakazi sita (6) wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu katika vyuo mbali mbali, wafanyakazi kumi na saba (17) wamehudhuria semina au mafunzo nje ya nchi na wafanyakazi sabiini na tano (75) wamehudhuria semina mbali mbali ndani ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, Bodi ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2014/2015 inaombewa rukuzu ya jumla ya TZS 8,300 milioni ili kutekeleza malengo yake yafuatayo:

i) Kukusanya jumla ya TZS 199,700.00 milioni kutokana na vyanzo vya kodi na mapato yasiyo ya Kodi;

ii) Kuendelea kuimarisha miundombinu ya mtandao wa (*ICT*) na utendaji kazi;

iii) Kushajihisha ulipaji kodi wa hiari na kutoa huduma bora kwa walipakodi; na

iv) Kuweka mazingira bora ya kufanyakazi kwa kununua vitendeakazi na kuwajengea uwezo watendaji katika masuala ya fedha, kodi,*TEHAMA*, utawala kwa kuwadhamini katika mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

C.2 MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (*TRA*)

Mhe. Mwenyekiti, Jukumu la Mamlaka ya mapato (*TRA*) ni kukusanya mapato yatokanayo na vianzio vya Muungano ikiwemo Ushuru wa Forodha, Ushuru wa Bidhaa na Kodi ya Mapato ya Ndani. Ofisi ya *TRA* Zanzibar ilipangiwa kukusanya TZS 147,900.00 milioni. Idara ya Forodha na Ushuru ilipangiwa kukusanya jumla ya TZS 98,793 milioni sawa na asilimia 67 ya makadirio na Idara ya Kodi za Ndani ilipangiwa kukusanya TZS 49,107 milioni sawa na asilimia 33 ya makadirio.

Mhe. Mwenyekiti, makusanyo halisi hadi kufikia mwezi Mei, 2014 ni TZS 122,934 milioni sawa na asilimia 98 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha zilizokusanywa Idara ya Forodha iliweza kukusanya TZS 79,042.2 milioni, sawa na asilimia 64.6 ya mapato yote yaliokusanywa na asilimia 80 ya makadirio. Aidha, Idara ya Kodi za Ndani imemudu kukusanya jumla ya TZS 43,891.8 milioni, sawa na asilimia 35.4 ya mapato yote ya *TRA* na aslimia 89 ya lengo la makadirio.

Mhe. Mwenyekiti, Pamoja na kutofikia lengo lililowekwa, utendaji wa *TRA* unabainisha ukuaji mkubwa wa asilimia 28 ikilinganishwa na ukusanyaji wa TZS 95,768.4 milioni zilizokusanywa kwa kipindi kama hicho mwaka 2012/2013. Idara ya forodha ndio iliyoripoti ongezeko kubwa zaidi la asilimia 34 katika kipindi hicho.

Kwa kiasi kikubwa mafanikio haya yamechangiwa na kupungua kwa aslimia 47 kwa misamaha ya kodi kutoka TZS 33,370.0 milioni iliyotolewa kipindi kama hicho mwaka 2012/2013 sawa na asilimia 35 ya makusanyo ya kipindi hicho ikilinganishwa na misamaha ya TZS 17,560.0 milioni iliyotolewa hadi Mei 2014, sawa na asilimia 14 ya makusanyo.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*). Ofisi ya Zanzibar imepangiwa kukusanya TZS 166,056 milioni, sawa na ongezeko la asilimia 24 ya matarajio ya kukusanya TZS 134,000 milioni hadi June 2014.

C.3 MFUKO WA BARABARA

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha wa 2013/14, Mfuko wa Barabara umeendelea na jukumu lake la usimamizi wa fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara kwa dhamira ya kuwa na miundombinu endelevu.

Mhe. Mwenyekiti, Mfuko wa Barabara katika mwaka wa fedha 2013/2014, ulitarajia kupokea makusanyo ya jumla ya TZS 6,903 milioni zikiwemo TZS 6,046 milioni kwa ajili ya mategenezo ya barabara na TZS 857 milioni kwa uendeshaji wa Mfuko. Hadi kufikia mwezi Mei 2014, jumla ya TZS 6,045 milioni sawa na asilimia 88 ya makadirio ya mwaka zimeweza kuingizwa. Kati ya Fedha hizo, jumla ya TZS 3,402 milioni sawa na asilimia ya 49 ya fedha zilizopatikana zilishatumika, ambapo TZS 3,577 milioni zililipwa kwa kazi za barabara sawa na asilimia 59 ya makadirio na TZS 679 milioni sawa na asilimia 87 kwa kazi za uendeshaji wa mfuko.

Mhe. Mwenyekiti, ndani ya kipindi hicho, Mfuko umeweza kutekeleza yafuatayo:

i. Kukamilisha kwa wakati ufungaji wa hesabu pamoja na kukamilisha ukaguzi wa fedha na ufundi kwa mwaka 2012/2013;

ii. Kukagua na kutathmini matengenezo ya barabara yanayofanywa na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kama yanalingana na uhalisia wa fedha zinazotolewa;

iii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa mfuko kwa kuwadhamini katika mafunzo ya muda mfupi;

iv. Kuendesha semina kwa wadau mbali mbali kuhusu kazi za Mfuko na majukumu ya taasisi nyengine katika utunzaji wa barabara;

v. Kuendelea na matengenezo ya bustani ya maegesho ya magari mbele ya jengo la ofisi ya mfuko;

vi. Kuandaa Mpango Mkakati wa Mfuko wa miaka mitatu 2014/2015 – 2016/2017;

vii. Kuhudhuria mkutano wa mwaka wa Jumuiya ya Mifuko ya Barabara - Afrika (*ARMFA*) na mkutano wa Kanda ya Afrika Mashariki wa Jumuiya hio nchini Ethiopia kwa lengo la kubadilishana uzoefu;

viii. Kuandaa ripoti ya utekelezaji ya mwaka 2012/2013; na

ix. Kufanikisha maadhimisho ya kutimia miaka kumi (10) ya Mfuko wa Barabara;

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/2015, Mfuko unatarajia kupokea jumla ya TZS 7,108 milioni, ambapo TZS 7,102 milioni zikiwa ni kwa makusanyo yatokanayo na '*Road Development Levy'* na TZS 6.37 milioni kutokana na ukodishaji wa jengo. Kati ya fedha hizo jumla ya TZS 6,189 milioni zitatumika kwa kazi za matengenezo ya barabara na TZS 919 milioni kwa kazi za Uendeshaji wa Mfuko.

C.4 MAMLAKA YA UKUZAJI VITEGA UCHUMI ZANZIBAR (*ZIPA*)

Mhe. Mwenyekiti, jukumu la *ZIPA* ni kushajihisha wawekezaji wa nje na ndani ili kuwekeza nchini pamoja na kufanikisha uwekezaji huo. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Mamlaka ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 3,918.18 milioni ili kuweza kufanikisha utekelezaji wa shughuli za kawaida na maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Mei 2014, *ZIPA* ilifanikiwa kupata jumla ya TZS. 1,622.0 milioni sawa na asilimia 41 zikiwemo TZS 1,372.0 milioni kutokana na vianzio vyake na TZS 250.0 Milioni kama ruzuku kutoka Serikalini. Katika kipindi hicho, mambo yafuatayo yametekelezwa:

i. Kukamilisha zoezi la utafiti na mwendo wa mitaji binafsi na taarifa yake kuchapishwa, kusambazwa na kuwekwa katika tovuti ya *ZIPA*;

ii. Kuvutia na kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vidogo vidogo vikiwemo vya maziwa; usarifu wa mazao ya baharini na usindikaji wa mitungi ya gesi ya kupikia;

iii. Kuidhinisha Jumla ya miradi 28 kati ya maombi ya miradi 29 yalifanyiwa upembuzi. Kati ya hiyo, miradi 19 ni ya wageni na miradi 9 ni ya wenyeji. Sekta ya utalii imeendelea kuwa na miradi mingi, lakini pia, kumejitokeza miradi katika sekta ya ujenzi wa majengo ya biashara katika eneo la Fumba; na

iv. Kuendelea kutangaza fursa za uwekezaji ndani na nje ya nchi kwa kutumia njia mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Mamlaka imepanga kukusanya na kutumia TZS. 2,968.0 Milioni, kati ya hizo TZS. 1,496.0 milioni kutoka vianzio vya ndani, TZS. 250.0 ikiwa ni ruzuku na TZS. 671.0 milioni mchango wa washirika wa Maendeleo. Kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2014/15 ni kama ifuatavyo:

i. Kushajihisha wawekezaji wa ndani na nje kwa maeneo ambayo fursa bado zipo hususani za uvuvi na mazao ya baharini. Katika hili Mamlaka inakusudia kufanya kongamano maalum;

ii. Kuidhinisha miradi 50 ya uwekezaji kwa kutilia mkazo sekta ya viwanda vidogo vidogo, uvuvi, utalii wa mikutano na utalii wa michezo;

iii. Kufanya utafiti wa mwenendo wa Mitaji ya Uwekezaji (*Private Capital Flows*);

iv. Kufanya kongamano la ndani na wawekezaji wazalendo na wa kigeni ili kuwahamasisha kuzitumia fursa za uwekezaji zilizopo.

C.5 CHUO CHA UONGOZI WA FEDHA – *ZIFA*

Mhe. Mwenyekiti, Chuo cha Uongozi wa Fedha kinatoa mafunzo ya ngazi ya cheti, Stashahada na Shahada katika ya fani ya fedha na fani zinazolingana, zikiwemo Uhasibu, Fedha na Benki, Manunuzi na Ugavi na *TEHAMA*. Aidha, Chuo kinajihusisha na kutoa huduma za ushauri, kufanya tafiti na kutoa mafunzo mafupi katika fani mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Chuo kilikadiria kukusanya jumla ya TZS 2,675.87 milioni kutokana na ada na huduma inazozitoa na mkopo wa TZS 800.00 milioni kutoka *ZSSF*. Aidha, Chuo kiliidhinishiwa ruzuku ya TZS 1,800.00 milioni kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi Mei 2014, Chuo kimekusanya kiasi cha TZS 2,400.61 milioni kutokana na ada za masomo, huduma nyenginezo na ruzuku ya TZS 1,943.2 milioni kwa kazi za kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha hadi kufikia Mei 2014, Chuo kimetekeleza shughuli zifuatazo:

i) Kufanya mapitio ya mitaala katika fani za Stashahada ya Uongozi wa Fedha-Uhasibu, Stashahada ya Ununuzi na Ugavi na Stashahada ya *TEHAMA;*

ii) Kuongeza idadi ya programu, ambapo mpaka sasa mtaala wa Stashahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Fedha umekamilika;

iii) Kufanya tathmini ya ndani ya kila programu (*Self -Review Study*) kwa ajili ya ithibati endelevu;

iv) Kufanya manunuzi ya vifaa vya kisasa vya kufundishia pamoja na vitabu vya kiada na ziada (500);

v) Kuwawezesha wafanyakazi kumi na mbili (12) na walimu thelathini na nne (34) kwenda kwenye mafunzo mafupi na ya kitaalamu;

vi) Kuendesha mafunzo ya matumizi ya *TEHAMA*, kutoa taaluma juu ya njia na mbinu bora za ufundishaji na Utafiti kwa walimu wake;

vii) Kufanya usajili wa wanafunzi wapya 650 katika ngazi ya Cheti, Diploma, Shahada ya kwanza na Stashahada ya Uzamili na hatimae kufundisha na kuwatahini wanafunzi 1,165 katika fani mbali mbali;

viii) Kuandaa na kufanya mahafali ya kumi (10) ya chuo ambapo wanafunzi 513 walihitimu katika fani mbali mbali wakiwemo wanafunzi 187 ngazi ya cheti, Stashahada ya kawaida 238, Stashahada ya juu 1, Stashahada ya Uzamili 40 na Shahada ya kwanza wanafunzi 47;

ix) Kuwapeleka wafanyakazi wanne wa kada ya Utawala kwenye mafunzo ya muda mrefu;

x) Kuwawezesha walimu sita (6) kwenda katika mafunzo ya Shahada ya Uzamivu (*PhD*) na mwalimu mmoja (1) kwenda katika mafunzo ya Shahada ya Uzamili;

xi) Kuchangia shughuli za Maendeleo kwa wana jamii ikiwemo kununua vitabu vya kusaidia shughuli za kitaaluma Skuli za Chwaka na kuendesha mafunzo ya ujasiriamali kwa wadau wa Chwaka na maeneo ya karibu;

xii) Kuendesha mafunzo sita (6) ya kuongeza uwezo wa utendaji na mihadhara miwili (2) ya kitaalamu;

xiii) Kuendelea kufanya utafiti mmoja (1) kuangalia fursa za ukuzaji uchumi kupitia kilimo cha mwani kwa vijiji vya mwambao;

xiv) Kuendeleza mchakato wa kuanzisha kituo cha kulea wajasiriamali *(Incubation Centre)* na kutoa ushauri wa kitaalamu katika Taasisi sita (6) za Serikali na binafsi; na

xv) Kimeandaa na kuchapisha Jarida la Uchumi *(Zanzibar Economic Bulletin)* kwa kuadhimisha miaka 50 ya Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Chuo kimekadiria kukusanya jumla ya TZS 1,986.05 milioni kutokana na ada na huduma inazozitoa. Aidha, Chuo kinaombewa ruzuku ya TZS 1,800.3 milioni kwa kazi za kawaida. Mambo yaliyopangwa kutekelezwa na chuo ni haya yafuatayo:

i) Kufanya mapitio ya mitaala ya Shahada ya Kwanza (Uhasibu, *TEHAMA* na Ununuzi);

ii) Kuongeza idadi ya programu; Shahada ya Uzamili ya Fedha, Cheti cha Bima na Kodi na Kuimarisha kitengo cha ubora *(Quality Assurance Unit);*

iii) Kufanya manunuzi ya vitabu vya kiada na ziada (400);

iv) Kupeleka wafanyakazi kumi (10) na walimu 30 kwenye mafunzo mafupi na ya kitaalamu;

v) Kutoa mafunzo kwa walimu yakiwemo matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na utafiti;

vi) Kuimarisha mtandao wa mawasiliano kwa kujiunga na Mkonga wa mawasiliano *(fibre optic cable);*

vii) Kuimarisha Mfumo wa uwekaji taarifa za kitaaluma (*Academic Computerized System);*

viii) Kusajili wanafunzi wapya 700, ngazi ya cheti, Stashahada ya kawaida, Shahada ya Kwanza na Stashahada ya Uzamili;

ix) Kuandaa na kufanya Mahafali ya 11 ya chuo ambayo wanafunzi 632 wanatarajiwa kuhitimu;

x) Kufanya uajiri wa wafanyakazi kumi na moja (11);

xi) Kupeleka wafanyakazi watano wa kada ya utawala kwenye mafunzo ya muda mrefu (watatu wanaendelea na wawili wapya) na walimu wawili katika mafunzo ya muda mrefu ya Shahada ya Uzamili*;*

xii) Kukitangaza Chuo kupitia vyombo vya habari na njia nyenginezo na kutayarisha Mukhtasari wa Chuo *(Prospectus);*

xiii) Kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wadau kwa wilaya mbili za Unguja na mbili za Pemba;

xiv) Kutoa mafunzo 6 ya kuongeza uwezo wa utendaji na mihadhara miwili ya kitaalamu;

xv) Kufanya tafiti 2 za Kitaifa; moja inayoendelea na moja mpya;

xvi) Kuendeleza kituo cha kulea wajasiriamali na kutoa ushauri wa kitaalamu katika taasisi sita (6) za Serikali na binafsi;

xvii) Kuandaa na Kuchapisha Majarida Mawili; Jarida la *ZIFA* na Jarida la Uchumi;

xviii) Kufanya Mapitio ya uwezo wa taasisi kwa kuandaa Mpango Mkakati wa Chuo (2015-2020);

xix) Kugharamia masomo ya walimu saba (7) kwenye Shahada ya Uzamivu; watano (5) wanaendelea na wawili (2) wapya;

xx) Kufanya matengenezo ya dakhalia ya wanawake kwa ajili ya Zahanati; na

xxi) Kufanya manunuzi ya jenereta, kwa matumizi ya chuo.

SHIRIKA LA BIMA LA ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Bima la Zanzibar ni moja kati ya Mashirika ya Serikali yaliyoanzishwa baada ya Mapinduzi likiwa na lengo la kutoa huduma za BIMA kwa ujumla. Katika mwaka wake fedha 2013, Shirika lilikadiria kukusanya jumla ya TZS. 12,370 milioni kutokana na vianzio vyake mbali mbali vya mapato. Hadi kufikia Disemba 2013 Shirika liliweza kukusanya TZS 12,983 milioni sawa na ziada ya asilimia 5 ya makadirio ya mwaka. Kwa upande wa matumizi, Shirika lilipanga kutumia jumla ya TZS 3,854 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 692 milioni kwa matumizi ya kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Disemba 2013 Shirika lilishatumia jumla ya TZS 3,800 milioni kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 98.6 ya makadirio na TZS 278 milioni kwa kazi za Maendeleo sawa na asilimia 40 ya makadirio. Mbali ya fedha za uendeshaji, Shirika limetumia jumla ya TZS 4,046 milioni kuwalipa wateja waliopata ajali katika bima mbali mbali ambapo asilimia 98 ya madai hayo ni madai ya ajali za gari.

Mhe. Mwenyekiti, Katika kipindi cha mwaka 2014 Shirika linakadiria kukusanya jumla ya TZS 14,976 milioni kutokana na vianzio mbali mbali vya mapato. Makadirio haya ya mapato yameongezeka kwa asilimia 15 ukilinganisha na mapato halisi ya mwaka uliopita. Aidha, Shirika linatarajia kutumia jumla ya TZS 5,109 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 1,057 milioni kwa kazi za maendeleo. Kwa mwaka 2014, Shirika limejiwekea kutekeleza yafuatayo:

i) Kuendelea kutoa huduma za BIMA kwa ufanisi na kwa kuhimili ushindani katika maeneo yote ambayo Shirika lina ofisi;

ii) Kuanza kutoa huduma ya bima ya Kiislamu ambayo inasubiriwa na wengi;

iii) Kuongeza mapato yake kwa asilimia 15;

iv) Kuanza kutoa huduma ya BIMA ya Afya;

v) Kujenga uwezo kwa watendaji wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi katika kuongeza ufanisi na utoaji wa huduma bora.

MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (*ZSSF*)

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ilianzisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Zanzibar kwa lengo la kuwa na utaratibu endelevu kwa kulipa mafao ya uzeeni kama sehemu ya hifadhi ya jamii. Lengo hili lina timizwa kwa kusajili

wanachama, kukusanmya michango yao, kuwekeza fadha hizo katika miradi yenye tija na hatimae kutoa mafao kwa wanachama muda unapofikia. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Mfuko umetekeleza kazi zifuatazo:

i. Kusajili waajiri 99 dhidi ya lengo la kusajili waajiri 85 sawa na asilimia 117. Wanachama waajiriwa waliosajiliwa ni 4,142 dhidi ya lengo la kusajili waajiriwa 4,000 sawa na asilimia 104;

ii. Kusajili wanachama 2,219 kupitia Mfumo wa uchangiaji wa Hiari *(Zanzibar Voluntary Social Security Scheme)* dhidi ya lengo la kusajili wanachama 2,500 ambapo jumla ya TZS 75.5 milioni zimekusanywa;

iii. Kulipa mafao ya jumla ya TZS 7,100 milioni ya lengo la kulipa mafao ya TZS 5,853 milioni sawa na asilimia 122;

iv. Kukusanya michango ya wanachama yenye jumla ya TZS 19,532 milioni dhidi ya lengo la kukusanya TZS 24,000 milioni sawa na asilimia 81.3;

v. Kuendeleza ujenzi wa kiwanja cha kufurahishia watoto cha Uhuru (Kariakoo) na kuanza matayarisho ya ujenzi wa kiwanja cha kufurahishia watoto cha Umoja (Tibirinzi) Pemba; na

vi. Kuwekeza katika maeneo ya muda mrefu na ya muda mfupi, zikiwemo dhamana za Serikali, hati fungani za Serikali, hesabu za muda maalum, ununuzi wa hisa pamoja na mikopo, ambapo jumla ya TZS 15,000 milioni zimekusanywa kutokana na uwekezaji huo, dhidi ya lengo la TZS 12,300 milioni.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Mfuko unatarajia kufanyakazi zifuatazo:

i. Kuongeza wigo wa kusajili wanachama na kutumia mfumo wa uchangiaji wa hiari pamoja na kuimarisha ukaguzi wa taasisi mbali mbali za binafsi;

ii. Kukusanya jumla ya TZS 40,000 milioni kutoka kwa wanachama, pamoja na kulipa mafao yenye jumla ya TZS 9,184 milioni kwa wanachama wa mfuko;

iii. Kuimarisha mfumo ya uwekezaji taarifa na kumbukumbu za wanachama pamoja na kutoa kadi mpya kwa wanachama;

iv. Kukamilisha zoezi la mageuzi ili kuufanya mfuko uwe endelevu ikiambatana na kuanza kutoa mafao ya uzazi *(maternity benefit)* kwa wanachama wanawake;

v. Kukamilisha ujenzi wa viwanja vya kufurahishia watoto cha Umoja (Tibirizi) Pemba, kiwanja cha Kariakoo cha Uhuru Unguja pamoja na ujenzi wa mnara wa kumbukumbu ya miaka 50 ya Mapinduzi; na

vi. Kuendeleza ujenzi wa nyumba za kisasa Mbweni na jengo la biashara Michenzani.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Mfuko umetenga jumla ya TZS 15,500 milioni katika utekelezaji wa kazi za uwekezaji kwa viwanja vya kufurahishia watoto, nyumba za kisasa Mbweni na Jengo la biashara Michenzani.

BENKI YA WATU WA ZANZIBAR LTD (*PBZ*)

Mhe. Mwenyekiti, *PBZ* ni Benki ya biashara hivyo ina jukumu la kupokea amana na kukopesha kwa wateja wake wanaohitaji pamoja na kutoa huduma mbali mbali za kibenki. Hadi kufikia Mei 2014, Benki ilitekeleza yafuatayo:

i. Kupokea amana za wateja zenye kiwango cha TZS 51,700 milioni sawa na asilimia 79 ya lengo lililowekwa la TZS 65,500 milioni. Amana za wateja sasa zimefikia TZS 280,057 milioni;

ii. Kutoa mikopo ya jumla ya TZS 89,512 milioni sawa na asilimia 116 ya lengo lililowekwa la TZS 77,115 milioni hadi kufikia Mei 2014. Mikopo kwa wateja mbali mbali sasa imefikia TZS 165,485 milioni;

iii. Kuongeza rasilimali za Benki kwa TZS 57,301 milioni ikilinganishwa na lengo la TZS 75,744 milioni. Rasilimali za benki kwa sasa zimefikia TZS 327,022 milioni;

iv. Kupata mapato ya TZS 31,607 milioni yanayotokana na huduma mbali mbali za kibenki ambayo ni sawa na asilimia 126 ikilinganishwa na makadirio ya TZS 500,103 milioni kufikia Mei 2014;na

v. Kulipa gawio la faida kwa Serikali lenye jumla ya TZS 443.0 milioni kwa mwaka 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu maendeleo ya Benki ya Kiislamu ya *PBZ,* hadi kufikia tarehe 31 Mei 2014, Benki imeweza kupata jumla ya wateja 38,000. Amana za wateja za Benki ya Kiislamu ya *PBZ* zimefikia jumla ya TZS 60,733 milioni. Kwa upande wa mikopo inayofata misingi ya sheria za Kiislamu, Benki imeshatoa mikopo yenye thamani ya jumla ya TZS 16,724 milioni, ambapo wakopaji ni wafanyakazi wa Serikali, taasisi za Serikali na Makampuni binafsi. Benki imefungua tawi lake la nne na Makao Makuu ya Benki ya Kiislamu yaliopo Mpirani. Kwa ujumla huduma za benki ya Kiislamu zinakuwa kwa zaidi ya asilimia mia (100%) kila mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, Katika kipindi cha mwaka 2013/2014 benki imeanzisha huduma mbali mbali zikiwemo:

i. Kutoa mikopo ya nyumba ambayo inatoa fursa kwa wateja wa *PBZ* kupata makaazi bora;

ii. Kutoa huduma mbali mbali za kibenki kupitia mitandao ya simu na *internet;*na

iii. Kujiunga na mfumo wa haraka wa kusawazisha hundi *(Tanzania Automated Clearing House)*. Mfumo huu utawawezesha wateja wa benki kupata fedha zao siku moja badala ya muda wa sasa wa siku nne.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa mwaka 2014/2015 *PBZ* imekusudia kutekeleza yafuatayo:

i. Kuendeleza majukumu yake makuu ya kukusanya amana za wateja ambapo imepanga kukusanya *TZS* 318,491 milioni hadi kufikia Disemba 2014 na kutoa mikopo ya TZS 170,494 milioni hadi kufikia Disemba 2014;

ii. Kuongeza mapato yanayotokana na vianzio mbali mbali ya kiasi cha TZS 37,841 milioni hadi kufikia Disemba 2014;

iii. Kuanzisha matawi Mkoa wa Mtwara pamoja na kuongeza tawi jipya la *PBZ* maeneo ya TAZARA, Jijini Dar es Salaam;

iv. Kuanza ujenzi wa jengo jipya la Makao Makuu ambalo litaendana na hadhi ya Benki ya Watu wa Zanzibar *Ltd*;

v. Kujiunga na mitandao ya '*Mastercard'* na *'Union Pay'* ambayo itawawezesha wateja wa Benki ya Watu wa Zanzibar *Ltd* kupata huduma za kibenki popote pale duniani na pia Benki kuwa na uwezo wa kutoa huduma kwa wageni wanaokuja Zanzibar. Huduma hizi pia zitawezesha benki kuanzisha machine zinazoweza kupokea kadi kwa ajili ya kufanyia malipo 'Point of Sale' (*PoS*);

vi. Kuanzisha huduma za kufanyia malipo kwa njia ya electronic (E-shilingi) katika taasisi mbali mbali za Serikali na binafsi;

vii. Kuanzisha mikopo ya Wajasiriamali wadogo na wakati (*SME*);

viii. Kuanzisha mikopo ya Elimu ya juu kupitia Benki ya Kiislamu;

ix. Kuanzisha huduma za ukodishaji vifaa mbali mbali (Ijara) kupitia Benki ya Kiislamu;na

x. Kuanzisha akaunti za uwekezaji *(Mudharabah)* kupitia Benki ya Kiislamu.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo haya mbele ya Baraza lako tukufu, juu ya hali ya utekelezaji wa malengo na majukumu ya Wizara hii kwa kazi za kawaida na za maendeleo na zile za taasisi, naomba nihitimishe kwa kutoa matarajio ya jumla katika utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka ujao wa 2014/2015.

Kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, wizara ya Fedha inatarajia kuendelea kuimarisha uwezo wa ukusanyaji wa mapato kwa kiwango cha asilimia 23 ya pato la Taifa na kusimamia vyema matumizi yake pamoja na kuimarisha na kendeleza Kitengo cha ukusanyaji taarifa za mapato ikiwemo matumizi ya mashine za kutolea risiti kwa wafanya biashara na kudhibiti matumizi ya fedha za Umma. Aidha, wizara itaendelea kusimamia Kitengo cha Mahakama ya Rufaa kwa Walipa kodi kwa kushirikiana na Mahakama Kuu ya Zanzibar. Vile vile, wizara imejiandaa kuzingatia madhara ya mabadiliko ya nchi kwa kuhakikisha mipango na mikakati ya wizara na Taasisi zake inayaingiza kwenye utekelezaji.

Mhe. Mwenyekiti, wizara ya Fedha itaendelea kulipa mafao ya uzeeni na malimbikizo ya kiinua mgongo kwa wastaafu kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha utakavyoruhusu.

Mhe. Mwenyekiti**,** natoa shukrani za dhati kwa Baraza lako tukufu kwa ushirikiano mzuri tunaoendelea kuupata kutoka kwako wewe binafsi, Baraza lako Tukufu, Taasisi na wananchi wote. Hivyo, napenda kukushukuru wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa wawakilishi wote kwa kunipa nafasi hii na kwa kunisikiliza kwa makini wakati nikiwakilisha makadirio ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015. Makadirio haya yanatokana na kazi nzuri iliyofanywa kwa ushirikiano wa wafanyakazi wa Wizara ya Fedha, Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya Fedha.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa uongozi wote wa Wizara ya Fedha, unaoongozwa na Ndugu Khamis Mussa Omar, Katibu Mkuu na Ndugu Juma A. Hafidh Naibu Katibu Mkuu kwa umahiri wao wa kuiongoza Wizara kwa ufanisi. Aidha, nawashukuru Wakuu wa Idara na Taasisi pamoja na Wafanyakazi wote kwa michango na ushirikiano wao mkubwa katika kutekeleza majukumu ya Wizara hii yenye umuhimu wa pekee katika Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, wizara inaomba kupewa idhini ya matumizi ya jumla ya TZS 147,390.12 milioni kwa mgawanyo ufuatao:

E. MWELEKEO WA BAJETI YA MWAKA 2014/2015

VOTE 19 NA 45 - WIZARA YA FEDHA

S/N	VIFUNGU	TZS Milioni	TZS Milioni
I	**MATUMIZI YA KAWAIDA**		
	Mishahara	4,389,10	
	Matumizi mengineyo (O/C)	5,718.31	
	Ruzuku kwa Taasisi	17,452.30	
	Marekebisho ya Mishahara	8,500.00	36,067.70
II	**MATUMIZI YA MAENDELEO**		
	Mchango wa Serikali	7,203.00	
	Ruzuku na Mikopo	14,293.50	
	Ununuzi wa meli ya Serikali	20,000.00	41,496.50
III	**MFUKO MKUU WA SERIKALI**		
	Gharama za mfuko Mkuu wa Serikali	69,825.92	69,825.92
	JUMLA KUU		**147,390.12**

Mhe. Mwenyekiti: Baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja.*(Makofi)*

Kiambatisho Nam.1

UKUSANYAJI WA MAPATO KUTOKA VIANZIO VYA NDANI

S/N	CHANZO	MAKADIRIO KWA MWAKA 2013/14	MAKUSANYO HALISI KWA MWAKA 2013/2014	MAKADIRIO KWA MWAKA 2014/15
1	Ukodishwaji wa mashamba ya mpira	175,000,000.00	-	160,000,000.00
2	Uuzwaji wa Risiti	28,000,000.00	3,026,000.00	60,000,000.00
3	Ukodishwaji wa Majengo	32,760,000.00	-	602,500,000.00
4	Uuzaji vifaa chakavu	2,993,000.00	17,496,000.00	95,000,000.00
5	Mapato kutokana na Uhamiaji	3,870,000,000.00	3,238,106,099.00	4,000,000,000.00
6	Ukodishwaji wa matangi ya Mafuta	251,000,000.00	22,750,000.00	30,000,000.00
7	Mapato Mengineyo	57,516,000.00	4,246,000.00	20,000,000.00
8	Uvuvi wa Chini ya Bahari	-	-	-
9	Malipo ya Mkonga wa Taifa	1,440,000,000.00	-	840,000,000.00
	JUMLA	**5,997,269,000.00**	**3,285,624,099.00**	**6,007,500,000.00**

Kiambatanisho Nam.II

MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA KWA MWAKA 2013/2014				
KASMA	**IDARA**	**MAKADIRIO 2013/14**	**MATUMIZI HALISI**	**UFANISI %**
03	AFISI KUU PEMBA	825,075,000.00	811,987,523.00	98.41%
04	MIPANGO SERA NA UTAFITI	285,297,000.00	201,805,340.00	70.74%
07	MHASIBU MKUU WA SERIKALI	3,183,570,000.00	2,825,228,258.00	88.74%
09	FEDHA ZA NJE	173,868,000.00	156,572,500.00	90.05%
13	MITAJI YA UMMA NA UHAKIKIMALI	502,750,000.00	401,510,516.00	79.86%
19	UENDESHAJI NA UTUMISHI	3,962,349,000.00	3,741,891,609.00	94.44%
22	BAJETI	671,121,000.00	476,418,953.00	70.99%
	MAREKEBISHO YA MSHAHARA	17,500,000,000.00	17,500,000,000.00	100.00%
	RUZUKU	18,663,000,000.00	13,908,454,736.00	74.52%
	JUMLA	**45,767,030,000.00**	**40,023,869,435.00**	**87.45%**

Kiambatisho Nam.III

ORODHA YA PROGRAMU/MIRADI ILIYOTEKELEZWA NA WIZARA KWA MWAKA 2013/2014

WIZARA YA FEDHA - TZS "000"

JINA LA MRADI	**MAKISIO KWA MWAKA 2013/2014**				**MATUMIZI HALISI**				
	SMZ	**MUHISANI**		**JUMLA**	**SMZ**	**%**	**MUHISANI**	**%**	**JUMLA**
Programu ya Mageuzi katika usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP)	-	World Bank	500,000.00	500,000.00	-	-	29,000.00	6%	29,000.00
Kuimarisha Usimamizi wa Misaada Zanzibar	5,000.00	UNDP	700,000.00	705,000.00	5,000.00	100%	389,420.00	56%	394,420.00
Program ya Ujenzi wa Afisi za Serikali Zanzibar	7,000,000.00		-	7,000,000.00	1,692,282.30	24%	-	-	1,692,282.30
i) Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko									-
ii) Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano									-
iii) Wizara Ya Fedha,									-
iv) Wizara ya Ustawi wa jamii, Vijana, Maendeleo ya Wanawake									-
v) Wizara ya Katiba na Sheria									-
vi) Wizara ya Nchi (AR) Utumishi wa Umma na									-

JINA LA MRADI	MAKISIO KWA MWAKA 2013/2014				MATUMIZI HALISI				
	SMZ	MUHISANI		JUMLA	SMZ	%	MUHISANI	%	JUMLA
Utawala Bora									
Programu ya Kuimarisha Huduma za Miji (ZUSP)	50,000.00	World Bank	15,200,000.00	15,250,000.00	38,626.30	77%	10,270,813.81	68%	10,309,440.11
Programu ya Mageuzi katika usimamizi wa Fedha za Umma (PFM)	40,000.00		-	40,000.00	6,142.50	15%	-	-	6,142.50
Utayarishaji wa mpango mkuu wa maeneo huru Fumba	150,000.00		-	150,000.00	-		-	-	-
Ujenzi wa Chuo na Dahalia Chwaka (Maabara ya Computer na madarasa).	200,000.00		-	200,000.00	100,000.00	50%	-	-	100,000.00
Mradi wa kufanya tathmini ya mali za Serikali	500,000.00		-	500,000.00	123,599.90	25%	-	-	123,599.90
Kuimarisha Utawala Bora Awamu ya pili	55,000.00	AFDB	1,088,403.00	1,143,403.00	55,000.00	100%	751,407.50	69%	806,407.50
JUMLA	**8,000,000.00**	-	**17,488,403.00**	**25,488,403.00**	**2,020,651.00**	**25%**	**11,440,641.31**	**65%**	**13,461,292.31**
UNUNUZI WA MELI	**17,000,000.00**			**17,000,000.00**	**10,048,391.60**	**59%**			**10,048,391.60**
JUMLA KUU	**25,000,000.00**		**17,488,403.00**	**42,488,403.00**	**12,069,042.60**	**48%**	**11,440,641.31**	**65%**	**23,509,683.91**

Kiambatisho Nam.IV

MATUMIZI YA KAZI ZA MAENDELEO KWA MWAKA 2013/2014

TZS "000"

	MCHANGO WA SERIKALI	**MATUMIZI HALISI JULAI 2013-2014**	**UFANISI %**
za Umma (PFMRP)			
	5,000	5,000.00	100%
	7,000,000	1,692,282.38	24%
ya Wanawake			
Utawala Bora			
	50,000	38,626.30	77%
za Umma (PFM)	40,000	6,142.50	15%
umba	150,000	-	0%
Computer na madarasa).	200,000	100,000.00	50%
	500,000	123,599.91	25%
	55,000	55,000.00	100%
	8,000,000	**2,020,651.09**	**25%**
	17,000,000.00	**10,048,391.60**	**59%**
	25,000,000.00	**12,069,042.69**	**48%**

Kiambatanisho Nam. V

MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA KAZI ZA KAWAIDA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

KASMA	**IDARA**	**MAKISIO YA MWAKA 2013/2014**
3	AFISI KUU PEMBA	825,075,000
4	MPANGO SERA NA UTAFITI	285,297,000
7	MHASIBU MKUU WA SERIKALI	3,183,570,000
9	FEDHA ZA NJE	173,868,000
13	MITAJI YA UMMA NA UHAKIKIMALI	502,750,000
19	UENDESHAJI NA UTUMISHI	3,962,349,000
22	BAJETI	18,171,121,000
	RUZUKU	18,663,000,000.00
JUMLA		**45,767,030,000.00**

Kiambatanisho Nam.VI

ORODHA YA PROGRAMU/MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA NA WIZARA KWA MWAKA 2014/2015

WIZARA YA FEDHA - "000"TSHS.

JINA LA MRADI	MCHANGO WA SERIKALI		MCHANGO WA WAHISANI			JUMLA YA BAJETI
	MAKISIO YA MWAKA 2013/2014	MAKISIO YA MWAKA 2014/2015	WAHISANI	RUZUKU	MKOPO	
1	2	3	4	5	6	3+5+6
Programu ya Mageuzi katika usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP)	0	10,000	Norway	2,630,000		2,640,000
Kuimarisha Usimamizi wa Misaada Zanzibar	5,000	10,000	UNDP	326,000		336,000
Program ya Ujenzi wa Afisi za Serikali Zanzibar	7,000,000	3,000,000				3,000,000
i) Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko						
ii) Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano						
iii) Wizara Ya Fedha,						
iv) Wizara ya Ustawi wa jamii, Vijana, Maendeleo ya Wanawake						
v) Wizara ya Katiba na Sheria						
vi) Wizara ya Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora						
Programu ya Kuimarisha Huduma za Miji (ZUSP)	50,000	1,600,000	World Bank		10,611,176	12,211,176
Programu ya Mageuzi katika usimamizi wa Fedha za Umma (PFM)	40,000	20,000				20,000
Utayarishaji wa mpango mkuu wa maeneo huru Fumba	150,000	150,000				150,000
Ujenzi wa Chuo na Dahalia Chwaka (Maabara ya Computer na madarasa).	200,000					

JINA LA MRADI	MCHANGO WA SERIKALI		MCHANGO WA WAHISANI			JUMLA YA BAJETI
	MAKISIO YA MWAKA 2013/2014	MAKISIO YA MWAKA 2014/2015	WAHISANI	RUZUKU	MKOPO	
Mradi wa kufanya tathmini ya mali za Serikali	500,000					
Kuimarisha Utawala Bora Awamu ya pili	55,000	10,000	AFDB		726,325	736,325
Programu ya Upatikanaji wa Rasilimali Fedha		2,403,000				2,403,000
JUMLA	**8,000,000**	**7,203,000**		**2,956,000**	**11,337,501**	**21,496,501**
UNUNUZI WA MELI	**17,000,000**	**20,000,000**				**20,000,000**
JUMLA KUU	**25,000,000**	**27,203,000**		**2,956,000**	**11,337,501**	**41,496,501**

Kiambatisho Nam.VII

MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

TZS Bilioni

	2012/2013			**2013/2014**		
	MAKISIO	**HALISI**	**ASILIMIA**	**MAKISIO**	**HALISI**	**ASILIMIA**
	139.8	132.6	95%	155.5	149.6	96%
	71.1	59.3	83%	80.6	50.1	62%
	44.3	40.7	92%	52	40.1	77%
	54.9	54.9	100%	66	61.1	93%
	310.1	287.5	93%	354.1	300.9	85%
	37.3	31.2	84%	70	34.9	50%
	347.4	**318.8**	**92%**	424.1	335.8	79%
ikali	31 / 05 / 2014					

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Naomba uniruhusu kuwasilisha hotuba ya maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujalia uzima, siha na nguvu zilizoweza kutufikisha hapa Barazani na tukaweza kufanya shughuli zetu kama tulivyopanga, hatuna budi kusema *Alhamdulilah.*

Mhe. Mwenyekiti, shukurani zangu za dhati pia zije kwako Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kusimama hapa, mbele ya Baraza lako Tukufu kutoa muhutasari wa maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumzi kwa mwaka 2014/15 ambayo punde hivi Mheshimiwa Waziri wa Fedha amewasilisha mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe nafasi hii pia kumshukuru Waziri wa Fedha Mhe. Omar Yussuf Mzee, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wengine wote wa Wizara hii kwa mashirikiano yao ya dhati kwa Kamati wakati wote tulipokuwa tukifanyakazi zetu za kawaida za Kamati. Tunawashukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, sitakuwa nimetenda haki iwapo nitaendelea na hotuba hii bila ya kutoa shukurani za pekee kwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati yangu, ambao tumeshirikiana kwa umoja wetu kuyapitia na kuyachambua makadirio haya ya Bajeti, nawashukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kutambua mchango wao mkubwa kwenye Kamati hii hadi kufanikisha kazi hii, naomba sasa niwataje kwa majina Wajumbe na Makatibu wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo:

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin Mwenyekiti
2. Mhe. Hija Hassan Hija Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Hamad Masoud Hamad Mjumbe
4. Mhe. Viwe Khamis Abdalla Mjumbe
5. Mhe. Raya Suleiman Hamad Mjumbe
6. Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mjumbe

7. Mhe. Asha Abdu Haji Mjumbe
8. Ndg. Haji Khatib Haji Katibu
9. Ndg. Fatma Omar Ali Katibu

Mhe. Mwenyekiti, kama inavyofahamika kuwa wizara hii imefanyiwa mabadiliko ya muundo wake ambapo sasa Tume ya Mipango imekuwa chini ya Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora na Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ iliyoko Dar es Salaam imekuwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mabadiliko hayo bado wizara hii imekuwa na majukumu makubwa na mazito yakiwemo yale ya kusimamia ukusanyaji wa mapato yanayoratibiwa na Bodi ya Mapato nchini (*ZRB*) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) na yale yanayoratibiwa na Idara ya Fedha za Nje.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majukumu hayo mazito pia husimamia idara na taasisi mbali mbali zilizo chini ya Wizara hii ya Fedha, lakini pia, ina jukumu la kufanyakazi kwa karibu na taasisi za Muungano kama vile Tume ya Pamoja ya Fedha, Benki Kuu ya Tanzania, Mamlaka ya Kusimamia Bima (*TIRA*), Benki ya Posta na taasisi nyenginezo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la kusimamia matumizi ya Serikali ni muhimu, Wizara husimamia Idara ya Bajeti na Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ili kuona kuwa matumizi ya Serikali yanatumika kwa mujibu wa sheria za fedha na Sheria za matumizi ikiwa ni pamoja na kufuatwa Kanuni zilizopo na kuhakikisha kuwa fedha zinagawiwa kwa mujibu wa mahitaji yaliyopo na si vyenginevyo.

IDARA YA MHASIBU MKUU WA SERIKALI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ina majukumu makubwa ya kuitunza Hazina ya Serikali, kusimamia mwenendo wa Deni la Taifa, kudhibiti mapato na vile vile, kusimamia shughuli za kihasibu na Ukaguzi wa Ndani kwa kuhakikisha kwamba taratibu na Sheria zote zinazohusika zinafuatwa katika suala zima la kudhibiti mapato na matumizi ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza awali kuwa suala la usimamizi wa matumizi ya fedha za Serikali ni jambo muhimu ili kudhibiti mianya inayoweza kujitokeza ya upotevu wa fedha za Serikali. Katika kutekeleza hilo Wizara na Serikali kwa ujumla inapaswa kutilia mkazo zaidi suala zima la kufanya mabadiliko makubwa katika usimamizi wa matumizi ya fedha za Serikali ikiwa ni pamoja na kufanya mapitio ya mfumo mzima wa Ukaguzi wa Hesabu za Ndani katika taasisi mbali mbali za Serikali. Aidha, mabadiliko hayo yanapaswa yahusishe pamoja na mambo mengine kuwajengea uwezo wakaguzi wa Ndani wa Hesabu na kuweka utaratibu maalum utakaowawezesha wakaguzi hao kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na uadilifu mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, ni muda mrefu sasa limekuwa likizungumzwa suala la uanzishwaji wa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani ambapo Wajumbe wa Baraza hili wamekuwa wakiiona haja na umuhimu wa kuazishwa kwa Ofisi hii ili kuongeza uwajibikaji, kuleta utaraibu mzuri wa mgawanyo wa majukumu na kuongeza Utawala Bora katika suala hili muhimu la Ukaguzi wa Hesabu za Serikali. Hivyo, Kamati inaitaka Wizara kuharakisha mipango yake ya kuimarisha nyanja hii ya Ukaguzi wa Ndani wa Hesabu ikiwa ni pamoja na suala la kuanzisha Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Hesabu itayosimamia wakaguzi wote wa Ndani wa Hesabu.

Mhe. Mwenyekiti, moja kati ya jukumu la idara hii ni kulipa mafao ya kiinua mgongo na pensheni kwa wastaafu wa Serikali ambapo kwa mwaka huu wa fedha unaomalizika wa 2013/2014 jumla ya Tsh. billioni 10 zilitengwa kwa ajili ya malipo ya mafao ya kiinua mgongo kwa wastaafu wa SMZ ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2014 zaidi ya Tsh. billioni 4.7 zilikuwa zimeshalipwa kwa wastaafu 592 ikiwa ni malipo kwa wastaafu wa mwezi wa Januari. 2013 hadi Juni, 2013.

Mhe. Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha kuona kuwa hadi sasa mafao kwa wastaafu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yamekuwa duni na wastaafu hawa inaonekana kama wamesahauliwa kwani viwango vya viinua mgongo na hata pensheni za wastaafu wa SMZ wa ngazi za kawaida havilingani kabisa na mabadiliko ya hali ya maisha ambayo imekuwa ni ngumu sana kwa wastaafu. Aidha, hali za maisha za wastaafu hawa huwa ngumu zaidi pale wanapokumbwa na maradhi mbali mbali ambayo huhitaji fedha si kidogo katika kuyashughulikia.

Mhe. Mwenyekiti, Wastaafu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar walifanyakazi kubwa na kuvuja jasho lao kwa muda mrefu katika kulijenga Taifa letu. Hivyo, Serikali haitakuwa imetenda haki hata kidogo kwa kuwaandalia mafao manono viongozi wa Serikali pekee na kuwapuuza na kuwaacha wakitapatapa wastaafu wengine wa ngazi za chini ambao nao pia wanastahiki kuenziwa, kutunzwa na kuengwaengwa kwa kupatiwa mafao yaliyo bora yanayolingana na hali ya maisha ya wakati uliopo. Kwa mnasaba huu basi, Kamati inaitaka Serikali kufanya mapitio ya kina juu ya sheria, taratibu na miongozo inayoongoza malipo kwa ajili ya mafao ya wastaafu wa Serikali ili Serikali iwapunguzie dhiki za kimaisha zinazowakumba wastaafu wake ambao walijitolea nafsi zao katika kutekeleza majukumu yao mbali mbali ndani ya Serikali hii wakati wa enzi zao.

IDARA YA MIPANGO SERA NA UTAFITI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ya Wizara ya Fedha, pamoja na mambo mengine inaratibu masuala mtambuka, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya sekta ya fedha.

Mhe. Mwenyekiti, moja kati ya miradi inayosimamiwa na wizara hii ni Mradi wa Huduma za Jamii Mijini (*ZUSP*). Mradi huu umekuwa ukiulizwa sana na wananchi na baadhi ya Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kutokana na ukimya wake wa muda mrefu. Aidha, inafahamika kuwa Mradi huu unakusudia kuimarisha na kuendeleza huduma mbali mbali za miji yetu pamoja na kujenga uwezo wa kitaasisi wa Baraza la Manispaa na Mabaraza ya Miji Mikuu ya Chake Chake, Wete na Mkoani ambapo jumla ya Dola za Marekani millioni 38 kutoka Benki ya Dunia zinatarajiwa kutumika. Mradi huu umepangwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka 5, kuanzia Juni 2011 hadi Juni 2016.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuwa mradi huu umeonekana kuwa kimya kwa muda mrefu, Kamati imekuwa ikiufuatilia mradi huu na kupata taarifa juu ya hatua mbali mbali za utekelezaji wa kazi mbali mbali zilizopangwa kufanywa katika mradi huu. Hata hivyo, Kamati bado inaisisitiza wizara pamoja watendaji wa mradi huu kuharakisha taratibu mbali mbali zinazohitajika katika utekelezaji wa kazi za mradi huu zikiwemo kazi zinazowagusa moja kwa moja wananchi wetu wanaoishi katika maeneo mbali mbali zikijumuisha ujenzi wa michirizi ya maji ya mvua katika maeneo mbali mbali ya mji, Uwekaji wa taa kwenye baadhi ya maeneo ya Mji Mkongwe na baadhi ya barabara kuu za Mjini Unguja, Ujenzi wa ukuta wa bahari katika eneo la Mizingani pamoja na kukamilisha kazi ya ujenzi wa vibaraza vya kuwekea taka.

Mhe. Mwenyekiti, kazi hizo nilizozitaja hususan kazi ya ujenzi wa michirizi ya maji ya mvua ni jambo muhimu la kumalizwa kwa vile hii ni ahadi ya Serikali kwa wananchi wake ambayo imechukuwa muda mrefu kutekelezwa. Hivyo, Kamati inaitaka wizara na uongozi wa mradi huu kuwa mara tu baada ya kupata ruhusa iliyokuwa inasubiriwa kutoka Benki ya Dunia, ichukue hatua za haraka za kutangaza kazi ya ujenzi wa michirizi hiyo pamoja na hatua nyengine zinazofuata ili kazi hii ya kujenga michirizi angalau iweze kuanza na kurejesha imani na matumaini ya wananchi kuhusu kujengwa kwa michirizi hiyo na hatimae kuondokana na tatizo la kutuama kwa maji katika maeneo yetu na pia kuondokana na uchafu mitaani.

IDARA YA BAJETI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Bajeti ina majukumu ya kusimamia utayarishaji wa Bajeti ya Serikali pamoja na kusambaza maelekezo yanayohusu mbinu bora za kibajeti pamoja na kupanga na kudhibiti matumizi ya rasilimali fedha kwa taasisi mbali mbali za umma.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa wote tunaamini kuwa ukuaji wa uchumi ni nguzo muhimu kwa maendeleo ya kila nchi, ni vyema basi Serikali kupitia wizara hii ikaelekeza nguvu zake katika Idara ya Bajeti kwa kuwapatia wataalamu wa kutosha katika fani za uchumi. Kama wote tunavyofahamu kuwa Serikali imeingia katika mfumo mpya wa Bajeti inayotumia Programu (*PBB*) kwa wizara mbali mbali, tungelipenda kufahamu ni mafanikio yepi hadi sasa yamepatikana katika kipindi chote na ikiwa kuna mapungufu, basi ni vyema tungelifahamishwa ili tuweze kuyafahamu na ikiwezekana tuweze kuyatatua.

Mhe. Mwenyekiti, mfumo huu mpya unaotumia programu bado haujaeleweka vizuri, ni vyema basi Wizara ya Fedha ikaendelea kutoa mafunzo ya kina kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na watendaji wa Serikali ili wapate uelewa zaidi kuhusu dhana hii mpya na kujua umuhimu wake katika kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, bado mwenendo wa matumizi ya fedha za umma sio mzuri, matumizi ya fedha za umma yasiyolingana na uhalisia (*value for money)* ni tatizo kubwa katika Idara za Serikali na Taasisi za umma. Kuendelea kutumia fedha nyingi za umma kwa semina, makongamano, viburudishaji na safari ni jambo lililozoweleka siku hizi, suala la kutumia fedha nyingi za umma kwa maandalizi tu ya jambo fulani ni matumizi mabaya ya fedha za umma.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza lako limeshuhudia hili katika bajeti mbali mbali za Wizara zenye matumizi ya aina hii, mafungu makubwa ya fedha kwa mamilioni yametumika kwa kuandaa sera, kanuni, sheria na kuacha kutumia fedha za umma kwa jambo linaloonekana machoni.

Mhe. Mwenyekiti, utayarishaji wa Bajeti ya Serikali ni jukumu la msingi la idara hii. Hata hivyo, wote ni mashahidi kuwa utayarishaji wa Bajeti ya mwaka huu wa fedha wa 2014/2015 ulikuwa na kasoro nyingi, hali ambayo imesababisha usumbufu mkubwa wakati wa kujadili Bajeti hii katika Kamati na hata katika Baraza lako hili Tukufu. Miongoni mwa kasoro hizo ni kuwepo kwa majina ya kasma ambayo hayalingani na muktadha wenyewe wa kasma inayokusudiwa. Aidha, katika kazi za maendeleo baadhi ya wizara ziliwekewa Washirika wa Maendeleo wasiohusiana kabisa na kazi za maendeleo za wizara hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kasoro hizo, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ambayo ndio inayosimamia utekelezaji wa majukumu ya wizara hii na taasisi zake haikufurahishwa na mapungufu haya na hivyo basi, inaitaka wizara kufanya uchunguzi wa kina juu ya sababu zilizopelekea mapungufu hayo yaliyojitokeza ili hatimae kuchukua hatua zinazofaa ili kuyarekebisha mapungufu hayo na kuhakikisha kuwa kasoro hizo hazitokei tena katika siku zijazo.

IDARA YA UHAKIKIMALI NA MITAJI YA UMMA

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ina majukumu mbali mbali yakiwemo kufuatilia taratibu za ununuzi na uhakiki wa Mali za Serikali pamoja na kuendeleza tathmini ya mali za Serikali katika wizara mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa changamoto kubwa inayoikabili idara hii hususan kwa upande wa Pemba ni ukosefu wa taarifa za uhakika kuhusu mali za Serikali na maeneo zilipo hususan mashamba kutokana na mabadiliko mbali mbali yaliyotokea katika maeneo ambayo mali hizo zipo.

Mhe. Mwenyekiti**,** kutokana na hali hiyo, Kamati inaiomba wizara kupitia idara ya Uhakiki Mali iwe na ushirikiano wa karibu kati yake na taasisi nyengine za Serikali ili kupatikana usahihi wa taarifa za kumbukumbu za mali za Serikali zilizo sawa kwa pande zote mbili ili kuondoa migongano ya taarifa hizo baina ya Idara ya Uhakiki Mali na taasisi nyengine za Serikali.

MAMLAKA YA UKUZAJI VITEGA UCHUMI ZANZIBAR (*ZIPA*)

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi, Zanzibar (*ZIPA*) ina jukumu kubwa la kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza nchini. Suala la kujiuliza Mhe. Mwenyekiti, Je, jukumu hili kubwa kwa maendeleo ya nchi hii limetekelezwa ipasavyo?

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Vitega Uchumi imekuwa ikijitahidi kutekeleza jukumu hili, lakini bado juhudi hizi zimegonga mwamba kutokana na urasimu mkubwa uliopo kati ya taasisi na taasisi. Kumekuwa hakuna mashirikiano ya dhati katika vyombo au taasisi zinazohusiana na masuala ya uwekezaji nchini jambo linalosababisha kuzorotesha kasi ya uwekezaji nchini.

Mhe. Mwenyekiti, mara kwa mara Kamati ya Fedha, Biashra na Kilimo imekuwa ikizungumzia umuhimu wa kuanzishwa kwa *"One Stop Centre*" ikiwa na lengo la kuwaweka pamoja wadau wote wanaohusika na uwekezaji ili iwe rahisi kutoa maamuzi juu ya uwekezaji nchini.

Mhe. Mwenyekiti, dhana hii imekuwa ni ndoto, lakini wale watendaji wenye dhamana na maamuzi ama na vitengo vyao au taasisi zao au idara zao hawahudhurii katika vikao vinavyoitishwa na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Vitega Uchumi, badala yake huwapeleka maofisa wa chini wasio na maamuzi ya jambo lolote.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa suala hili tumekuwa tukililalamikia sana bila ya mafanikio na kwa kuwa wizara yako ina lengo la kuifanyia mapitio Sheria ya Mamlaka ya Vitega Uchumi, basi katika sheria hiyo ikiwemo kifungu cha sheria kinachowalazimisha wakuu wanaohusika na uwekezaji kushiriki katika vikao hivyo kisheria kwa manufaa ya nchi na wananchi wetu kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, uwekezaji nchini ni dhana pana, lakini pia, uwekezaji una eneo pana katika kulipeleka Taifa hili katika maendeleo. Nchi haiwezi kuendelea bila ya kuwa na uwekezaji, mapato ya nchi hayawezi kuongezeka bila yakuwa na uwekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, Jamhuri ya Watu wa China imekuza uchumi wake kutokana na uwekezaji. Serikali ni lazima itoe kipaumbele katika eneo hili la uwekezaji, maeneo huru ya uchumi Fumba na Micheweni ni lazima yashughulikiwe ipasavyo. Ile *Master Plan* ya maeneo huru ya uchumi ya Fumba ni lazima imalizike ili tutoe fursa kwa wawekezaji waweze kuwekeza katika eneo lile. Suala la miundombinu katika maeneo ya uwekezaji lipewe kipaumbele kama vile barabara, maji na umeme ili iwe kivutio kwa wawekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuyashughulikia maeneo huru ya uchumi, Serikali inapaswa pia kuzichukulia hatua kwa uzito unaostahili changamoto kadhaa zinazojitokeza katika maeneo hayo hasa katika maeneo huru Fumba, ili malengo yaliyokusudiwa ya kuyatenga maeneo hayo ya uwekezaji yaweze kufikiwa. Miongoni mwa changomoto hizo ni kuvamiwa na wananchi kwa baadhi ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya maeneo huru ya uchumi. Aidha, Idara ya Upimaji nayo ambayo hupewa kazi ya upimaji wa maeneo hayo kwa ajili ya matayarisho ya mpango wa matumizi ya ardhi katika maeneo hayo (*Master Plan*) imekuwa ikichelewa kukamilisha kazi hiyo muhimu ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hatua mbali mbali ambazo Serikali inapaswa kuzichukua katika kuzitatua changamoto hizo, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inashauri kuwa bado elimu zaidi inahitajika kwa wananchi ili kujua kwamba nia ya Serikali sio kuwaumiza wala kuwanyang'anya ardhi zao bali wao wananchi wanatakiwa kutoa ushirikiano wao kwa Serikali kwa mujibu wa taratibu za Serikali na sio kwa kufuata utashi wao binafsi.

BODI YA MAPATO ZANZIBAR (*ZRB*)

Mhe. Mwenyekiti, Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) imeanzishwa chini ya sheria Nam. 7 ya mwaka 1996 kama taasisi ya ukusanyaji mapato ya Serikali yatokanayo na vyanzo vya ndani ambapo mnamo mwezi wa Septemba, 1998 Bodi hii ilianza kazi zake rasmi.

Mhe. Mwenyekiti, jukumu hili ni kubwa na linahitaji umakini wa hali ya juu, uaminifu na moyo wa kujituma bila ya wafanyakazi wake kuwa na mambo hayo muhimu, basi hali ya ukusanyaji wa mapato haitapiga hatua au haitafanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kikawaida wananchi au wafanyabiashara huwa hawapendi kulipa kodi kwa hiari na mara zote maofisa wa kodi huonekana kama ni kero kwa wafanyabiashara.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi inaendelea kutoa wito kwa wananchi na wafanyabiashara kulipa kodi zao kwa hiari bila ya shuruti na wasiwaone maofisa wetu wa kodi kama ni kero kwao. Maofisa hawa wanafanyakazi zao kwa mujibu wa sheria na wanatekeleza majukumu yao ya kazi kama wafanyakazi wengine.

Mhe. Mwenyekiti, nchi bila ya kukusanya kodi haiwezi kupata maendeleo, tunapozungumzia madawa hospitalini, maana yake ni kodi, tunapozungumzia elimu bora nchini, maana yake ni kodi, tunapozungumzia maji safi na salama, maana yake ni kodi. Kwa maana hiyo, huwezi kuzungumzia maendeleo ya nchi bila ya kuhusisha ulipaji wa kodi nchini.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inampongeza Kamishna wa Bodi ya Mapato nchini (*ZRB*) pamoja na maofisa wake wote kwa kutekeleza majukumu yao vizuri hali inayoonesha mafanikio makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo bado inaendelea kuamini kuwa mapato zaidi yataweza kupatikana ikiwa mambo yafuatayo yatazingatiwa:

1. Ikiwa Serikali itasimamia kisawasawa ukwepaji wa kodi unaotokana na wafanyabiashara wengi kutokutoa risiti wanapofanya biashara zao;

2. Ikiwa Serikali itawawekea vitendea kazi vya kisasa (*ZRB*) ambavyo itakuwa ni rahisi kuvitumia kwa kukusanya kodi kama vile utumiaji wa risiti uliounganishwa na mtandao (*electronic receipt*) kwa wafanyabiashara wakubwa na wadogo kama vile nchi nyengine Tanzania Bara, Kenya na kadhalika;

3. Ikiwa Serikali itaachana na utaratibu wa kukubali kupokea watalii wa makundi (*package tours*) katika mahoteli. Utaratibu huu hupoteza mamilioni ya fedha, nchi nyingi duniani zimeachana na utaratibu huu;

4. Ikiwa Serikali itadhibiti kisawasawa mapato yanayotokana na *visa* yanayokusanywa na Idara ya Uhamiaji katika viwanja vya ndege;

5. Ikiwa Serikali itadhibiti mapato yanayotokana na utalii *VAT* mahotelini na kuwadhibiti wale wafanyakazi wa *ZRB* waliokuwa sio waaminifu katika kufanyakazi zao; na

6. Ikiwa Serikali itadhibiti kisawasawa suala la magendo ya mafuta ya petroli na *diesel* nchini.

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (*TRA*)

Mhe. Mwenyekiti, taasisi nyengine yenye jukumu kubwa la kukusanya kodi ni Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*). Mamlaka hii hukusanya mapato yatokanayo na vianzio vya ushuru wa forodha, ushuru wa bidhaa, kodi ya mapato na kodi nyengine zinazotokana na biashara za Kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo inampongeza sana Naibu Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania pamoja na watendaji wake wote kwa kutekeleza majukumu yao vizuri na kufikia malengo yaliyowekwa.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na utekelezaji mzuri wa majukumu na malengo ya taaasii hii, Bado Mamlaka hii ya Mapato imekuwa ikikabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo upungufu wa wafanyakazi hususan katika Idara ya Kodi za Ndani ambayo inahitaji wafanyakazi wengi kwa ajili ya ufuatiliaji na ukusanyaji wa kodi husika. Vile vile, wafanyakazi kutokuwa na ujuzi wa kutosha wa kodi katika sekta za mawasiliano ili kujua kwa undani namna sekta hizo zinavyoofanya kazi. Aidha, misamaha ya kodi nayo bado ni changamoto katika ukusanyaji wa mapato ya mamlaka hii.

Kutokana na hali hiyo, mamlaka hii inapaswa kujipanga upya katika mikakati yake ili kuongeza nguvu kazi pamoja na kuwajengea uwezo wafanyakazi waliopo ili kuongezea mapato Serikali. Aidha, Kamati inaona kuna haja kwa Serikali kufanya utafiti wa kina ili kujua kwa kiasi gani misamaha ya kodi inalinufaisha Taifa hili na haiwanufaishi watu wachache tu.

BENKI YA WATU WA ZANZIBAR *LIMITED (PBZ)*

Mhe. Mwenyekiti, jukumu kubwa la Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*) ni kupokea amana za wateja wake na kukopesha kwa wanaohitaji pamoja kuwapatia wateja huduma mbali mbali za kibenki.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inatoa pongezi za dhati kwa viongozi na watendaji wa benki hii kwa jitihada kubwa wanazozionesha katika utekelezaji wa majukumu yao zilizopelekea benki hii kuendesha shughuli zake kwa faida, mwaka hadi mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mafanikio makubwa yaliyofikiwa na benki hii, bado benki hii imekuwa na kilio cha muda mrefu cha kutooengezewa mtaji na mmiliki wake ambae ni Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Hata hivyo, Kamati inatambua na kuthamini sana hatua mbali mbali za mazungumzo zilizochukuliwa kati ya viongozi wa wizara

hii na wale wa *PBZ* katika kuona namna bora zaidi ya kulishughulikia suala hili. Kwa mnasaba huu basi, Kamati inaishauri wizara kuharakisha hatua zake hizo ilizozianzisha katika kuhakikisha kuwa benki hii inaongezewa mtaji ili iweze kukabiliana ipasavyo na ushindani wa huduma za kibenki uliopo hapa nchini hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati pia inawataka viongozi wa *PBZ* kuimarisha na kupanua huduma za benki hiyo katika sehemu nyingi zaidi hususan vijijini, ikiwa ni pamoja na kuongeza huduma za *ATM* katika maeneo hayo ili kuwaondoshea usumbufu usio wa lazima wateja wake ambao wengi wao ni wananchi wa kipato cha kawaida. Aidha, Kamati inawasihi watendaji wa benki hii hasa wa matawi yake yaliyopo Zanzibar kubadilika kiutendaji kwa kudumisha nidhamu ya kazi na kuachana na tabia ya kufanya kazi kwa mazeoa, ili kuongeza ufanisi katika benki hiyo na kuwaondoshea wateja wake malalamiko kutokana na kero mbali mbali wanazozipata pindi wanapohitaji kupatiwa huduma katika benki hiyo.

SHIRIKA LA BIMA LA ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, kama inavyofahamika kuwa Shirika la Bima la Zanzibar lina jukumu la kutoa huduma za bima kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imefarajika kuona kuwa Shirika la Bima la Zanzibar limekuwa likifanya kazi zake kwa ufanisi pamoja na kupanua huduma zake katika Mikoa ya Tanzania Bara. Hatua ya Shirika hili ya kufanikiwa kuongeza mawakala watatu (3) wenye uwezo katika Mkoa ya Dar es Salaam, Mtwara na Mwanza katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, ni jambo la kupongezwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, licha ya mafanikio makubwa yaliyofikiwa, shirika hili limekua likikabiliwa na changamoto kadhaa hususan suala la ucheleweshaji wa ulipaji wa fidia ambalo limekuwa likilalamikiwa sana na wateja wa shirika hili. Aidha, kwa upande wa mawakala wa shirika hili nao pia wamekuwa wakikabiliwa na changamoto mbali mbali, miongoni mwa changamoto hizo ni ukosefu wa usafiri, kukosekana kwa utambulisho wa mawakala katika maeneo waliopo ambao baadhi yao hawana hata mapango ya kujitangaza.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, suala la utaratibu wa malipo ya mawakala limekuwa ni changamoto kwa vile mawakala hao hulipwa fedha zao baada ya kupeleka marejesho ya fedha katika shirika. Utaratibu huu umekuwa pamoja na mambo mengine ukichelewesha malipo ya mawakala hao.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaishauri uongozi wa shirika kuzipa uzito unaostahili changamoto hizo na hatimae kuzitatua ipasavyo kwa vile zinaweza kuzorotesha maendeleo ya shirika hilo kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, Kamati inaisihi sana uongozi wa shirika kubuni njia za ziada za kutoa elimu zaidi kwa wananchi juu ya umuhimu wa kukata bima katika shughuli mbali mbali. Pia, kwa upande wa Tanzania Bara shirika linapaswa kuzidisha nguvu katika kujitangaza ili wananchi na taasisi nyingi zaidi ziweze kutumia huduma zinazotelewa katika maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyofahamu kwa miaka hivi karibuni kumekuwa na engezeko kubwa la kampuni zinazotoa huduma za bima. Kuwepo kwa kampuni hizi kumepelekea kuwepo kwa ushindani mkubwa katika masuala ya bima. Aidha, ongezeko hili linaweza kupelekea baadhi ya kampuni kutoa huduma hizi za bima bila ya kufuata utaratibu ipasavyo. Hivyo, Kamati inaiomba Serikali ikae na Mamlaka ya Usimamizi wa Huduma za Bima (*TIRA*), katika usimamizi wa masuala mbali mbali muhimu ikiwemo kanuni na viwango vyao vya bima.

MFUKO WA HIFADHI YA JAMII (*ZSSF*)

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaupongeza uongozi na watendaji wa mfuko kwa utendaji wao mzuri wa kazi zao na jitihada mbali mbali wanazozichukua katika kutekeleza majukumu yake kwa wananchi katika kuhifadhi na kuwapatia mafao yao.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na mfuko huu, Kamati unautaka mfuko uongeze njia za kutoa taaluma juu ya huduma mbali mbali zinazotolewa na mfuko huo ikiwemo huduma ya uchangiaji kwa hiari (*Voluntary Scheme*) inayowapa fursa hata watu binafsi waliojiajiri wenyewe kuweka fedha zao na kufaidika na

huduma zinazotolewa na mfuko huo. Kufanya hivyo, kutawafanya wananchi wengi zaidi waliojiajiri hasa katika maeneo ya vijijini kuwa na mwamko wa kuzitumia fursa zinazotolewa na mfuko huo.

CHUO CHA UONGOZI WA FEDHA- CHWAKA ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, Chuo cha Uongozi wa Fedha (*ZIFA*) kina jukumu la kutoa mafunzo ya fani ya fedha na zinazolingana, kuandaa semina za kiutawala na kutoa mafunzo ya muda mfupi katika fani maalum.

Mhe. Mwenyekiti, inasemekana kuwa Serikali ina mpango wa kukihamishia chuo hiki kuwa katika Usimamizi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha (*SUZA*).

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inapenda kuishauri Serikali kuwa si nyema chuo hicho kukihamishia katika Usimamizi wa Chuo Kikuu cha Taifa (*SUZA*) na badala yake ni vizuri kukiacha kijiendeshe wenyewe. Isipokuwa Serikali ikiongezee ruzuku chuo hicho kwa ajili ya kukiongezea ufanisi katika utendaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, ushauri huu wa Kamati unatokana na sababu zifuatazo:

1. Kukihamishia chuo hicho kwenda *SUZA* kitaoengezea Chuo cha *SUZA* mzigo ambao hata upatikanaji wa fedha wa chuo hicho cha *SUZA* sio mzuri sana;

2. Kamati inaona kuwa Chuo cha Uongozi wa Fedha kwa hivi sasa kimejijengea sifa kubwa kutokana na ufanisi na uendeshaji wa chuo hicho kwa ujumla na haioni tatizo la kiuendeshaji lililopo katika chuo hicho;

3. Maalum zinazohitaji umakini na uangalifu mkubwa katika kuziendeleza na kuzidumisha kiufanisi. Kukichanganya Chuo hicho na Chuo cha *SUZA* kunaweza kupelekea kuzivisa fani hizo na kudumaza taaluma za masuala ya fedha kwa ujumla;

4. Kwa hivi sasa chuo hiki kipo chini ya Wizara ya Fedha ambayo pamoja na mambo mengine ndiyo yenye dhamana ya kusimamia uingizaji wa fedha katika taasisi mbali mbali za Serikali. Hivyo, Kamati inahisi kuwa upatikanaji wa fedha katika chuo hiki kwa hivi sasa ni wa uhakika zaidi, kwa vile “aliye karibu na waridi haachi kunukia”;

5. Nia hii ya Serikali ya kuviunganisha vyuo vyake na *SUZA* inaweza kuviua vyuo hivi, ambavyo kimsingi ni muhimu sana katika kuziendeleza taaluma mbali mbali zenye umuhimu wa kipekee hapa nchini. Aidha, azma hii inaweza kuua ushindani wa vyuo kitaaluma ambao unasaidia sana katika kuvikuza vyuo vya juu katika nchi yoyote.

MFUKO WA BARABARA

Mhe. Mwenyekiti, Mfuko wa Barabara una jukumu la usimamizi wa fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara hapa nchini, ambapo kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014 Mfuko huu uliidhinishiwa ruzuku ya jumla ya Shilingi Elfu Sita, Mia Tisa na Tatu milioni (Tsh 6,903 milioni), kati ya fedha hizo, Shillingi Elfu Sita na Arubaini na Sita Milioni (Tsh 6.046 milioni) ni kwa ajili ya matengenezo ya barabara na Shilingi 857 milioni kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi.

Mhe. Mwenyekiti, wote ni mashahidi kuwa barabara nyingi hasa za mjini zimekuwa zikikumbwa na tatizo la kukaa na ubovu kwa muda mrefu bila ya kufanyiwa matengenezo, kana kwamba wahusika wa matengenezo ya barabara hizo hawaoni au hawapo, wakati ambapo fedha kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo barabara hizo zinakuwepo. Kuchelewa kuzifanyia matengenezo barabara zetu kunakua ni kero kwa watumiaji kwa kusababisha usumbufu wa kupita katika barabara hizo, bali pia inakuwa chanzo kwa baadhi ya ajali zinazotokea katika barabara hizo na pia zinakuwa ni chanzo cha kuharibika mara kwa mara kwa vyombo vya usafiri vinavyotumia barabara hizo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, inathamini sana jitihada zinazoendelea kufanywa za kuzifanyia matengenezo baadhi ya barabara zetu hivi sasa. Hata hivyo, kamati inauhimiza uongozi wa Mfuko wa Barabara kuzidisha mashirikiano kati yake na taasisi zinazofanya matengenezo katika barabara ikiwemo *UUB*

pamoja na kuharakisha taratibu zinazohitajika ili zile barabara zinazohitaji kufanyiwa matengenezo ziweze kufanyiwa matengenezo stahiki kwa wakati unaotakiwa bila ya kuchelewa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande mwengine, Kamati inatoa wito kwa wananchi kuzitumia vyema na kuzitunza vizuri barabara zetu, ili barabara hizo ziweze kudumu kwa muda mrefu zaidi na kupitika bila ya usumbufu. Tukumbuke kuwa ujenzi na matengenezo ya barabara ni kazi zenye gharama kubwa na hivyo basi, Serikali yetu inatumia fedha nyingi kugharamia shughuli hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, kupitia vyanzo vyake vya ndani wizara hii inakadiria kukusanya Shilingi 6,007,500,000. Kwa upande wa matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015, wizara hii imetengewa jumla ya Shilingi 36,067.70 millioni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, kwa upande wa kazi za maendeleo wizara inakadiriwa kutumia jumla ya Shilingi 41,496.50 millioni. Pia, Shilingi 69,825.92 millioni kwa ajili ya Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, idhini ya mapato na matumizi ya fedha zote hizo imeshaombwa mbele ya Baraza lako tukufu hivi punde. Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imeyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2014/2015, na ninawaomba Wajumbe wako waijadili, watoe mapendekezo yao na hatimae kuipitisha bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini na utulivu mkubwa wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba yangu.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kunipa nafasi hii yale na nilikuwa nikiisubiri sana wizara hii, sikuikamia isipokuwa nimeisubiri sana kwa sababu hapa ndipo pa kueleza taaluma zetu hasa sisi tuliopita kusoma soma na kujaribu kutafuta elimu.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza sina sifa za kumsifu mtu kama hana sifa na hata nikifika pahala kumsifu mtu basi sifa anakuwanazo. Kwanza mimi niingie ukurasa wa 14 Idara ya Uhakikimali. Nataka niwapongeze sana kwa jitihada zao na hii ni moja katika hazina kubwa kwa Wizara ya Fedha na hasa katika uratibu wao wanaofanya katika shughuli ambazo zinatafiti masuala ya ununuaji na utumiaji vitu chakavu na kuweza kuvitolea ruhsa kwa watu ambao wanataka vitu hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kuwa bado idara hii hatujaipa nguvu na nikisema hivyo naamini kuna baadhi ya sheria zinataka kufanyiwa maboresho. Sasa Mhe. Waziri, aangalie katika maeneo ya utendaji wao kuweza kutunga sheria ambazo zitaweza kuwapa nguvu watu wa aina kama hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, vitendeakazi bado viko duni na naamini hata gari za kwendea *field* hawana. Mimi naamini hivyo na hii ndio wizara yenyewe na hawa ndio wahusika, naomba sana watafutiwe vitendea kazi kwa mujibu wa wakati. Sasa hivi tunakwenda na sayansi na teknolojia kwa hivyo tuwaone. Nashangaa sana wafanyakazi hawana hata ile *laptop,* kwa sababu kuna vitu sasa hivi unaanza kuviangalia katika mtandao na baadhi ya mambo na wakaweza kuweka *data* zao kwenye mtandao ambao wamehusika wao wenyewe na wakajua siri zao. Mimi naomba sana tuwape fursa hizo ili waende na wakati.

Pamoja na haya ninaamini kuwa bado wanataka taaluma tusiwanyime haki zao za kupata taaluma ili kuwaongezea ufanisi hasa tukiweza kukopi katika nchi nyengine, wakiwa na *system* kama hii au wakiwa na idara ya aina kama hii. Ningeomba sana Mheshimiwa tuweze kuwafanikishia mambo haya.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 27 nimeona kuhusu mradi wa ujenzi wa meli na nimeona kutokana na Serikali ilivyotenga fedha zenyewe, lakini nataka nimuulize Mhe. Waziri ni lini meli hii hasa katika haya masuala mliyotiliana mikataba itakuja Zanzibar. Wazanzibari wanaingojea kuishangiria meli hiyo na kwa kuwa Serikali imeona kuwa iko haja ya kuweka chombo hiki kwa kuwasaidia Wazanzibari kutoka upande wa Pemba kwa sababu kule ni *deep sea*, ni bahari kubwa sana. Ninaamini Serikali imechonga kutokana na uzito wa ile meli yenyewe, naomba Mhe. Waziri, hapa aje aogelee kwa sababu yeye namuamini kabisa, anakuwa na lugha nzuri tena tamu, lakini hapa aje atueleze hii meli itawasili lini ili Wazanzibari waweze kunufaika na meli hii.

Mhe. Mwenyekiti, mradi wa uimarishaji wa maeneo ya Fumba. Hii baadhi ya wakati inakuwa ni maelezo tu, lakini hasa hatujaonesha miundombinu kule Fumba, jinsi gani ambavyo tumekusudia ile dhana au lengo lenyewe hatujalifikia bado, tunachelewa nini Mheshimiwa, hatujaweka maji na umeme, hatuja *design* masuala kama hayo, sijui inakuwa ni sababu gani. Naomba Mhe. Waziri, aje aniambie hili suala linakwazwa na kitu gani wakati lengo la kuweza kupata fedha, la kukaa akatuletea *briefcase* yenye *hundred billions* sehemu zenyewe ndio kama hizi. Lakini yeye anatwambia tu kwamba ana shilingi bilioni mia moja, lakini haitambulikani kianzio kipi na kipi ambacho kinaweza kikatusaidia. Tunaomba sana miundombinu na mara nyingi sana tangu nilipokuwa kwenye Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa kweli kulikuwa hakuoneshi dalili ya kuweza kufanikisha, tuna mwitu tu, tunafuga chui kule? Mimi naomba tuweze kufanikisha.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 35, *ZRB*. Pamoja na sifa zote, lakini bado tungali nyuma sana katika ukusanyaji wa mapato. Siku moja nilikwenda hoteli moja *Zanzibar Beach Resort*, nilimuona *accountant* pale anasema hii *ZRB* inasumbua, sasa mimi nikasema ama hii jeuri tena kubwa, kwa kuwa *ZRB* wanafanya kazi zao yeye anasema asubuhi anakuja Juma na jioni anakuja Haji anataka *document*. Sasa kwa kweli hili suala linasumbua sana, mimi sina ugomvi na *foreigners,* nataka nieleweke, lakini nina uchungu sana kukosa mapato yetu. *ZRB* anafanyakazi kwa mujibu wa sheria iliyotungwa ndani ya Baraza hili, usione tabu wao kuingia wakati wowote mlango wako ukawa wazi kwa sababu ndio utendaji ulivyo na ndio maana wanafikia malengo.*(Kicheko)*

Sasa tuseme ukweli, kuna hoteli zina mikono yenu mawaziri hio wala sio siri na ndio maana tunawapa kiburi hawa ma-*foreigners,* ondoeni mikono nitakuja kuwasema hapa kwa sababu ninawajua kwa *timetable*, ninakwambieni, kwa sababu hawa *foreigners* wana jeuri. Kuna Mhe. Waziri mmoja Mr. X, aliendewa na wafanyakazi wa *labour,* basi alipiga simu tu kwa Mhe. Waziri mwengine, kama ananisikia leo atanisikia baadae atanipa ki-*note* kunambia Mheshimiwa pale umeniumbua; alisema hebu achia hao baada ya muda fulani wanamaliza waondoke, hapo tumeshakosa pesa za mapato.

Mhe. Waziri, jitihada zake zinafika pahala mimi naamini yeye hayumo kwenye hizo hoteli hamna mkono wake, naamini hivyo na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu amjaalie hivyo hivyo aende peponi kwa hilo. Lakini wenzako wanakwendea kinyume hupati mapato Mheshimiwa. Hapa kuna jambo moja la kuchekesha huku *OC* iko shilingi bilioni tano (5,000,000,000), mishahara shilingi bilioni nne (4,000,000,000), hapa kidogo nakuwa nashangaa sana sijui vipi kwa sababu *certificate* ya uchumi mpaka leo sijakabidhiwa, lakini mimi hapa inanitia kizunguzungu ukurasa wa 57, hebu nije nielezwe. Halafu leo akinambia *OC* shilingi bilioni tano na saba juu baadae inakuwa ile *percentage* inashindwa ku-*complete, why*? Naomba Mheshimiwa aje anieleze hapa anipe taaluma, mimi namjua Mhe. Waziri, hodari sana kumsomesha mtu akamfahamu.

Sasa *ZRB* wanajitahidi watendaji wake chini ya usimamizi wa Mhe. Waziri, mwenyewe mkuu, lakini wanashindwa kufanyakazi ukweli ulivyo ni huo, wanaona haya kukwambia, mimi sioni haya kwa sababu ndio kula yangu kusema ukweli. Watu wako hawa wanakumbwa na vikwazo vinavyohusiana na sisi wenyewe viongozi. Namuomba Mheshimiwa Mohamedraza, hebu lipeni kodi, naomba sana hawa wawekezaji wetu wa ndani humu, hebu lipeni kodi na Mheshimiwa Mohamedraza anzeni kuonesha mfano nyinyi kulipa kodi kwa wakati unaotakiwa kubalini mpekuliwe, *I'm serious* kabisa sio tufanye mchezo kwa sababu kila siku tunakuwa tunasema uongo, mnamsemesha uongo waziri chini kuna watu ambao hawako *willing* ya kutaka kulipa hii kodi.

Ushauri wangu bila ya *foreigner*, unda Kamati ndogo kama sheria inakupa ruhusa na sisi tukija mle ndani tukakutizamie kodi wala usione tabu, unda Kamati maalum kwa operesheni. Operesheni sakasaka wasiolipa kodi hilo ndio jina lake. Hiyo sio tabu Mhe. Waziri, itakusaidia wewe na itakuwekea heshima kubwa na itaweka heshima ya Serikali yetu, fanya hivyo usione tabu tuko *free* hatutaki chochote usitulipe, hiyo lazima tusitake pesa tuna uchungu wa nchi tunataka watoto wasome, tunataka watu mishahara yao ipande.

Sasa mimi naomba Mhe. Waziri, ajitahidi sana katika hilo na niwape pole sana watu wa *ZRB,* malengo wanafikisha vizuri, lakini wanapata vikwazo wenyewe, hawavisemi, mimi naviona tena naviona kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye *TRA*. *TRA* Zanzibar niwapongeze kwa jitihada zao za kukusanya mapato ambayo kwa asilimia zinazowekwa, lakini kuna moja linanisikitisha. Zanzibar *TRA*, Tanzania Bara *TRA*, kwa nini wanapoamua *value* ya hapa inakuwa hai-*play* kule? Mhe. Waziri, anajitahidi nimemsikia juzi kwenye vyombo vya habari alisema sana, lakini kuhusu habari ya makontena sitaki kuisema pengine tunafanyiwa *teaching* wenyewe,

tunageuzwa na kugeuzwa kwa kutumiwa jina la Zanzibar na inawezekana makontena yale yakawa sio ya Zanzibar. Sisi tumeona kama ni ya Zanzibar, hilo mimi silitii mkono naliacha kama lilivyo. Mheshimiwa umeshapewa hoja nzuri na leo utakuja kutupa hoja nzuri ya kuwaridhisha Wazanzibari kutokana na tukio lililotokea lile la makontena kuwaambia ukweli ulivyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi Mhe. Waziri, ninamuamini, katika mawaziri wawili hapa kidogo wanatuchangamsha kwa mambo mazuri yeye na Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, wanakuwa wanasema kitu cha kweli kabisa. Hiyo sio siri wala si ajabu kabisa, kwa sababu unajua wakati mwengine Rais anakuwa hafumbi macho akichagua viongozi, anachagua kweupe tena asubuhi hakuwachagua usiku. Hivyo ndivyo inavyotakiwa, lazima uwe muwazi katika utendaji wa kazi, hiyo ndio sifa ilivyo.

Sasa mimi naomba kutokana na hali halisi ilivyo niwasifu sana ndugu zangu wanajitahidi, wastarehe hapa, lakini hali halisi wanashindwa ku-*compete* na wale kule wenzao inaonesha kama wanakuwa wanapewa heshima. Naomba hilo Mheshimiwa atuweke sawa atusawazishe.

Mfuko wa Barabara mpaka sasa hivi naona hatunufaiki nao, wengine wananufaika lakini wengine hatunufaiki maana mpaka leo hii hatujamaliziwa barabara zetu za ndani. Mimi naomba yeye ndiye Mheshimiwa watwambie *system* gani wanayotumia na sisi Wawakilishi tuweze kupata Mfuko huo kuneemeka nao. Mhe. Waziri, aje atwambie Wawakilishi tupite njia gani hata tuweze kunufaika kwa sababu tuna barabara mbovu, mama zetu wanazaa njiani kutokana na barabara zile.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Vitegauchumi *ZIPA*. *ZIPA* hapa niseme ukweli, kwanza wizara yako ni kubwa sana, lakini naona watu wachache tu, sijui wengine wanaogopa wamejificha nyuma na hapa ndio pahala ambapo tulitakiwa maafisa wako wasogee mbele wasikie. Kuna wengine wanakuwa hawasikii, wanataka kufahamishwa. Lakini Mhe. Mwenyekiti, naona leo kule *bench open*, hii ndio Wizara ya Fedha kweli! Angalia nyuma mwenyewe uone, ni suala ambalo linatia aibu kubwa sana, halijaridhisha kutokana na *attendance*, tofauti na wizara nyengine. Tazama Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati jana ilivyojaza hapo. Lakini leo naona wote wapo nyuma wanaogopa, sijui wanaogopa hoja gani. Hii inapita tu waambie hakuna wasi wasi wowote.

Mhe. Mwenyekiti, naomba tuangalie sheria hapa kati ya *Labour* na *ZIPA*. Kidogo kuna kitu mimi kinanishinda kutofautisha, labda kwa kuwa kila mtu na taaluma yake na kufahamu kwake au vile vyuo vinavyosomesha *syllabus* zake zinakuwa tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hapa kuna wawekezaji ambao wanapoingia nchini ndipo wanapoomba vibali vya kufanya kazi. Sijui *ZIPA* wao wakoje wanaeleza vipi. Naomba hili nifahamishwe kwa sababu haiwezekani mtu yumo ndani ya nchi unapeleka ombi la kutaka kupata *work permit*, mimi hiki kitu kinanishughulisha sana. Naomba hapa kidogo mnisaidie.

Mhe. Mwenyekiti, niwashukuru sana hawa watu wa *ZIPA* wanafanya kazi vizuri. Halafu ningeomba sana hebu tuwe na elimisho wawekezaji wa ndani na wawekezaji wa nje; tuna manufaa gani katika kitengo hiki cha *ZIPA*. Naomba tupewe semina hiyo. Aidha, tupewe semina Waheshimiwa tuwaelimishe watu wetu. Lakini jitihada ya kupokea miradi nawashukuru sana.

Halafu kuna mengine nawaomba watu wa *ZIPA*, sasa hivi wawe macho sana kati ya wawekezaji na wananchi. Wanaifanya hiyo kazi lakini bado wameregeza kamba kidogo. Kuna wawekezaji wengine wanakuwa ni nduli kwa wananchi. Kwa kweli wanawadhalilisha tena sana, nikitolea mifano mpaka leo suala la Nyanjale halijapatiwa ufumbuzi, na kamati imekwenda hakuna suluhisho.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana pale pana mgogoro mkubwa kati ya *investor* na wananchi. Sasa tuangalie na hii tuwape taaluma wananchi wetu jinsi gani *investor* umuhimu wake kwa wananchi. Hili ni jukumu lenu watu wa *ZIPA* kuwaelimisha kabla hujatoa mradi. Hii naomba sana jamani, nakupeni ushauri wa bure. Hii nakwambieni ni jambo muhimu sana, mnapokuwa tayari mumeshaamua eneo gani mnataka kumpa *investor*, wakusanyeni wananchi waelimisheni na yule *investor* mumwambie sheria zetu za Zanzibar zipo hivi na hivi.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hizi za *ZIPA* bado zipo *weak*. Naomba sana tuziangalie kuweza kuziboresha ziwe na viwango. Wanafika pahala wanagonga huko, hata wenyewe wanagonga ukuta huku kutokana na sheria. Sasa mimi

nawapongeza sana kuwa taaluma hii ya kuwatafuta hawa wananchi, suala la Nyanjale mpaka leo halijapata ufumbuzi wowote na wananchi bado tunawataka na hasa katika kipindi cha kupiga kura. Sasa na sisi huyu mtu ni *transit* tu anaweza akasema leo mimi naondoka akatuachia nchi yetu iko pale pale.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze sana katika jitihada zao za kutafuta *funds*. Lakini mimi niliwahi kutoa ushauri siku moja msidharau jamani ushauri wetu, hasa mimi kichwa changu msidharau. Mhe. Mwenyekiti, kuna wengine Mwenyezi Mungu anawajaalia *nature* ya kufahamu na kuona jambo la msingi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilisema hebu jigeuzeni mifumo ya kuwa na benki. *PhD* ya Mwenyezi Mungu ninakuwa nayo. Twende na mifumo tuwakopeshe hawa watu wetu wafanyakazi ambao wenye mfuko ule. Mhe. Mwenyekiti, mishahara hatupandishi, basi hata kuwakopesha kwenye mfuko huu. Naomba sana Mkurugenzi husika wa *ZSSF* awasaidie hawa watu wakopeshwe fedha zao angalau ziweze kuzunguka.

Mhe. Mwenyekiti, halafu nilisema sheria hii Mhe. Waziri sasa hivi ya kungojea mtu miaka 60 ipo mbali sana. Kwa nini tunaona tabu kuweza kugeuza? Kwa sababu kuna watu wanafukuzwa makazini na hasa kwenye mahoteli. Au tuwasamehe watu wa mahoteli mimi nakubaliana nalo. Tuwasamehe watu wa mahoteli kwa sababu mtu wa mahoteli ndani ya wiki moja, mwezi mmoja *one mistake* anafukuzwa kazi, *disappear* pesa inakuwa haipati tena. Sasa kama ni hivyo basi bora tuwasamehe. Ikiwa unawataka basi watengenezee mazingira ya sheria, ili wakifukuzwa waweze kupata haki yao.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kiwanja chetu cha Kariakoo kesho kutwa kitakuwa kizuri sana. Na mnara wetu baada ya muda fulani pale kutokana na ramani *Alhamdulillah* wametugeuzia, mimi nawashukuru sana. Na hiyo *plan* ya *shopping mall* tunawashukuru na wao waende mbio mbio ili waweze kugeuza maduka yetu yawe maduka ya kisasa na watu waweze kufanya kazi ya biashara hii. Ninashukuru sana hilo suala Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nilisikia hivi karibuni wametoa matangazo ya vibanda vya watu kukodisha hayo maduka shilingi 50,000/=, vibanda vya kawaida shilingi 30,000/=, halikadhalika na masuala mengine. Mhe. Mwenyekiti, hatujui maduka sasa hivi yapo mangapi na vibanda hivyo vipo vingapi.

Mhe. Mwenyekiti, niingie katika Benki ya Watu wa Zanzibar *(PBZ).* Mhe. Mwenyekiti, benki hii inaendeshwa vizuri sana, inajitahidi hadi vichochoroni kufungua matawi. Lakini Serikali tuliwaomba siku moja kuwa na wao waongezewe mfuko, Mhe. Waziri umefikia wapi. Naomba sana nijue hii benki katika walioomba na wao angalau waweze kupambana na mabenki mengine, ili Serikali ioneshe pale jitihada zake imefikia wapi. Na kama huna fedha Mhe. Waziri tujibu utwambie sababu gani huna na wakati wewe unatwambia una vianzio.

Lakini nilisema kuwa *CBOs;* hawa watu wadogo wadogo wajasiriamali, na ile sheria sijui iko wapi. Ninaomba sana ikiwa tayari njooni huku chini Mheshimiwa mtusaidie mikopo midogo midogo, wajasiriamali wadogo wadogo wafanye biashara ndogo ndogo. Wenzenu sasa hivi wanashuka, *KCB* wanashuka, *CRDB* wanashuka, nyinyi basi mnataka kukaa kwenye viti vya kuning'inia tu hivi, haiwezekani tafuteni biashara.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia benki ya kinamama nilisema mimi, nina uchungu sana na kinamama, hawa kinamama ndio waliotuzaa. Wenzetu Bara kule wameshafika katika malengo makubwa, hebu tuigane. Mhe. Mwenyekiti, tulizungumzie suala la benki ya kinamama. Kinamama kwanza wao ni *population* kubwa, wao ndio wengi waliokuwa maskini. Kwa nini tusiwapatie benki yao? Mhe. Mwenyekiti, nitapiga buti hapa, nazuia fungu. Nieleweshwe kwa nini kinamama mpaka leo tunawasumbua hatuwapatii benki yao. Hawa hamtaki tuwe sawa sawa na kinababa katika maisha? Tutawadhalilisha tu mpaka lini?

Mhe. Mwenyekiti, naiunga mkono robo tu, atakapokuja kuniambia Waziri mpenzi nitammalizia pesa zake. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Mjumbe alipokuwa anazungumza alikuwa anasema kwamba watu wa Wizara ya Fedha hawatoshi. Watu wa Wizara ya Fedha wapo wengi kuliko Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi humu ndani. Wale pale juu, hebu simameni wakuoneni. Kaeni kitako. Ahsanteni.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutupa pumzi hizi tulizokuwa nazo, na kuendelea kuwa nazo kwa uwezo wake na kuhudhuria katika Baraza lako tukufu ukawa unatuongoza. Mhe. Mwenyekiti, na mimi nichukue nafasi hii nikushukuru kwa dhati kabisa kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuyazungumza haya ambayo nimekusudia kuyazungumza.

Mhe. Mwenyekiti, hii inaelekea ni bajeti yangu vile vile kutokana na utaalam. Kama bajeti iliyokuwa ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, basi hii Wizara ya Fedha pia inatugusa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri Mhe. Waziri atakapokuja kwa heshima, namheshimu sana, kaka yangu, mwenzangu, ndugu yangu, pamoja na watendaji wake wote, leo lazima tupate tamko la Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, sisi wafanyabiashara nikiwemo na mimi mfanyabiashara mwenzao Raza, lakini hapa nimesimama kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini. Tubadilikeni wafanyabiashara kwa kusaidia kulipa kodi. Kwa sababu humu ndani sote kelele zetu tunamwambia Waziri wa Fedha mhusika; dawa hakuna, maji hakuna, umeme hakuna, pampu imeungua. Mwananchi ambaye hana uwezo anaandikiwa dawa hospitali akiambiwa hakuna ni sawasawa unamwambia kufa. Maana yake Mhe. Mwenyekiti, yule mtu anayetoka kijijini hae hoi uwezo wake ni ukulima akenda hospitali akiandikiwa dawa hizi, halafu anaambiwa dawa hizi nunua, au dawa hazipo, maana yake unamwambia kufa.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri Serikali yetu hii ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa, asitizamwe mtu kwa ukada wake, ikiwa kada wa CCM, ikiwa kada wa CUF sheria ifanye kazi, nchi hii katika makusanyo ya kodi.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mhe. Waziri, Wazanzibari sisi hasa wafanyabiashara si kila anayepepesuka mlevi, lakini kumekuwa na tabia ya kuona kama kodi ni jambo ambalo si lazima, matokeo yake tunakwenda kuwakamata wale *taxi driver* ambao wazee wana magari yao. Wale walikuwa wasamehewe hasa hata shilingi 50,000/= wasizilipe. Ni watu wazima wamestaafu wanakaa na *taxi* zao hata shilingi 10,000/= hawapati. Kwa hivyo, mimi ushauri wangu kwa Wizara hii ya Fedha, na kwa kuwa uwezo wa kusimamia hii upo, kwa sababu hawa watendaji wote *TRA, ZRB* na sehemu nyengine za ukusanyaji wa kodi ni watu wana uwezo, wana hekma, wana busara.

Mimi niwapongeze kwa dhati kabisa, lakini sasa kuwepo na operesheni maalum, tubadilikeni. Kwa hivyo, vyombo hivi vianze kutoa elimu kwa wafanyabiashara. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, hizi kelele zote unazozisikia humu ndani, huyu anasema barabara, huyu umeme, hii yote hae hoi Serikali, na Serikali ni wafanyabiashara. Sasa mimi nafikiri tuwe na utaratibu maalum.

Mhe. Mwenyekiti, *ZRB, TRA* na sehemu nyengine nawapongeza Makamishna wote kwa hekma, busara na usikivu. Lakini pia na sisi akina Raza angalau tubadilikeni, ili kusaidia hii Serikali yetu. Mhe. Mwenyekiti, uwezo huo wanao. Mimi naweza kuthubutu kusema asilimia kubwa sana ya wafanyabiashara wengine hata hawajui *pay as you earn*, lakini wafanyakazi wa Serikali na Mashirika wao hawajafika mwezi pesa zao zimeshakatwa.

Sasa operesheni kama hizi tusiweke tu kwenye Mashirika ya Serikali na Serikali. Kwa hivyo, tuwape elimu; kuna wafanyabiashara wengine wanafahamu kazi zao, lakini tukikusanya pesa hizi za wafanyabiashara kwa utulivu, kwa amani, sio kufunga maduka tutafanikiwa pakubwa sana lakini Serikali itoe tamko. Aanze tuliokuwemo humu ndani akina Raza, pata watu wa ndani halafu watu wa nje, hivyo ndio tutaweza kufika.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mapato mimi kwa Zanzibar sina tatizo kabisa. Nataka niwaambie tu Wajumbe wenzangu wa Baraza hili tukufu, mapato yote ya Zanzibar yanabakia Zanzibar. Hakuna pato la Zanzibar linakwenda Bara. Mimi kama mchumi, mfanyabiashara naelewa haya.

La pili, hili suala la vitega uchumi, kufanya kosa si kosa kosa kurejea kosa, na hili halikuwa la Waziri wa Fedha. Kipindi cha nyuma kilichopita kuna baadhi ya wafanyabiashara kama huyu *Venta Club* alikuwa anadaiwa mamilioni ya pesa; pesa ameshachukua ameshafanya biashara akaachiwa tu akakusanya mamilioni. Ninakumbuka na tarehe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, Mkuu wa Shughuli za Serikali aliwaita ofisini kwake watendaji, ili kwenda kumkamata yule mfanyabiashara *owner* wa *Venta Club* akalipe zile kodi ambazo amekuwa

amekusanya. Matokeo yake haikufika jioni watendaji aliowaita Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa nia moja, watendaji wake katika aliowaita mmoja alihakikisha anamsafirisha usiku wake kumuondosha hapa Zanzibar. Matokeo yake Serikali imekosa mapesa yale. Serikali imeingia hasara zaidi ya milioni 400 kwenda kuwalipa wakulima waliouza mboga mboga, samaki, kuni kwenda kufidia yule Mtaliana.

Alikuwa amechukua pesa na akaondoka pesa zikawa hazijalipwa, kesi ikenda Mahkamani, Wazanzibari wakawa wanadai, Serikali ikaingia tena mzigo mwengine wa kulipa. Na huku tuna matatizo ya dawa, huku tuna matatizo ya barabara, huku tuna matatizo ya maji.

Mhe. Mwenyekiti, hata mimi nilipoambiwa nibadilike nilibadilika. Mhe. Waziri wa Fedha aliniita akaniambia Raza anza wewe kubadilika basi, na mimi nilibadilika na nilimheshimu, kwa sababu Serikali ni usikivu. Kila mfanyabiashara anachokifanya asubuhi mpaka usiku Serikali inajua kila kitu. Raza hapa kapunguza ngapi, Jecha kapunguza ngapi, Mussa kapunguza ngapi. Serikali yetu inataka amani na utulivu. Lakini mimi ninachoomba kwamba itolewe taaluma tuwaachie watu watengeneze kazi ya kufanya.

Mimi nafikiri *ZRB* hivi vitu vya *pay as you earn* na mambo mengine kama leseni na vyenginevyo wakaachiwa wao wafanye hiyo kazi. Tutafika pazuri, tutajua tuna nini.

Mhe. Mwenyekiti, narejea tena watendaji wote wa Wizara ya Fedha katika kukusanya mapato ni watu wenye uwezo Mwenyezi Mungu amewapa kipaji, Mwenyezi Mungu awazidishie kipaji, wanazungumza, wanafahamu. Sasa Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Waziri wa Fedha aende na mambo kama haya.

Pia na hili kuwe na tahadhari, nilisikia tu mimi sitaki kuingia sana hili sokomoko kubwa la makontena. Sasa ninachosema taratibu tu zifuatwe. Lakini mtu anapoambiwa fungua kontena ufungue kontena. Nasema kuna taratibu Waziri wa Fedha anaelewa, Serikali inaelewa. Huku tuna matatizo ya dawa tunafahamu kwamba Zanzibar tuna-*raise pressure.*

Mhe. Mwenyekiti, nataka nikuhakikishie hakuna mfanyabiashara wa Zanzibar anijie mimi aniambie amekula hasara. Afueni tunaipata Zanzibar hatuipati Afrika nzima ya kontena, huu ndio ukweli. Kwa hivyo, nilikuwa naomba wafanyabiashara wasije wakawazidishia hawa mama zetu, baba zetu nguo za watoto waseme *TRA* wanatukomoa. *TRA* wanatukomoa?

Nani anayelipa hapa aje aniambie mimi kama alilipa amelazimishwa. Kwa hivyo, nafikiri tusichukue jambo kila kitu tukaipaka Serikali matope. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, ninachoomba nguo hizo sehemu zote hakuna ushuru uliopanda Zanzibar. Kama gari tunatia dola 1000 hapa ndio tunacholipia, Bara wanatia gari dola 6000, huu ndio ukweli. Na mpaka leo ndio utaratibu wetu tunaoendelea kwa sababu hii tumewekewa sisi fursa Wazanzibari. Utaratibu wa Zanzibar kwa sababu kuna umaskini, hatuna viwanda, wenzetu wana dhahabu, wana kahawa. Kwa hivyo, Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein ameweka utaratibu maalum kwa Wazanzibari, ili wafanye biashara wapewe upendeleo maalum kama kontena ya kutoa tofauti na wenzetu wa Bara. Tukawaambia Bara nyinyi musituingilie humu. Kama kontena tunakusanya milioni ni pesa zetu. Ikiwa nyinyi munakusanya milioni hamsini, zitabakia hamsini huko. Hiyo ndio uwazi wa serikali yetu Mhe. Mwenyekiti, kwamba hakuna ushuru uliopanda Zanzibar. (Makofi).

Mhe. Mwenyekiti, tuwe wakweli. Mhe. Mwenyekiti, sisi tulikuwa huko chini ndio maana tukafika hapa. Sasa tunapofika hapa tuwaangalie na wenzetu waliokuwepo chini. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, katika mazingira yote hayo, suala la chakula vile vile. Mimi ninataka nimuombe tu Mhe. Waziri wa Fedha, kuna msamaha wa mchele anaosimamia chini ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa huruma za wananchi, kuna msamaha wa mchele, tende, sukari *just it is ten percent*.

Lakini kama hakuna uangalifu mzuri, neema ile ambayo waliyoikusudia serikali haiwafiki wananchi. Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano tunaye Bopar, Bombay Bazaar, Said Salim Bakheressa, Turkey, hawa ni waingizaji wakubwa Mwenyezi Mungu awazidishie awape nguvu. Mhe. Mwenyekiti, hawa wanapoleta zile bidhaa, ninataka nikuhakikishie wao wanatumia nafasi ile ile ya fursa waliyopata ya msamaha kwa kuuza afueni.

Huyu mtu wa pili na wa tatu Mhe. Mwenyekiti, anakwenda kununua *balky***,** mfano kwa Turkey au kwa Said Salim Bakheressa bwana niuzie mimi tani 10, anamuuzia kwa sababu yule ni mfanyabiashara anataka zile biashara ziende kila sehemu. Yule mtu wa pili na wa tatu Mhe. Mwenyekiti, anakwenda kuzifungia kwa sababu amepata afueni kutokana na serikali imetoa msamaha.

Matokeo yake Mhe. Mwenyekiti, ule mchele hauonekani, sukari haionekani, tende zinakuwa zinaonekana, ikimalizika mwezi wa Ramadhani, yule mtu wa pili na wa tatu au wa nne, anakuja kuuza bei kama ile ambayo imelipiwa. Sasa ninataka Mhe. Waziri wa Fedha na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mujue hali halisi ndio hivyo. Hawa wenzetu na ninakuhakikishieni kwa jina la Mwenyezi Mungu Mhe. Mwenyekiti, si jamaa zangu akina Said Salim Bakheressa ni watu ambao wanaipenda nchi, akina Turkey, Bopar na watumia zakka zao hasa katika kusaidia wakati mwengine nchi hii.

Lakini kuna watu kama nilivyosema sio kama anayepepesuka ni mlevi. Hivyo kuna watu wachache wanakuja kuzifungia. Mimi ninachotaka kumuomba Mhe. Waziri Mhe. Mwenyekiti, pamoja kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Biashara, ni watu ambao ninawaheshimu sana hawa.

Mhe. Mwenyekiti, ninakwambia Mhe. Mwenyekiti, kama wizara hizi zitakaa, Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko hata ukimwambia usiku, ukimtajia mtu nani, atakwambia huyu kidogo mjanja, huyu kidogo anachakachua, huyu kidogo mkweli, usiku saa nane muende umtajie majina elfu atakwambia. Kwa sababu tumekaa naye na tumeishi naye na hawa wafanyabiashara tumeishi nao.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo mimi ninataka kutoa tahadhari kwa Wajumbe wangu kuwa kuna baadhi ya makontena ambayo hayana majina ya Zanzibar, wanaweza kutuchafulia hali yetu ya hewa mambo yetu ambayo tusipokuwa makini na akili zetu timamu. Kwa hivyo, ninachoomba hata kama kuna taratibu za TRA na nini, utaratibu tu ufuatwe, ili tuone jinsi gani tunaweza kufika.

Kama huyo mtu kafika Zanzibar anapeleka huko huko, yeye huo atakuwa na hiyari yake. Lakini haiwezekani Mhe. Mwenyekiti, ninataka nizungumze wazi na mimi kwa sababu ni mfanyabiashara, nilitoa dola mia tano gari yangu hapa. Huo ndio ule ukweli ulivyo. Halafu niipeleke Dar es Salaam nikatoe tu ile gari dola mia tano, yule wa Dar es Salaam analipa dola elfu tano, *unless* kuwepo na utaratibu, *it is not fair*. Wakati mwengine sisi wenyewe ndio tunazembea haya mambo mengine.

Kama leo magari yetu ya ZNZ tunalipa mamilioni pale. Sasa inakuwaje magari ya TZ yakija yatembee tu, yasipewe majina ya Zanzibar. Hilo ndilo tatizo letu. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete alisema Dodoma, kwamba Wazanzibari magari yao yakenda kule yanabadilishwa namba, alisema kwenye Bunge Maalum la Katiba.

Sasa mimi ninafikiri Mhe. Mwenyekiti, kuwe na utamaduni wa kukaa kuona ni jinsi gani, tuwazonge wananchi, tusiilaumu serikali, tusitukanane wenyewe bila ya kufahamu haya mambo yanavyokwenda. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi niliona nitoe ufafanuzi wa mambo haya ili na wananchi waelewe.

Ramadhani hii keshokutwa. Huyu aliyesema kishalipa aje kwangu na atakwambia nguo zimepanda elfu thalathini, anijie mimi, halafu na anipe hiyo *entry*, *wallahi* anijie na anipe hiyo *entry*. Si hapa, huku nje. Yule aliyesema kama kalipwa mara kumi anijie, musiwaumize wananchi, huu ni mwezi wa zakka, ni mwezi wa sadaka tusichukulie *advantage* ya mama zetu hawa kutoka shamba. Hawa wanakuja washauza kuni, mboga zao tuwasaidie sote. Hakuna mfanyabiashara anayekula hasara, itokee tu bahati mbaya.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi hapo nije katika sehemu yangu ya pili. Mhe. Mwenyekiti, jana kidogo nilipata mshtuko kwenye....

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika 5 Mhe. Mjumbe.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mheshimiwa Mtume! Haya.

Jana nilipata mshtuko kidogo ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe. Mwenyekiti, mshtuko niliopata, nilisema mwanzo ninayo Katiba hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kwenye ukurasa wa 176 na 177, ibara ya 132 mpaka ibara ya 134.

Mhe. Mwenyekiti, hii Katiba kuhusu suala la ukusanyaji wa pesa ya pamoja ya muungano. Imo ndani, imo kwenye taratibu na mpaka leo kwa zaidi ya miaka 10 haijatekelezwa ambayo tumekubaliana kwa pamoja. Ninafikiri matatizo yote ya muungano yasingeliweza kuwepo leo haya lakini kwa sababu mumetugombanisha, imo ndani ya Katiba, utaratibu mzima haujatekelezwa mpaka leo.

Mhe. Mwenyekiti, kilichonishtua jana. Wenzetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walikuwa wanazungumzia kuhusu sarafu ya pamoja. Jana mswada uliokwenda Bungeni, wanazungumza sarafu moja kati ya *East Africa* na Tanzania. Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo *very sensitive*.

Mhe. Mwenyekiti, mimi tokea kuwepo kwangu hapa sijaona kama sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuzungumziwa suala la sarafu ya pamoja. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, unaposema Tanzania, Tanzania maana yake ni *partnership* na Zanzibar. Kenya, Uganda, Burudi, Rwanda wao hawana mshirika katika nchi zao.

Tanzania unaposema kuna mshirika wake nchi mbili huru zimeungana, *you call* Tanzania. Sasa Mhe. Mwenyekiti, tumekwenda kwenye Bunge la Maalum la Katiba, ninamalizia kuondosha kasoro Mhe. Mwenyekiti, mapungufu ili tupate Katiba ambayo itasaidia nchi mbili kuita Tanzania, muungano uliokuwa imara.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni *very sensitive*. Kuna nchi za ulaya kama Muingereza pale kakataa kuingia kwenye *Euro*. Akasema tushirikiane mimi sitaki. Sasa ilikuwa sisi wenzetu hapa walikuwa wapate ridhaa kwa wananchi, kama si kwa wananchi. Ule mswada na sisi tulikuwa tuletewe kwenye Baraza la Wawakilishi kama ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hili naliona litakuja kuwa sokomoko kubwa sana. Kama tumelifanyia mchezo. Litakuwa kama mfano wa Fungu Mbaraka hili, kwa sababu hii ni suala la fedha ya pamoja. Nilisema kwamba London walijitoa Waingereza. Sasa tusichukulie jambo, huku tuna Bunge Maalum la Katiba tunaeleza mapungufu yetu, huku ndio kwanza munatugonga. Munakwenda kuzungumza mswada, ridhaa ya Zanzibar haujapata.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho. Nilizungumze vile vile, suala hili la mwisho hili la dakika moja, suala la mkopo. Mhe. Mwenyekiti, kwenye Bunge lililopita lilinishtua sana, tuliambiwa serikali imekuwa haina mapato, ipo katika kufilisika. Hiyo imezungumzwa wazi wazi. Sasa ukisema Serikali ya Jamhuri ya Muungano Mhe. Mwenyekiti, inashtua kwa sababu tunakwenda kwenye Bunge Maalum la Katiba, ni serikali ipi. Maana yake sisi Zanzibar tukikopa tunalipa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, wenzetu wanakopa hawa Serikali ya Muungano wa Tanzania, serikali gani inayolipa.

Mhe. Mwenyekiti, halafu la pili tusije tukapandishwa mkenge, tukaja tukarithi madeni ambayo sio yetu. Tunakwenda kwenye Bunge Maalum la Katiba, vitu ambavyo si vyetu. Mimi nilikuwa ninashauri serikali zikae, zitizame mahesabu kabla hatujamaliza huko, ione hesabu ngapi tunagaiwa sisi, hesabu ngapi zipo huko, raslimali zetu zipo ngapi na raslimali zao zipo ngapi.
Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, tunapokwenda huko itakuwa hakuna wa kumkamata. Lakini yakiwepo maandishi na pakiwepo na *terms of reference*, ukiwepo na utaratibu mzuri, kila kitakachokuja kitaonekana ni nani ambaye anadaiwa.

Tukiacha hii, tukenda huko itakuwa hakuna mtu wa kumkamata. Kwa hivyo, ni uzuri serikali zetu mbili hizi zikae zitazame madeni, faida ya muungano. Halafu tunapokwenda huko tuwe tushazifanyia mahesabu kwa hesabu zote yanayohusu mambo ya muungano.

Mhe. Mwenyekiti, *wallahi* ninakushukuru sana, naishukuru Wizara ya Fedha. Mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini na kwa sababu ninawaamini kwamba majibu yao haya nitayapata. Mhe. Waziri wa Fedha kama nilivyomwambia Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, ninaamini kwa niaba ya Jimbo la Uzini, ninaiunga mkono zaidi ya asilimia mia.

Ninakuhakishieni hata siku moja hapa kwa mulivyo nyinyi watendaji mumejenga imani kwa Mwenyezi Mungu, mimi hamunisikii kupiga buti tokea juzi; tokea kwa Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, Wizara ya Kilimo na Maliasili na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaunga mkono hoja. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana mheshimiwa. Sasa nafasi tunampa Mhe. Asha Bakari Makame na Mhe. Mohammed Haji Khalid ajiweke tayari.

(Hapa microphone ilikuwa haifanyi kazi vizuri)

Mhe. Asha Bakari Makame: .....

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hicho chombo naona hakifanyi kazi, hebu aangalie nyengine hapo. Hebu watu wa *system* ndani msaidieni kwenye nafasi ya Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano. Mhe. Asha hebu tuendelee sasa.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli nitakuwa ni mwizi wa fadhila kama sikumpongeza Mhe. Waziri wa Wizara ya Fedha, Katibu Mkuu wake, Makamishna na wale ambao wanawasaidia kwa kazi kwani hii ndio roho ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba pia niipongeze serikali kwa jumla. Kwa nini nikasema niipongeze serikali kwa jumla? Tokeo tulipoingia hapa 2010 mpaka sasa hivi mwaka 2014, kwa kweli imejionesha dhahiri kuwa kila kipindi cha bajeti mambo yanabadilika.

Kwa sababu gani mambo yanabadilika, ni kwa sababu ya kutoa maelekezo kwa Wajumbe wako wa Baraza hili tukufu kupeleka Wizara ya Fedha na kwa kweli wizara hii wanapopewa maelekezo au wanaposhauriwa na Baraza hili, kwa kweli wanajitahidi na wanachukua maelekezo hayo. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi niipongeze tena wizara hii. Kama unakumbuka hapa paliundwa Kamati Teule ya kuchunguza namna gani serikali inavyokosa mapato. Kamati ile kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, ilifanya kazi kubwa sana na baadae ikaleta ripoti yake hapa. Niishukuru sana Wizara ya Fedha kwamba maelekezo ya Kamati ya Teule na mimi nikiwa ni mmoja wapo, kwa kweli waliyafuata na ndio ukaona mapato mengi kwa kweli yamepatikana kutokana na Kamati Teule ile. Niipongeze sana Wizara ya Fedha. (*Makofi*)

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kizuri chochote kile hakikosi ila. Pana mapungufu ya hapa na pale na haya itabidi niyazungumze. Ni imani yangu kwamba wizara hii itayachukua. Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 3, pameelezwa baadhi ya mambo hapa ambayo yanataka kutekelezwa. Kusimamia mali za serikali pamoja na mashirika ya umma.

Mimi niiombe tu Wizara ya Fedha, sio kusimamia tu. Niombe kuwe na kipa umbele maalum ya mambo yetu au mashirika yetu au taasisi zetu ambazo zinaweza kusaidia serikali kwa upande mmoja au mwengine. Kwa mfano, tuna Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano hii, kuna sehemu ambayo serikali inatakiwa ipeleke magari, lakini ukiangalia gari nyingi za wizara hazipelekwi kwenye utengenezaji wa magari katika taasisi yetu ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Waziri, kipa umbele hicho akione. Lakini si hapo tu, kumbi za mikutano ambazo tuna mashirika yetu, tuna wizara zetu wana kumbi za mikutano. Niombe pia hii pesa ndogo ndogo inatusaidia nayo.

Uwekaji wa *furniture* katika maofisi. Tuna wenzetu hapa wanatengeneza *furniture* nzuri sana. Nimuombe Mhe. Waziri kwamba tuwape vipa umbele. Ujenzi wa majengo madogo madogo ambayo tunazo taasisi zetu, zina uwezo huo wa kujenga. Pia ninamuomba Mhe. Waziri aweze kutoa vipa umbele kwa mambo hayo.

Lakini pia nikirudia hapo hapo Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Waziri na nimuombe kwa makusudi, kwa sababu ameeleza katika kitabu hiki kwamba ataangalia vitu vichakavu vya mawizara. Si vichakavu tu Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Waziri ashirikiane na wizara nyengine husika kuhakikisha wizara zetu ukenda

mule ndani utakuta magari yamelala hata hayana maana. Mambo ya *furniture*, magogo yametupwa tu, hata yale mazingira ya kiofisi ukiingia mule ndani hayapendezi. Maana tusionekane hivi wengine tunang'ara mwili tu na kujitia rangi za midomo, lakini mtu ukenda pale mlangoni pake, ukipatizama utajua kama huyu ni mchafu. Kama hapa mlangoni hapatizamwi nje, ukiingia ndani patakuwaje. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri, kuanzia bajeti hii wizara zote wazifanyie utafiti, kama kuna magari hayafai ndio hayafai yatupiliwe mbali, kama kuna makachara ya *furniture* hayafai yatupiliwe mbali. Mtu akiingia ofisini Mhe. Mwenyekiti, aone kuwa nimeingia ofisi ya Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, iwe ni ofisi ya uhakika na yenye usafi wa mazingira. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, hilo nitamuomba Mhe. Waziri, mukae mukubaliane ili mambo haya yaondoke na mambo mengine. Lakini pia nimuombe Mhe. Waziri saa nyengine yananunuliwa magari mazuri tu, lakini *wallahi* gari *clutch* tu, basi itaanza kung'olewa kitu kimoja kimoja mpaka gari itamalizika. Nimuombe katika mambo haya pia tuwe makini na watu wetu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nije katika suala la pencheni na kiinua mgongo na kila nikisimama hapa Mhe. Mwenyekiti, nazungumzia suala la pencheni. Naiomba sana serikali, najua kwamba serikali ina mambo mengi. Lakini miongoni mwa mambo hayo hawa waliostaafu ndio walionyanyua na kuijenga nchi hii mpaka tukafika sisi na sisi tutawaachia vijana wetu.

Kwa hivyo, nawaomba sana Wizara ya Fedha wakae na watafakari, lakini pencheni kwa kweli haitoshelezi. Sasa hivi mtu kwa maslahi ya kujiendesha angalau kidogo. Namuomba sana Mhe. Waziri pencheni wote waangaliwe kwa mujibu wa taratibu na sheria zao za kifedha, ili watu hawa na wao wajihisi kwamba na mimi ni miongoni mwa wale waliotumikia serikali hii, ni miongoni mwa waliotoa jasho lao kwenye serikali hii. Kwa hili Mhe. Waziri nakuomba na nadhani sio mara ya kwanza kulizungumza hili.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende kwenye mashirika ambayo yaliyotaifishwa. Nimuombe Mhe. Waziri kwamba wale ambao bado wataendelea na kazi basi waendelee, lakini wale ambao anahisi kwamba hawa wameshastaafu na wakati wao umekwisha, niombe haki zao zifanyiwe busara. Kwa sababu binadamu anapanga mipango yake kwa mujibu anavyoona yeye mwenyewe, nimuombe sana Mhe. Waziri kwamba suala hili aliangalie vizuri.

Nikitoka hapo Mhe. Mwenyekiti, na mimi niulize tu kwamba meli yetu itakuja lini, nina hamu. Mhe. Mwenyekiti, sasa nije katika *ZIPA*, *ZRB* na *TRA*. Mhe. Mwenyekiti, kwanza niwapongeze sana tena niwapongeze kweli kweli, kwa sababu pamoja na yote lakini watu hawa wanajitahidi, hakuna mkamilifu, dosari za hapa na pale zipo. Lakini mimi nichukuwe nafasi hii kuwapongeza kwa dhati kabisa.

Tuangalie toka tulikotoka, nilisema mwanzo na mpaka hapa tulipofika ni kwamba wanajitahidi tena wanajitahidi. Ni lazima watatokezea wale wadogo wadogo ambao wanafanya mambo yao, mimi nasema niwapongeze. Pia niipongeze *ZSSF* kwa kweli nitowe pongezi za dhati kabisa, *ZSSF* inafanyakazi vizuri na kwa kweli wanastahili sifa.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niingie katika suala la miundombinu; kuna wawekezaji wetu hawa niiombe sana wizara hii na serikali kwa jumla, kama hatujawa tayari basi mwekezaji kwanza tumuache, pamoja na kwamba tunataka fedha. Lakini pahala popote ambapo tutampa mwekezaji basi tuhakikishe miundombinu imefika yote yakiwemo maji, umeme, barabara na mambo mengine madogo madogo, ili kumpa moyo mwekezaji kuona kwamba kweli tuko tayari kuekeza Zanzibar.

Haya Mhe. Mwenyekiti, yametokea huko nyuma, lakini sasa hivi niishukuru serikali kwamba imefanya kazi kubwa sana, sehemu nyingi sana zimefika barabara, umeme, maji na kadhalika,. Niishukuru sana serikali. Lakini bado tufunge mkaja.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho nimuombe sana Mhe. Waziri, zile mashine za risiti, nakuomba Mhe. Waziri tulilizungumza siku nyingi, lakini usimamizi wa mashine hizi za risiti uwe mzuri na naomba tufanye haraka ili kuhakikisha angalau tunazidisha mapato, kwa sababu ni lazima tukubali binadamu ndio binadamu. Mtu anakwenda dukani hachukuwi risiti, haulizi chochote anapimiwa mchele au anachukua vipolo viwili vya mchele, kipolo kimoja

cha unga na baadhi ya mambo hata haulizi risiti. Sasa hapa tunakosa mapato, nimuomba Mhe. Waziri kwamba suala hili tulisimamie kwa makini.

Baada ya kusema hayo niwaombe wenzangu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa sababu hii ndio roho ya serikali, tuchangie, tukosowe hapa na pale, ili tuweze kuipitisha kwa nguvu zetu sote na tuweze kutimiza ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono ahsante sana.

Ahsante Mhe. Asha Bakari Makame, sasa nafasi nitampa Mhe. Mohammed Haji Khalid, baadaye Mhe. Mgeni Hassan Juma.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kupata nafasi ya kueleza machache sana kuliko wote watakaozungumza juu ya bajeti hii ya Mhe. Waziri wa Fedha. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kuwepo hapa, hasa tukizingatia kwamba wenzetu wengi hawapo kwa sababu mbali mbali, sisi Mwenyezi Mungu katujaalia tupo hapa kwa hivyo ni jambo la kushukuru.

Pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na hatimaye niipongeze Wizara ya Fedha kwa kazi yao kubwa na nzuri wanayoifanya katika ukusanyaji wa mapato. Vile vile niwashukuru sana kwa ile dhana ya *charity begins at home*, wao wameifanya vizuri, kwa sababu hakuna hata idara yao moja iliyopata chini ya 70 katika kuingiziwa fedha, kama na sisi wizara nyengine wangetufanyia hivyo, basi malalamiko kutoka kwetu sisi yangekuwa madogo.

Kwa kuwa wametumia hivyo kuwa sadaka ianze nyumbani, naomba mwaka ujao wa fedha nyumbani mmeshatoa sadaka, kwa hivyo na wizara nyengine muziingizie ili nazo ziweze kufanyakazi vizuri kama mlivyofanyakazi nyinyi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimeitazama kwanza bajeti kuu ya serikali fedha ambazo imepangwa kutumiwa shilingi bilioni 7 na kidogo. Makusanyo yetu ya ndani, nakusudia kwa mwaka uliopita ni shilingi bilioni 365.8 na iliyobakia ni mikopo na ruzuku, yaani mapato kutoka nje ya nchi.

Hii kidogo Mhe. Mwenyekiti, ni hatari kwa sababu hii mikopo na misaada ndio sehemu kubwa tunayoitegemea kwa ajili ya miradi yetu ya maendeleo, sasa kuifanya maendeleo yetu hadi tupate ruzuku, misaada na mikopo ndio tuweze kuendelea. Itabidi tukaze buti tufanye kazi ya ziada kubuni mbinu mbali mbali za kukusanya mapato, ili nchi yetu isijekuwa na ukoloni mamboleo, tusikae na uhuru wa bendera tu lakini ikawa nchi inaendeshwa kutokana na mikopo na misaada kutoka nje, hii itakuwa ni hatari kubwa, tunaweza kufika pahala tutakavyoambiwa vyovyote tukubali ili tuweze kwenda.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, kwanza nitazame kidogo huu ukusanyaji wa mapato kutoka vianzio vya ndani. Hapa pana vianzio kadhaa, ukusanyaji wa mapato kwa ukodishwaji mashamba ya mpira, yamewekwa makadirio ya kumi na tatu kumi na nne mia moja na sabini na tano milioni, lakini hakuna tulichokusanya, lakini kwa mwaka ujao tumeweka milioni 160.

Mhe. Mwenyekiti, hapa ningependa niulize kwamba mwaka huu uliomalizika hatukukusanya chochote, hii ina maana hakuna shamba la mpira lililokodishwa, lakini mwaka unaofuata tumeweka makisio mengine tena makubwa. Je, tumetumia kigezo gani cha kuona kuwa tuna tamaa ya kukusanya chochote kwa mwaka unaokuja, wakati ambapo mwaka huu uliopita hakuna tulichopata kutokana na chanzo hiki cha mapato.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ni uuzwaji wa riziki. Tulikadiria kukusanya milioni 28, lakini tumekusanya milioni 3. Tumeweka makadirio ya mwaka mpya wa fedha kukusanya milioni 60. Lakini Mhe. Mwenyekiti, tulikadiria milioni 28 na tumekusanya milioni 3. Pengine niulize kwa nini makadirio haya makubwa na tulikusanya kidogo sana, je tulikuwa hatujajiandaa au hatujajitayarisha au hatukujidhatiti kupata mapato kutoka kwenye chanzo hiki ambacho tumekiweka hapa.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni ukodishwaji wa majengo, tulikadiria tukusanye milioni 32 na kidogo, hatukukusanya hata shilingi moja. Lakini kwa mwaka ujao tumeweka tukusanye milioni 602 na kidogo. Swali langu linakuja pale pale, kwa mwaka uliopita hatukukusanya kitu, lakini tumeweka makisio makubwa karibu mara mbili ya yale ambayo mwaka uliopita hatukupata chochote. Sasa tumekuwa na tamaa gani ya kuweza kukusanya mapato makubwa, wakati mwaka uliopita hatukupata chochote.

Halikadhalika inaendelea hivyo hivyo, isipokuwa mapato yanayotokana na Uhamiaji. Takriban hapa makusanyo ni mazuri na makadirio tuliyoweka kwa mwaka ujao ni mazuri zaidi, kwa sababu hayana tofauti kubwa sana baina ya mwaka uliopita, kilichopatikana na makadirio mapya. Hapa labda niseme mumeongeza utalaamu wa kukadiria, lakini kule kwengine mumekadiria kikubwa, hamkupata kitu na halafu mkaweka kikubwa tena vile vile, sijui kigezo chenu ilikuwa ni kipi kilichotumika.

Mhe. Mwenyekiti, halafu kuna kitu cha mwisho mnakiita mapato mengineyo. Haya mengineyo ni yapi ambayo hayana jina. Kwa hivyo, ningeomba nijuwe haya mapato mengineyo ni mapato gani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kama nilivyosema mchango wangu sio mkubwa sana. Lakini nataka nitazame kidogo kwenye ukurasa wa 20 kwenye Idara ya Mipango Sera na Utafiti, kwenye kifungu cha 35(1). Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki kinasema hivi hadi kufikia Mei 2014, idara imetumia hiyo iliyotumia kama asilimia 71 kwa kutekeleza mambo yafuatayo.

Kuzifanyia mapitio sheria za *ZSSF* na *ZIPA* katika ngazi ya wizara. Mhe. Mwenyekiti, hili ni muhimu zaidi ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kutaza kufanya marekebisho baadhi ya sheria zake. Sasa ile ambayo inamtaka muajiriwa au mlipaji wa mfuko huu atimize dakika 60 ndio alipwe malipo yake.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hii kwa kiasi fulani inawakandamiza kidogo wafanyakazi, na zaidi wale ambao wanatumikia taasisi za watu binafsi. Mara nyengine watu wanafanyakazi kwa mikataba maalum na kwa muda maalum. Sasa mtu anamaliza muda wake wa utumishi bado hajafika miaka 60, anataka aipate haki yake hii, ili atumie katika kujiendeleza kwa sababu hajafikia umri kwa hivyo haki yake hii haipati.

Kwa hivyo, ningeomba miongoni mwa sheria ambazo zitapitiwa na kufanyiwa marekebisho, basi moja wapo iwe sheria hii ya kutimia umri wa miaka 60 idogoshwe sana. Mimi sio mtaalamu wa sheria wala lolote, lakini popote pale ambapo mfanyakazi kamaliza utumishi wake katika taasisi ambayo alikuwa akiitumikia, basi haki yake hii akiiomba apewe mwenyewe. Isiwe lengo ni kumsaidia uzeeni, iwe lengo ni kumuekea akiba ili anapomaliza utumishi aweze kupata fedha yake aendeleze maisha.

Mhe. Mwenyekiti, kuna watu wamefukuzwa kazi na kuna watu wameacha kazi kwa hiyari yao, lakini huku wamewekeza na wana miaka 30 au 40 fedha zao hawapewi na pengine miaka 60 hafiki atakufa. Kwa nini tungoje aridhiwe wakati mwenyewe yupo na hafanyi kazi tena. Kwa hivyo, ningeomba sheria hii nayo ifanyiwe kazi katika kufanyiwa marekebisho.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 36(5), kinachosema kufanya utafiti wa kuangalia ukubwa wa serikali na mashirika ya umma nchini. Hii nayo ni vyema ikaangaliwa vizuri, kwa sababu hii serikali iliopo ni kubwa sana na jinsi itakavyoongeza ukubwa wa serikali ndivyo tutakavyoongeza matumizi ya serikali. Mapato yetu ni machache lakini tumeongeza watumiaji.

Kwa hivyo, tunafanya matumizi makubwa lakini mapato yetu machache. Kama ingekuwa ni nyumba ya mtu, kipato chake ni *constant* lakini kila mara anaongeza mke na anazaa zaidi, lakini mapato hayaongezeki, basi inafika pahala watoto wawe hawashibi na hawezi kuwasomesha. Lakini kama ataongeza idadi ya watu pia atafute njia nyengine za kuongeza mapato yake, sio kuwa asiowe na aowe mpaka wake wanne aliyoruhusiwa, lakini pia atafute njia za kuongeza mapato na azae watoto wengi kama alivyoruhusiwa, ili tuwe wengi siku ya kiyama Waislamu na twende peponi. Lakini abuni mbinu za kujiongezea mapato ili aweze kuwaongoza hapa duniani.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni *ZRB* na *TRA*, vyote hivi ni vyombo ambavyo vinakusanya mapato. Mhe. Mwenyekiti, vitu viwili hivi au taasisi mbili hizi ziko katika ukurasa wa 35 hii moja ina jukumu la kukusanya mapato ya ndani ya Serikali kuu ya Zanzibar, kwa hivyo hii kazi yake ni kukusanya haya mapato yetu ya ndani, hii nyengine ambayo iko katika ukurasa wa 38 TRA jukumu lake ni kukusanya mapato yatokanayo na vianzio vya Muungano ikiwemo ushuru wa Forodha na vyenginevyo. Lakini pia itakuwa vianzio hivi vyote ambavyo viko ndani ya Zanzibar.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa zote ni taasisi ambazo au bodi ambazo zinakusanya mapato ndani ya Zanzibar kwa nini tusiwe na taasisi moja tu kubwa ya kukusanya mapato, ili kuondosha usumbufu kwa wafanya biashara wetu, hata hii ambayo tumesema inakusanya taasisi ambazo zinatokana na Muungano lakini zimo ndani ya

Zanzibar, kama mapato haya yanabakia Zanzibar basi hakuna haja ya kuwa na Taasisi mbili tofauti ya kukusanya mapato.

Kama hayabakii Zanzbar kwa nini yasibakie Zanzibar wakti ambapo yanakusanywa ndani ya Zanzibar, lakini kama yanabakia kwa hivyo taasisi hii ya pili ya TRA hapa Zanzibar itakuwa haina umuhimu wowote isipokuwa ihahishiwe kwenye ZRB, ambayo ndiyo taasisi pekee ya Zanzibar kubwa kukusanya mapato ya Serikali kuu ya Zanzbar. Tukifanya hivyo Mhe. Mwenyekiti tutaweza kupunguza kwa kima fulani usumbufu wa wafanya biashara wetu kulipa kodi hapa na pale.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimalizie maelezo yangu ya leo kwa kumwambia Mhe. Waziri huu mwezi unaomalizika ni mwezi wa mwisho wa mwaka wa fedha, na ulitulipa mapema sana hatuna pesa tena kesho Ramadhani inaanza, sikwambii utulipe leo lakini jipinde kweli kweli na mwaka mpya wa fedha utulipe mapema vile vile, ili tuweze kuikabili sikukuu, usingojee tarehe za kawaida kwa sababu sisi tunapita mtoni tunatembea katika mto lakini kiremba tayari kimerowa licha ya shuka iliyoko chini. Kama kiremba tayari kimerowa shuka ikojee. Kiremba ni mimi niliyemo humu, shuka ni mwananchi ambaye namuwakilisha huko nitokako na mfanyakazi mwengine wa kawaida na ikiwezekana tukopeshe, ili tukaanzie Ramadhani vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache mimi sina lolote la kusema leo nakushukuru, na naunga mkono hoja hii, ahsante sana.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa na mimi nafasi hii ya kuweza kuchangia machache katika bajeti ya hotuba ya Mhe. Waziri wa fedha. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema ambaye ametujaalia kufika hapa leo tukiwa wazima wa afya. Lakini nichukue fursa hii vile vile kumpongeza sana Waziri wa fedha kwa hotoba yake ambayo ameiwakilisha hapa mbele yetu leo ambayo hutuba hii imejaa matumaini hasa katika kuiangalia hali tuliyonayo. Lakini vile vile kujaribu kutengeneza uchumi wetu kwa hali ambayo itakuwa bora zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, umesema kwamba kama muda utabakia na nafikiri utabakia sana kwa sababu sina mengi sana ya kuchangia kwa sababu kidogo nimeridhika na hii hotuba, lakini vile vile sina budi kuchangia kwa machache lakini kabla ya kusahau vile vile nimpongeze pamoja na niwapongeze wafanyakazi wa Wizara hii ya fedha ambao tunaamini kwamba wamekuwa wakijitahidi katika kufanya kazi zao hasa katika kupanga na kuhakikisha kwamba Mipango ambayo wanaipanga kwa ajili ya matumizi ya fedha, basi itakuwa ni mipango itakayoweza kubebeka na uchumi wa Serikali. Lakini vile vile kufuatilia masuala mbali mbali ambayo yatasaidia katika kuengeza pato la taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze na ukurasa wa sita ambao unazungumzia Idara ya Bajati, Mhe. Mwenyekiti, katika mambo ambayo wanatakiwa kufanya Idara hii ya bajeti mojawapo ni hili ambalo tunalifanya na tumekuwa tukilifanya katika kipindi kizima hiki cha bajeti na suala zima la kuratibu shughuli za bajeti pamoja na uandaaji wa muongozo wa bajeti na mengine.

Sasa Mhe. Mwenyekiti na hili nafikiria hata kamati imeliona ndani ya matayarisho hayo ya bajeti yanajitokeza mapungufu machache na ningemuomba sana Mhe. Waziri haya ayaangalie tena na ajaribu kuweza kuwajengea uwezo wafanyakazi wake ambao wanafanya katika Idara hii, ili kuhakikisha kwamba pale wanapotuletea bajeti, basi bajeti ile kasoro zile ndogo ndogo ambazo zinajitokeza ziweze zisionekane ndani ya bajeti ile.

Nasema hivyo kwa sababu mara nyingi sana katika bajeti vinakuja vifungu, kwanza vifungu vingi ambavyo vinajitokeza vinakuwa vifungu ambavyo vimejifunga, kwa maana kwamba kifungu kile hakijielezi vizuri. Aidha, itakuwa kwa lugha au maana yake tafsiri yake inakuwa sio ambayo inaendana na lile tendo lenyewe. Nafikiri wananifahamu vizuri sana, kwa sababu hili tumeshakuwa tunalizungumzia hata tunapokutana na viongozi Makatibu Wakuu wa Wizara hii. Hilo ni moja.

Vile vile inavyoonyesha kwamba mara nyingi sana hata wale ambao wanaandamizwa yaani wanakuja wafanyakazi wale waajiriwa wa idara hii ya bajeti wanapokuja kufanya kazi pamoja na kamati, tukiwauliza masuala mengine wanashindwa kujibu. Sasa hio pia ni kasoro ambayo inajitokeza kwa sababu kunakuwa hakuna ushirikiano mzuri baina ya watendaji kutoka Wizara ya Fedha ambayo ni watu wa bajeti na sisi wawakilishi, matokeo yake Mhe. Waziri wa Fedha unakuja kuyaona humu ndani barazani.

Kwa hivyo, ningeomba sana watu wako kwanza uwawezeshe, ili waweze kufahamu vizuri namna wanapoandaa ile bajeti, lakini vile vile wakati tunapokaa kama kamati basi washiriki vizuri ndani ili bajeti zile za Wizara ambao wao ni wahusika wakuu waweze kuzifahamu vizuri.

Vile vile katika mapungufu hayo nimegundua Mhe. Mwenyekiti, ambalo hilo lilikuwa nimelizungumza pia hata kwenye kamati kunajitokeza kurudiwa kwa mambo ambayo hayahusiki na miradi ile. Kwa mfano Mheshimiwa mradi unaokuwa hauhusiki kabisa na masuala kwa mfano masuala ya UKWIMWI lakini utaona mfadhili mkuu eti ni Chai, Chai yeye ambaye ni mfadhili anayeshughulika na mambo ya UKIMWI lakini anakwenda kufadhili mfuko wa barabara ambao hauhusiani kabisa na suala hili. Wapo wafadhili ambo wanafadhili hata hao wa mambo ya UKIMWI ambao wanashughulikia mifuko ya barabara au mambo mengine, lakini katika fungu hilo linaonesha kabisa hakuna kifungu cha mambo ya HIV.

Si hayo tu, kuna masuala mengi yanajitokeza utaona mwaka huu yamejitokeza baada ya kusema nimeona kidogo pamefanywa marekebisho, kwa hivyo wahakikishe kwamba hata vile vifungu ambavyo vinajitokeza ndani ya mabuku yetu ya bajeti, wahakikishe wale wafadhili wanaotajwa wanakuwa ni wafadhili sahihi na sio kuweka tu mradi wameweka wafadhili.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niende katika ukurasa wa nane, mimi nimpongeze sana Waziri pamoja na watendaji wake kwa kuweza kusimamia vizuri katika Idara hii ya bajeti na kusema kwamba mradi ambao uko katika mfumo wa PBB ambao unatarajiwa kuanza, ambao tunatarajia sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuweza kupata elimu ya mradi huo, lakini vile vile tumeambiwa kwamba watahusishwa na watu wengine kutoka katika taasisi nyengine mbali mbali zikiwemo taasisi za kijamii. Mheshimiwa ningeiomba sana Wizara na nasisitiza hivi watu ambao mara nyingi wanatusaidia katika shughuli za kutoa elimu katika jamii na masuala mbali mbali ni taasisi hizi za kijamii. Ningeomba sana tena sana kwamba wawahusishe vizuri hawa wana AZAKI waweze kusaidia katika kuendeleza elimu hii ndani ya jamii.

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu wa PBB ni muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi yetu lakini bila ya kuhusisha jamii nzima mradi huu hautofanya kazi vizuri, sasa ikiwa kama tutawahusisha wana AZAKI vizuri nakuhakikishia Mhe. Waziri, kazi katika Wizara yako hii ambayo itakuwa ni ya kutoa elimu kwa jamii basi itakupungukia.

Mheshimiwa vile vile nataka kuzungumzia suala zima ambalo liko katika Idara hii hii ya kufuatilia matumizi ya fedha za umma, suala hili kidogo lina mtatizo kwa sababu linajitokeza sana hasa katika utekelezaji wetu wa ukusanyaji wa mapato na mambo mengine hasa katika makadirio tunayoyafanya. Mimi niseme mwaka huu kidogo tumejishusha lakini inaonesha kwamba yale ambayo tunafanyia makisio kile kiwango cha makisio ambacho tunakikisia mara nyingi kinajitokeza kwamba inakuwa sicho, kwa sababu gani? Kwa sababu makusanyo yake ni mabaya. Lakini pia inaonesha hatupimani kwa kazi zile ambazo tunafanya.

Mhe. Mwenyekiti, juzi tulikuwa na kikao na Ofisi ya Utalii walizungumzia suala zima la *Score card* kwamba kwa mradi ambao sasa hivi nataka kuufanya kutakuwa na *Score Card* kwa maana kwamba kila mfanyakazi atahukumiwa kwa kazi ambayo ameifanya, ikiwa ni nzuri basi atapewa sifa na ikiwa ni mbaya basi atachukuliwa hatua. Mimi ningeomba sana kwamba hii *Score Card* isitembee tu katika maeneo fulani, mfumo huu wa *Score Card* utembee katika Serikali yetu nzima.

Nasema hivyo kwa sababu inaonesha kwamba katika matumizi ya fedha ikiwa katika ukusanyaji lakini ikiwa katika matumizi ya fedha ambazo tunazipangia hapa matumizi yake yanakuwa sio matumizi bora, na kama mipango tunayo kwa nini matumizi yale yasiwe bora na hii inaonesha mpaka kwenye ripoti ya CAG kuna matatizo na sasa kama Serikali haitochukua hatua kuangalia vizuri kina nani wanatuharibia, tutakuwa tunaendelea kulia kilio cha umasikini kila siku. Mimi naamini kabisa Serikali yetu sio masikini. Lakini bado tumeshindwa kufuatilia mapato yetu. Bado tumeshindwa kufuatilia matumizi yetu na kuyasimamia vizuri na ni kazi ya Serikali kufanya hivyo.

Sasa kama hatutowahakiki wale ambao atunawapa majukumu, tukaona kwamba tukisha wapa majukumu wakawa na uwezo wa kutumia na bila ya sisi tukaanza kuwahakiki kiukweli ukweli kutokana na mipango ambayo tumeipanga, sio tu kutokana na kwamba wametumia na kutuletea risiti, mipango ambayo wameipanga wameitekeleza vipi na hii itapunguza mengi Mhe. Mwenyekiti.

Kuna mikataba ambayo tunafunga lakini mikataba ile inakwenda ovyo kabisa, fedha zinazotumika na zinazoharibika ni fedha za Serikali lakini kuna wengine wanajifikiria wao wenyewe binafsi. Sasa Mhe. Waziri nakuomba sana Wizara yako iwe makini katika kusimamia fedha za umma fedha ambazo umezipanga katika utekelezaji basi fedha hizo zitumike vizuri, sio ziingie kwenye mifuko ya watubinafsi.

Mheshimiwa niende katika ukurasa wa 14 na nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa uhakiki wao ambao wameufanya katika mitaji ya umma na tumeanza kuona mafanikio yake. Mimi nimpongeze sana tumeona shirika la ZSTC linavyofanya kazi vizuri, lakini nimeona pia kiwanda cha Sukari ambacho sasa hivi kimeshaanza kufanya kazi, lakini ningemuomba sana kujitahidi katika Wizara yake kuhakikisha kwamba hizi mali za umma zisiwe mzigo wa nchi yetu, lakini hizi ndio ziwe zinatuletea mapato.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa wa 41 kwa kifupi nataka kuzungumzia suala zima la ZIPA. Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Ukuzaji wa Vitega Uchumi yaani ZIPA bado haijafanya kazi vizuri, nasema hivyo kwa sababu wawekezaji wengi sana wanalalamika kwamba wakija hapa wanachukua muda mrefu mpaka kupata kibali cha uwekezaji ukilinganisha na nchi nyingi za Afrika. Sasa tufikirie sisi tunawahitaji wao, lakini sisi tunawawekea vikwazo vingi, hili tumelizungumza na sitaki kumtaja mtu lakini nimeshazungumza nae mpaka mtu ambaye alikuwa anachukua nafasi ya ubalozi, akanambia bado Zanzibar kuna matatizo ya uekezaji. Bado mnayo na hilo linarudisha nyuma wawekezaji ningeomba sana Mhe. Kama kuna sheria, kama kuna kitu chochote cha kuagiza kwa sababu tunaamini na tunajua kwamba hawa wanasafiri sana kwenda nje, kwenda kuitangaza Zanzibar, lakini tunachokipata *value for money* iko wapi kwa fedha ambazo tunazitumia katika kwenda kujitangaza nje, tunahitaji *value for money*.

Mheshimiwa jengine ningeomba sana, hili ni tatizo moja kubwa sana ambalo ninaliona kwamba hata ZIPA wanaweza kulifanya. Mheshimiwa tuna wajasiri amali wengi sana hususan wanawake wanatengeneza vitu vingi sana lakini vitu vyao havina soko. Hatuwezi kuwalaumu wao vitu vyao havina soko, kwa sababu kwanza hawana taaluma ya kutafuta masoko. Lakini vile vile kuna taaluma nyingi kama za usarifu na mambo mengine. Lakini tungeanzisha *centre of excellent* kwamba tunaanzisha kituo ambacho kituo kile kinahakikisha kwamba kinawa-*support.* Kuna wajasiriamali wetu wanatengeneza sabuni, wanatengeneza *lotion* vitu ambavyo ukenda hoteli za nje unavikuta unashangaa kwamba vina harufu na havina tofauti kubwa na vile ambavyo tunatengeneza sisi.

Bahati mbaya vitu vile hapa kweli unaambiwa kwenye hoteli nyingi havitumiki na hili si kosa la wawekezaji, ni kosa la serikali kutengeneza mfumo ambao wale wajasiriamali wataweza kupeleka bidhaa zao pale, ili sasa Serikali itengeneze masoko iwambie wenye mahoteli na wengine kwamba kuna bidhaa kama sabuni, zinaweza kununuliwa hapa hapa badala ya kwenda kununua Afrika ya Kusini.

Sasa hiyo ni kazi ya serikali kutengeneza sehemu ambayo itakuwa wajasiriamali wetu Mhe. Waziri wanahitaji kusaidiwa. Tusi-*assume* kwamba wakeshafundishwa suala zima la kutengeneza itakuwa basi wanahitaji msaada mkubwa. Huu ni wajibu wa Serikali kufanya hivyo.

Kwa hivyo ningekuomba Mhe. Waziri kwamba hili mlifikirie Mhe. Waziri, ninajua mna maabara; maabara yenu inatengeneza mambo mazuri mazuri na hili mlifikirie kutengeneza *centre* of Excellency ambayo itakuwa inakusanya bidhaa za wajasiri amali wadogo wadogo, na hapo mtaweza kujua mahitaji ya mahoteli. Kwa sababu nyinyi Wizara Mheshimiwa, pamoja na serikali yetu ina wataalam wa kutosha wa kwenda kutafuta wakajua *demand* iko vipi, na wanaweza ku-*supply* vipi, lakini masoko yatapatikana vipi.

Mheshimiwa hilo ni muhimu sana ili tupate kuondoa umaskini wa wananchi wetu, lazima tuwasaidie katika shughuli zao za kiuchumi. Bila ya kuwasaidia katika shughuli zao za kiuchumi, tukikaa kwenye madeski tukafikiria miradi mengine tukasahau mengine ya wananchi, Mheshimiwa bado wananchi wetu watalia umasikini.

Kwa hivyo Mheshimiwa nikupongeze sana, najua kazi unafanya vizuri pamoja na watendaji wako na niombe kwamba pale ambapo sisi tunatoa ushauri kama Wawakilishi tunaomba sana kwamba ushauri huo uchukuliwe *seriously*, na ufanyiwe kazi tunajua mengine yanachukuliwa kwa sababu tunakuja hapa tunayaona, lakini Mhe. Waziri tunakuomba sana yachukuliwe *serious* yafanyiwe kazi

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mheshimiwa ninamaliza. Haya yataweza kuleta manufaa katika Taifa letu pamoja na watendaji wako Mhe. Waziri.

Baada ya kusema hayo machache, nilikuwa sina mengi sana lakini yamejitokeza. Kwa hivyo naunga mkono hoja asilimia mia moja, wala sina nia ya kupiga buti.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, japo jina umelikosa kidogo lakini mimi jina langu ni Abdalla Mohammed na babu anaitwa Ali. Mhe. Mwenyekiti, umeniwahi kwa sababu nilikuwa ninaelekea msikitini na kwa sababu ulimtaja Mhe. Marina, maandalizi yangu yatakuwa nimeyaweka pembeni kidogo lakini ya hivyo...

Mhe. Mwenyekiti: Umepewa nafasi ya upendeleo, endelea.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Ninashukuru kwa hilo. Mhe. Mwenyekiti, juzi hapa tulikuwa tunazungumzia suala la TRA walioko bandarini Zanzibar na Mhe. Waziri suala hili akalichukulia ahadi kwamba atalifanyia kazi. Nina imani kwamba atalifanyia kazi.

Ninalotaka kusema Mhe. Mwenyekiti, kwamba suala hili limekuwa si la leo na mara nyingi huwa linatokea kama si bandari ya Zanzibar, basi itakuwa ni bandari ya Dar es Salaam. Ninafikiri Mhe. Waziri analijua. Sasa kwa leo ninajua kwamba wale watu watakuwa hawapo, lakini wao walikuja si kwa kubahatisha. Ninachokijua walikuja hapa kwa kujua kwamba wao ni TRA na TRA ni ya Tanzania wala sio ya Zanzibar pekee. Walikuja hapa wakiwa na mamlaka kamili na wamekuja kufanya kazi na sheria sijui kama zilikuwa zinawazuia, ili wao wasiweze kufanya kazi Zanzibar.

Mimi ninachotaka kusema ni kwamba huu umekuwa ni mtindo. Mhe. Mohammed Haji alisema kwamba *charity begins at home*. Sasa wao wameondoka Zanzibar lakini sisi kwa mizigo yetu huwa tunatumia bandari zote mbili; tunatumia bandari ya Zanzibar na mara nyengine makontena yetu yanashuka katika bandari ya Dar es Salaam. Pia bandari ya Dar es Salaam tunaitumia kwa kupeleka mizigo yetu, tunashushia kule na baadae yanakuja huku. Huu umekuwa ni utaratibu wa kila mwaka takriban ya wananchi wetu kusumbuka hasa wanapoingia katika bandari ya Dar es Salaam.

Sasa Mhe. Waziri anatuhakikishia nini kuhusu suala hili, je, huu mgogoro ushamalizika na wafanyabiashara wetu hawatosumbuka kwa kushusha mizigo yao pale na wakaileta Zanzibar na wale ambao wanaishusha hapa wanaipelekea kule hili tatizo halipo. Imani yangu kwamba ile *charity* kwa vile wameondoshwa Zanzibar na wao wana mamlaka sasa ule uwezo wanaweza wakautumia kule waliko Dar es Salaam, kwa sababu kule ndio *home* kwao, huku haikuwa *home* kwao. Sasa je, tutakapofika kule hawatotumia fursa hii wakaendelea kuwanyanyasa hawa wananchi. Mhe. Mwenyekiti, hilo ni moja.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ni ununuzi wa meli; kama sikosei nakumbuka mwanzo tulikuwa tunaambiwa sijui milioni kumi na saba, milioni kumi na nane, sijui ishirini na tatu. Mwaka huu ametuomba tena bilioni ishirini wakati ameshatumia asilimia 50 kwa alivyotwambia kwamba ameshalipa watengenezaji wa meli hii. Sasa kama ilikuwa ni bilioni kumi na nane, asilimia 50 itakuwa ni milioni 9 tayari zimeshalipwa. Sasa sijui hii meli Mhe. Waziri hasa itagharimu kiasi gani na tumepanga lini tumalize kuwalipa watengenezaji wa meli hii.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kidogo katika Idara ya Mhasibu Mkuu, Idara hii moja katika shughuli zake ni kuratibu wahasibu wa ndani na wahasibu wakuu. Mara nyingi huwa tunapokea ripoti kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu na ripoti hizi huwa zina mapungufu mengi. Mara nyengine unaambiwa kwamba kuna mapungufu katika upatikanaji wa risiti ya matumizi.

Idara hii ndio inayosimamia wahasiku ambao wao ndio wanaorodhesha matumizi na watoaji wa fedha za matumizi hayo. Lakini tushaona kwamba kuna kasoro nyingi zinazojitokeza katika manunuzi hasa katika serikali yetu. Sijui kwa mwaka huu uliopita kuna wafanyakazi wahasibu ambao wameripotiwa kwamba hawa wana mapungufu na wanahitajika wahamishwe au wameripotiwa hawa ni waharibifu wa mali ya umma na labda wamesimamishwa kazi. Mhe. Waziri atakapokuja angetupa maelezo kidogo kuhusu suala hili.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Wizara hii ndio inayosimamia mapato na wao pia wana jukumu la kukusanya mapato na wakajiwekea lengo kwamba sisi mwka huu tutaweka lengo la kukusanya mapato ya kiasi fulani. Lakini la

aibu ni kwamba, hii Wizara ambayo wao ndio wanaosimamia mapato ya nchi hii, wamefikia asilimia 55 tu. Sijui wao watatoa picha gani kwa zile Wizara nyengine ambazo nazo hazikufikia lengo au mapato yao yako chini.

Mhe. Mwenyekiti, ninafikiri mimi nisingelikuwa na mengi sana leo katika mchango wangu isipokuwa ni kusisitiza tu kama wanavyosisitiza wengine kwamba Wizara hii ina jukumu kubwa sana na moja katika majukumu yake ni kusimamia mapato. Ni imani yangu kwamba mapato yapo, lakini usimamizi wake bado haujawa sawa sawa. Moja katika hilo ni kwamba mwaka jana tulielezwa hapa kwamba kutakuja mashine maalum kwa ajili ya kupewa wafanyabiashara, ili mapato hayo yajulikane na watu wapate kupewa risiti. Lakini mara hii ripoti hii haijaonesha chochote je, zile mashine tayari zishaanza kutolewa/kuuzwa au hawa wafanya biashara watapewa moja kwa moja, ili kusaidia upatikanaji wa mapato ukawa ni mkubwa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho, tunatarajia kulifunga Shirika la Magari na programu hii ipo karibu mwaka wa nne na shirika hili ninavyojua hivi sasa linaendelea kulipa wafanyakazi wake mishahara, na linaendelea kufanya kazi kama kawaida. Sasa bado naendelea kujiuliza ile nia ya serikali ya kulifunga Shirika hili ipo na kama ipo imekusudia kutekelezwa lini kwa sababu kama linatia hasara kwa nini liendelee kutia hasara kwa kipindi hiki ambacho linaendelea kuwapo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache ninakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kwa sasa hivi kwa mujibu wa muda hatutokuwa na uwezo tena kumruhusu na kumpa nafasi mtu ya kuendelea kuchangia. Kwa hivyo basi niwaombe wale ambao walikwishakuomba mwanzo, jioni kwa kushirikiana na Mhe. Mwenyekiti Mgeni waje mapema na waanze kuchangia. Wajumbe wenyewe ni Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Marina Joel Thomas, Mhe. Fatma Mbarouk Said, hawa ndio wa kuanzia. Lakini vile vile nichukuwe fursa hii kukushukuruni kwa mashirikiano ambayo mumenipa, lakini zaidi Waheshimiwa Wajumbe tuseme tu kwamba bado kilio kingalipo pale pale; mahudhurio si yenye kuridhisha.

Kesho asubuhi tukijaaliwa tunataka kufanya majumuisho kwa Wizara zote mbili. Asubuhi tutafanya majumusho kwa Wizara ya Majenzi, na jioni tunategemea kufanya majumuisho kwa Wizara ya Fedha. Niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe wale ambao hawako hapa na wana shughuli zao nyengine nje, wajitahidi wawepo ili tumalize kazi hii ambayo tumeletewa hapa kuja kumaliza kwa umoja wetu. Ninawaombeni sana mashirikiano yenu katika hili.

Baada ya hayo naomba kusitisha kikao hiki hadi jioni saa 11.00 barabara. Ahsanteni sana.

(Saa 07.00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11.00 jion)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya upendeleo kwani asubuhi tulipoondoka hapa alikuwa anaanzia nafikiri Mhe. Marina Joel Thomas na wengine, lakini kwa sababu nimepata bahati hii nasema ni bahati yangu kwa hivyo niweze kuitumia vizuri namuomba Mwenyezi Mungu anisaidie kuichangia hotuba hii ya bajeti, ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha.

Kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa kutuwasilishia, pia niwashukuru na watendaji wake kwa hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza ningeanza na kitabu hiki kwa humu kuna ile Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma wametwambia jukumu lake ni kusimamia manunuzi na vile vile kuzi-*dispose* zile mali ambazo za serikali zilizokuwa za muda mrefu.

Kwanza niende na hiki kitabu chenyewe, nikitizama Idara ya Upigaji Chapa uchapaji wake wa hiki kitabu ni mzuri tu, lakini kama kuna *machine* ya *binding* basi kweli *binding* ya vitabu hivi si nzuri. *Machine* hii kama ni mpya na imenunuliwa bila shaka kutakuwa na *guarantee* kwa hivyo kuna lazima kwamba *machine* hii itakuwa hata ile *value for money* itakuwa haipo.

Vile vile sijui *machine* hii kama ni ya zamani basi ile kazi ya kufanya ile *process* yaku-*dispose* basi ilikuwa hii Idara ya Upigaji Chapa waandikie Idara hii ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma, la kama tumegaiwa tu basi vile vile niseme kwamba huyo aliyetugaia kwa kweli ametudharau, kwa sababu vitabu vyote mimi nilifikiria labda kutakuwa na mabadiliko au sijui vitabu vyote vimetengenezwa siku moja. Lakini kwa kweli safari hii maneno ya watu ni majanga makubwa.

Ni majanga vitabu hivi kwamba pale mwanzo zile wizara zilizoanza mwanzo vitabu vilikuwa viko vizuri, lakini mpaka hii leo niseme hii ni wizara sio mama. Hii ni wizara baba kwani baba ndiye mwenye nguvu sana, na mama ana majukumu yake vile vile lakini niseme ni wizara baba.

Kwa upande wangu mimi pia nitasema hii wizara ni wizara yangu ambayo wizara hii mimi kabla ya kuja humu ndani nilikuwa ni wizara ambayo nafanyia kazi, na niseme tu nilikuwa sina *degree* lakini kwa kweli miaka mitano niliyokuwepo hapa sasa Mhe. Waziri anione kwamba sasa hivi nimekuwa nina *degree* ya kazi hii, kwa sababu miaka mitano najifunza humu na nimejifunza mengi.
Kwa hivyo, aone kwamba nikitoka hapa baada ya kukosa ridhaa ya watu wa Amani niseme kwamba sasa nitafanya kazi vizuri kama mtaalamu mwenye *degree*.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye kitabu humu kama alivyotwambia Mhe. Waziri ametuonesha mambo mengi, kwenye ukurasa Nam. 13 Idara ya Fedha za Nje. Mhe. Waziri naomba ufafanuzi hizi fedha za ruzuku milioni 86,797,000 na hii arubaini milioni (40,000,000) pia hizi fedha milioni mia mbili sabiini na tano elfu mia nne kumi na moja (275,411,000) napenda kumuuliza Mhe. Waziri katika fedha hizi ambazo ni ruzuku naomba kujua ni kiasi gani zimemsaidia mwanamke katika kujikwamua kiuchumi. Katika fedha hizi ambazo ni ruzuku na pia ni mikopo.

Vile vile katika kitabu hiki nyuma huku nimeona ufupisho wa maneno, kuna maneno mengi tu ambayo yana ufupisho lakini kuna neno moja hapa sijaliona kwenye ufupisho na ningeomba Mhe. Waziri anipe kirefu chake MPAMITA. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri utakapokuja unipe kirefu chake neno hilo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu hiki unajua kimepanguka panguka samahani sana nitakwenda mbele halafu nitarudi nyuma. Idara ya Bajeti ukurasa Nam. 6, idara hii ina jukumu la kugawa rasilimali fedha, ibara ya 16 mpaka ibara ya 17 kazi ilizotekeleza. Mhe. Waziri kidogo kama nilivyosema kwamba kitabu hiki kidogo kimepanguka panguka hata hizo karatasi zake, kwa hivyo kidogo kinatupa mashaka itabidi Mwenyekiti unistahamilie na sijui kama hizo karatasi hazijapotea, kwa sababu sizioni kabisa, sijui kama zimechomoka lakini naona kwa kweli ukurasa huu Nam.16 zimechomoka naona sizioni kabisa, lakini kuna hii Idara hii ya Bajeti na kuna mambo ambayo nayaona idara ilikuwa na jukumu hilo. Lakini hata hivyo, ilikuwa nimeweka *point* na moja kwa moja nilikuwa niende na kitabu…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Fatma endelea na *point* nyengine uliyonayo.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Kwa sababu kulikuwa kuna mambo humu nimeya-*note* kuna kifungu hiki cha 8 kufanya tathmini na hatimae kushauri serikali kuyafunga, itakuwa kwenye Idara ya Uhakiki Mali wa Umma. Kufanya tathmini na hatimae kushauri serikali kufunga Shirika la Magari, Shirika la Utalii, serikali imeridhia kufungwa mashirika hayo na tayari Mhe. Rais ametoa amri rasmi ya kuyafunga mashirika hayo kama sheria inavyoeleza.

Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, mimi kama Mwakilishi wa Jimbo la Amani hili Shirika la Utalii moja kwa moja limeshafungwa lakini kwa kweli Shirika la Magari bado kama mwakilishi wa wananchi nasema bado Shirika la Magari linaweza kwenda wenyewe kujitegemea, kwa sababu juzi tulikwenda mwezi uliopita tumekwenda kama kamati na tumeona ni hali gani linajiendesha wenyewe kwa faida.

Kwa sababu mashirika haya mara nyingi huwa yanafanyiwa tathmini na kufungwa kwa sababu ya uwezo wake wa kujiendesha. Kwa hivyo, mimi niseme kwamba kwa shirika hili siungi mkono kufungwa kwa sababu nimeona namna gani, kwa sababu kulifunga shirika hili kwanza ni kuwakosesha ajira wananchi.

Ni kweli sasa hivi kuna biashara nyingi za magari lakini bado ni jukumu la serikali kuyasimamia haya mashirika ya serikali. Kwa sababu serikali kuwa haina mashirika ambayo yakujiongezea ingawaje haya kubinafsisha kwa wananchi kwamba kuna watu wanaagizishia magari, kuna *showrooms* nyingi za magari, lakini bado na serikali ina

nafasi yake ya kuagizishia magari na vitu mbali mbali. Si magari tu hata vyarahani kwa wafanyakazi waliokuwa kipato cha chini kwa kweli walikuwa wanatumia fursa hii kukopa vyombo mbali mbali.

Kwa hivyo, kulifunga shirika hili si vizuri kwani nina hakika kwamba linaweza kujiendesha kibiashara, nimeshakwenda kama Kamati yangu ya *PAC*. Kwa hivyo, ninaomba bado itathmini tena kwa Shirika hili la Magari bado lina uwezo mkubwa wa kujiendesha kibiashara.

Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi tatizo la mashirika haya ni kwamba serikali au taasisi za serikali inazikopa sana na kuzifanya kwamba haziwezi kujiendesha, ni sawa sawa na paka dume kula watoto yake. Kwa kweli hii haipendezi kwa sababu ukitizama tumeona kweli mashirika tathmini yake kubwa ni zile dhima zake za mpito na mali zake za mpito, kwa kweli zikiwa na uwiano itategemeana vipi mali zake za mpito na dhima zake za mpito zinakuwa. Kwa hivyo, mimi nasema kwa suala hili la kulifunga Shirika la Magari bado tathmini tena kwa sababu tunaweza tukakosesha ajira vijana wetu.

Mhe. Mwenyekiti, Mfuko wa Barabara nimeomba sana kwamba ijitahidi kwa kuzifanyia matengenezo ya haraka barabara pale zinapojitokeza athari za awali ili siziweze kuathirika, kwani athari ndogo inaweza ikasababisha ajali na pia kuweza kugharimu fedha nyingi zaidi pale tunapotaka kuzisawazisha athari zile. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ningeomba kama jana nilivyochangia vile vile kwamba siku zote tujitahidi kwani kuna msemo wa Waswahili unasema “usipoziba ufa utajenga ukuta”.

Kwa hivyo, ningependa sana hata vile vifungu ambavyo tunapiga kelele niliwaomba wajumbe wenzangu hapa kwamba kuna vifungu tunaona sasa hivi haviingizi pesa kwa zile kelele zetu humu ndani. Lakini kwa kweli italeta athari mbele kwa sababu kama kuna matengenezo madogo madogo ya majengo, sasa hata kama ushajenga nyumba kama hivi lakini kunaweza kukatokea athari ndogo ndogo na ukaziwahi mapema. Lakini sasa kama vifungu vile havina fedha ni tatizo. Kwa hivyo, ningeomba Mfuko wa Barabara hizi barabara zizitizame mapema.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda mbele nakuta kuna ukurasa Nam. 25 kuna programu ya ujenzi wa ofisi za serikali. Mhe. Mwenyekiti, niipongeze sana serikali na nasema naamini sasa tutakwenda na wakati naomba programu iwe endelevu…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Fatma umebakiza dakika tatu.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ofisi zetu nyingi haziendani na wakati, niwapongeze sana pia wale waliojenga ofisi kwa kutumia bajeti zao kama *CAG*, kwa kweli anastahili pongezi. Lakini nataka nimuulize Mhe. Waziri ni kiasi gani majengo haya ya ofisi yamezingatia hali ya watu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mradi huu wa ukurasa Nam. 25 juu ya uimarishaji huduma za miji, kuna kifungu cha 3 kidogo kinasema kufanya malipo ya ada ya shilingi 3,216.02 milioni kwa ushauri elekezi kwa wakandarasi kwa kazi mbali mbali.

Kwanza naomba Mhe. Waziri serikali iwe makini na hawa wakandarasi, naomba tutazame sifa zao zaidi wana uwezo kiasi gani kwa kuepusha matatizo mbali mbali baada ya kazi zao kushindwa kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, pia namuomba Mhe. Waziri anifafanulie zaidi kuhusu malipo haya haitoshi kusema kiasi hiki ni kwa ajili yakulipia mshauri elekezi na wakandarasi mbali mbali. Naomba atufafanulie hasa, unajua mimi nilimwambia Mhe. Waziri sasa hivi nimeshakuwa nina *diploma* miaka mitano yakukaa humu kwa kweli nimejifunza mengi na kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi chote cha miaka mitano ameniteua kwenye Kamati ile ile ya *PAC*. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri anichanganulie hizi fedha.

Mhe. Mwenyekiti, humu ndani mna wanasheria waliobobea na mimi nimeshabobea kwa fani hii. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kwenye mradi ukurasa wa 30…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Haya naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Fatma Mbarouk Said na nikuombe radhi kwamba nilikutaja wewe mtu wa kwanza, lakini kutokana na ratiba niliyonayo mbele yangu inajitokeza kwamba wewe ni wa kwanza ndio maana nikakutaja kuwa wa kwanza.

Waheshimiwa Wajumbe leo katika jukwaa letu la wageni tumepata wageni kutoka Kigoma Ujiji ambao ni Waheshimiwa Madiwani na watendaji wakuu kutoka Manispaa ya Kigoma Ujiji. Jumla yao ni 28 wanaongozwa na Meya wa Kigoma Ujiji Ndugu Bakari Hussein Beji pamoja na Naibu Meya Ndugu Rohanja Yunushash ambao ni wageni wa Baraza la Manispaa Zanzibar. Karibuni sana wageni wetu.

Waheshimiwa Wajumbe tunaendelea anayefuata sasa ni Mhe. Marina Joel Thomas na baada ya hapo atakuja Mhe. Jaku Hashim Ayoub na ajitayarishe Mhe. Panya Ali Abdalla.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Fedha. Pia napenda kumpongeza Mhe. Waziri kwa kusoma hotuba hii nzuri na yenye mchanganuo mzuri kabisa. Na pia napenda kuwapongeza Katibu Mkuu wa wizara hii, Wakurugenzi, Makamishna na watendaji wote kwa utendaji wao mzuri katika kutekeleza majukumu yao kwa ukamilifu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitazungumza katika maeneo matatu au manne, kwanza nitaanza na Chuo cha Uongozi cha Fedha ambacho katika kitabu cha hotuba ya bajeti ya Mhe. Waziri iko katika ukurasa wa 43.

Mhe. Mwenyekiti, katika Ripoti ya Kamati ambayo inaisimamia hii Wizara ya Fedha nimeisikiliza kwa makini lakini nikasikia kusema kwamba Chuo hiki cha Fedha cha Chwaka kinahamishiwa katika usimamizi wa Chuo Kikuu cha Taifa *SUZA*. Kwa kweli nilishangaa kwa hivyo naomba nipate maelezo kutoka kwa Mhe. Waziri. Je, chuo hiki kwa sababu ni chuo ambacho kinasimamiwa na Wizara ya Fedha, wizara imeshindwa kukisimamia? Au sababu gani ambazo zinafanya kichanganywe na Chuo Kikuu *SUZA.*

Nasema hivyo kwa sababu chuo hiki kwanza kimeshajijengea sifa ndani na nje ya nchi, isitoshe kinafanya kazi zake vizuri na ukikichanganya na Chuo cha Taifa cha *SUZA* kwanza wana fani tofauti, pia tunaweza tukaangusha soko la ushindani la vyuo. Vile vile kimeshafanya maghafali karibu kumi katika ripoti hii ya Mhe. Waziri imesema. Kwa hivyo, ni chuo ambacho sasa hivi kimeimarika kiasi fulani, sasa nashangaa kwa nini kichanganywe na Chuo Kikuu cha *SUZA*. Mhe. Waziri naomba anipatie maelezo, ili nijue sababu gani ambazo zinapelekea chuo hiki kichanganywe na chuo cha *SUZA*, tunaweza tukakiuwa kabisa pengine hata sifa yake isije tena.

Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda katika suala la mishahara. Suala hili lilizungumzwa na baadhi ya Waheshimiwa wengi siku za nyuma kuhusu Wahasibu wa mawizara ambao wana *degree* ya kwanza, ya pili na mishahara yao iko juu. Kuna wahasibu wengine wana *degree* hivyo hivyo ya kwanza na ya pili, *degree* ya kwanza wanapokea kwenye shilingi laki nne na *degree* ya pili wanachukua shilingi laki sita, lakini ukiangalia wahasibu wa wizara wanachukua mishahara zaidi ya hicho kiwango ambacho nimekitaja wakati elimu ni moja, majukumu yanafanana, kazi ni zile zile na ukiangalia hata katika vyuo pengine kuna wahasibu wa vyuo vyetu, ukiangalia pengine majukumu hayana tofauti sana na isitoshe katika vyuo hivi pengine mtu anafanya kazi zaidi ya saa 11. Sasa nilikuwa naomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi kuhusu hili, kwa sababu naona majukumu yanafanana, elimu inafanana, kwa nini wale wawe juu zaidi na hawa wawe tofauti.

Jengine nitazungumzia kuhusu Mfuko wa Barabara. Mfuko wa Barabara kwanza naupongeza unafanya kazi nzuri, lakini pia katika Mfuko huu nilikuwa naomba wizara iangalie katika fungu la matengenezo ya vifaa. Kwa sababu Idara ya Utunzaji Barabara vifaa vyake vya ujenzi ni vichakavu sana na vyengine haviko katika hali nzuri. Kwa hiyo, kupitia Mfuko wa Barabara ambao ungetengewa fungu, fungu najua lipo lakini pengine halitoshi kwa sababu vifaa vya ujenzi kwa kweli vina gharama kubwa sana. Hilo unalitambua Mhe. Waziri lakini sasa ukiangalia katika idara hii inashindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo kutokana na uchakavu wa vifaa ambavyo wanategemea kufanyia kazi. Nataka nimuombe Mhe. Waziri Mfuko wa Barabara uongezewe fedha ili vinunuliwe vifaa vya ujenzi wa barabara na idara hii iweze kufanya kazi zake kwa uhakika zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea niende Shirika la Bima. Shirika hili kwanza nalipongeza kwa kuongeza matawi yake matatu ambapo kwenye ripoti wamesema Tawi la Mtwara, Mwanza na Dar es Salaam. Hii ni hatua nzuri naipongeza sana kwa hilo. Lakini kwenye mafanikio pia kuna changamoto. Changamoto iliyopo kwenye shirika kuna suala zima la hawa mawakala, ucheleweshaji wa malipo kwa hawa mawakala. Mawakala wanakusanya mapato na wanarejesha

katika mashirika lakini wao malipo yao wanakawia kulipwa. Hili namuomba Mhe. Waziri hao mawakala wakirejesha marejesho yao basi na yale malipo yao walipwe kwa wakati wasicheleweshwe. Malalamiko hayo yapo Mhe. Waziri.

Pia kuna tatizo la usafiri kwa mawakala na mabango ya matangazo. Ili wakala ajulikane ina maana awe na bao la matangazo kumuonesha kama huyu ni wakala. Kwa hiyo, suala la mabango pia nalo liangaliwe kwa mawakala wetu.

Halafu nilisema niende kwenye suala la Mashirika. Mashirika Mhe. Mwenyekiti, kiuzoefu mashirika yetu mengi yamekufa na mengine yanajikokota kidogo kidogo, labda nimuulize Mhe. Waziri katika hayo mashirika yetu ambayo utekelezaji wake unasuasua au mengine yaliyokufa kabisa wizara si imefanya tathmini kuona ni sababu gani ambayo inasababisha mpaka haya mashirika yetu yanakufa kabisa, imefanya utafiti ikajua sababu gani. Naomba nipate maelezo kwa sababu ingefanya utafiti ingechukua zile changamoto ikazifanyia kazi baadae hata hayo mashirika ambayo yamo katika utendaji wakazidi kuboreka kutokana na zile changamoto ambazo zimejitokeza kwa mashirika mengine. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hapa akija anipatie maelezo Mhe. Waziri.

Sasa niende katika ukurasa wa 38 kuhusu *TRA*. *TRA* ina jukumu la kukusanya mapato yatokanayo na vianzio mbali mbali vikiwemo vya Muungano, Ushuru wa Forodha, Ushuru wa Bidhaa na Kodi za Mapato ya Ndani. Hili ni jukumu kubwa, hapa niombe wizara isimamie vizuri makusanyo haya. Kwa sababu naamini tuna vyanzo vingi vya mapato lakini usimamizi sasa, usimamizi ukiwa mzuri na mapato yatapatikana mengi na serikali itaweza kufanya kazi zake kwa umakini zaidi.

Pia niende katika Idara ya Bajeti. Idara ya Bajeti ina kazi kubwa kweli kweli, idara hii ina kazi ya kuandaa muongozo wa bajeti na kuusambaza katika mawizara mbali mbali, ina kazi ya kuchapisha makadirio na mapato ya matumizi ya serikali kwa mwaka. Hii ni kazi nzito na ukiangalia kila tukifanya bajeti kuna vitabu vingi tu, vinakuwa *Volume I, Volume II* ni vitabu vikubwa, kwa kweli wanafanya kazi nzito kabisa. Kwa hiyo, naomba niwapongeze kwa moyo wa dhati kabisa ni idara inayofanya kazi kwa uadilifu.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia wakati mwengine tunakaa katika zile kamati utakuta wale watu wa Wizara ya Fedha tunakaa nao mpaka usiku, kwa kweli wanajitahidi nawapongeza sana kwa moyo wa dhati. Ila Mhe. Waziri awaangalie na wao kwa sababu wanajituma na kujitolea kiuzalendo, basi awaangalie na wao muda wao wanaoutumia kama kuna fursa yoyote ya kuweza kuwaongezea chochote awaongeze au awafikirie watu hao, kwa kweli wanafanya kazi nzito kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia ni kuhusu suala zima la uingizwaji wa fedha katika mawizara. Uingizwaji wa fedha katika wizara unachelewa na inapelekea hata yale malengo ya kila wizara kushindwa kutekelezwa kwa wakati. Hapa pia nilikuwa namuomba Mhe. Waziri afanye kila jitihada zile pesa ziingie kwa wakati ili wizara ikijipangia kipindi hiki tutekeleze moja, mbili, tatu au miezi mitatu hii tunatekeleza hiki waweze kutekeleza. Naomba pesa zile wapate kwa wakati ili na wao zile kazi wazifanye kwa wakati ambao wamejipangia.

Pia nimuombe Mhe. Waziri kuna suala zima la Mradi wa Kengeja. Mwaka jana mradi huu ulitengewa fedha kwa nyumba ile ya Kengeja, lakini mwaka huu labda sikuona vizuri naona kama hawajatengewa fedha yoyote. Kama nimekosea naomba nisawazishwe. Je, ni kwa sababu gani wakati mwaka jana walitengewa lakini mwaka huu hawajatengewa. Pia mradi wa ***TAZA*** Pemba naomba maelezo kuhusu miradi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hotuba hii.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ama baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Allah (*S.W*) aliyeniwezesha kusimama hapa ikiwa huu sio uwezo wangu wala akili yangu, wala maarifa yangu ni pumzi alizoniazima ambazo sijui wakati gani atazihitaji mwenyewe Mwenyezi Mungu, nimshukuru kwa hilo.

Vile vile nataka nimpe pole rafiki yangu baada ya safari ndefu aliyokwenda na kurudi, Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, Mhe. Rashid Seif Suleiman kutokea China na machofu ya safari aliyokuwanayo nimwambie karibu katika uwanja wetu huu tena. Pole na machofu baada ya kushuka kwenye pipa moja kubwa *Boeing 737* na leo tunae hapa.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa sijafanya haki kama sijakushukuru wewe kunipa nafasi hii kuweza kuchangia. Nimshukuru Waziri wa Fedha kwa umakini wake, ufuatiliaji wake na kauli zake kwa vitendo anavyofanya humu ndani na mimi baadhi nimevishuhudia. Sasa nimpe haki yake hii kwa umakini wake.

Vile vile nimshukuru Katibu Mkuu wake Sheikh Khamis Mussa kwa uchapaji kazi wake makini uliokuwa haujali mvua wala jua. Nitakuwa sijamfanyia haki vile vile Mhasibu Mkuu, mchezaji mstaafu wa *Small Simba*, Omar Kingi kwa jitihada anazozichukua.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nitachangia tatizo la muda mrefu la wizara mbali mbali kuidhinishwa fedha na Baraza hili la Wawakilishi lakini baadae mtihani mtupu. Tumekuwa tukipiga kelele humu tukiidhinisha pesa kwa mawizara lakini mawizara bado tunaendelea kuwalaumu na tutaendelea kulaumu wakati bado Wizara ya Fedha, sijui fedha zenyewe hazipo hazipatikani hasa ukiangalia katika sekta ambazo ni muhimu kila mwananchi zimemgusa. Kuna Sekta ya Afya, kila kiumbe hai anaihitaji, kwenye elimu pesa hizi hazifiki kwa wakati.

Mimi nilikuwa ni Mjumbe wa Kamati ya Wizara ya Afya kabla ya kuingia mwenyekiti na nilipiga kelele sana, lakini ndugu yangu waziri msikivu na kasikia na bajeti kaiongeza kwa wizara hii. Lakini bado Mhe. Waziri utapokuja hapa hebu tueleze nini tatizo la mawizara haya kukosa fedha wakati sisi tunaidhinisha? Hazipo, majukumu mengi, kama majukumu mengi tungemuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais akamshauri Mhe. Rais akatafute naibu waziri wizara yako hii.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, nichangie katika eneo la kulipa kodi. Serikali yoyote ile lazima ichangie kodi ili iweze kuleta maendeleo na kujenga uchumi imara. Kwa mfano, ukusanyaji katika mahoteli hauridhishi, hii *formula* Mhe. Waziri ishapitwa na wakati kwenda usiku ukagonga mlango ukatafuta vyumba vitupu, wageni wangapi, hii sasa ishafika wakati *airport* na bandarini kuweka *data base.* Sasa hivi mambo ya kwenda kupapasa tu usiku ukafungua mna wageni wangapi, vyumba vimefungwa, hamna hii hairidhishi *formula* hii ishapitwa na wakati.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nichangie wafanyabiashara wadogo wadogo. Mhe. Waziri wafanyabiashara wadogo wadogo mtu ana mtaji wa shilingi milioni kumi analipishwa kodi tatu au nne; Halmashauri wanataka pesa, Baraza la Mji wanataka pesa, *ZRB* wanataka pesa. Hawa wanatakiwa wawe wakubwa watakuwaje wakubwa kwa kodi kama hizi, hawawezi kwenda kodi zimekuwa nyingi kuwe na *formula* angalau kwenye mtaji wa shilingi milioni 50 hebu angalieni hawa wanataka wawe wakubwa nao.

Leo utakuta wafanyabiashara wakubwa wanapewa msamaha wa kodi badala ya kuangalia wale wadogo hatuwezi kwenda, angalau tuwe na *formula* ya shilingi milioni hamsini ukawaachia hawa watu. Lakini huyu *ZRB* anamsubiri, Halmashauri anamsubiri, Manispaa anamsubiri, haji juu atamalizika tu.

Nikitoka hapo nije kuhusu misamaha ya kodi. Misamaha ya kodi hii nafikiri iangaliwe kwa umakini kabisa inapotolewa inafika kwa walengwa? Au imekuwa mbuzi tunampigia gitaa, tuna Mwezi Mtukufu wa Ramadhani huu kesho kutwa penye majaaliwa tuangalie misamaha inayotolewa ya tende imeshuka bei, mchele umeshuka bei, unga wa ngano umeshuka bei, sukari hamkutoa, tuseme inamuweka katika hali ya utajiri mtu fulani tu, yule wa chini mnyonge anazidi kuumia na kipato hiki. Mimi sijaona tofauti yake mpaka hii leo ipo haja sheria kuangalia *formula* hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nije katika eneo nyeti la *PBZ.* Kwanza niwashukuru wafanyakazi wote wa *PBZ* wakiwa chini ya uongozi wa *director* Juma Amour kwa kazi nzito wanayoifanya. Benki ile chini ya wasaidizi wake Mhe. Ame Mtumbatu huyu, Mhe. Mohamed Halfan na akinamama watatu akiwemo Mama Hamisa, Fatma Adinani na Mama Viwe na Said Mohamed Said. Hawa vijana Mhe. Waziri kama kitu cha kufikiriwa *PBZ* imetoka katika mdomo wa chewa, ilikuwa imeshafunga virago hakuna tena jina la *PBZ* hapa Zanzibar kwisha mchezo.

Mimi shahidi na nimeyaona, hawa watu wamefanya kazi katika mazingira magumu, leo viongozi humu ndani wawakilishi tunakuja kupiga kelele kuongezewa mishahara wale hatuwafanyii haki, kuongezewa mishahara wafanyakazi mtu unamchukua darasa la tatu na *Form II* tafauti ionekane, hata vidole haviko sawa hivi. Hawa watu wamefanya kazi katika mazingira magumu.*(Makofi)*

Vile vile nitakuwa sijamfanyia haki Rais Mstaafu Dr. Amani Abeid Karume, yeye baada ya Mwenyezi Mungu ambaye ndiye wa kwanza basi na yeye ndiye aliyesababisha benki ile kubaki baada ya kufahamishwa kuna hili na

hili, tulikuwa hatuna benki. Mhe. Waziri isifike wakati mtu kuja kusema mshahara wa huyu, huyu na huyu, hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu, benki serikali hamkuingiza pesa mumeingiza shilingi 16 milioni tu tangu mwaka 1966, tusione vinaelea vimeundwa.

Tuangalie mfano suala la Kariakoo lile, kulikuwa kuna kijana kapewa mwaka mmoja na nusu kazalisha shilingi 15 milioni, lakini hapa baada ya kupewa kijana mmoja mwaka ule mmoja na nusu keshasaini shilingi 30 bilioni suala la Kariakoo. Sasa tunataka nini, hebu tuangalie *FBME* bwana Dachi anavyofanya kazi, penye mfanyakazi mzuri anakwenda anamchukua anamvuta. *PBZ* mimi nakunasihini fanyeni kazi na sisi tunaiona nikiwa shahidi. Tawi lilikuwa moja tu, wameshakuja wazungu wameshafanya hesabu benki iondoke, lakini na Serikali hili gawio lenu hebu liachieni humu ndani benki ipate kukua hii, pana mabenki mengi yamekuja sasa hivi yanapiga vita hapa, tukifanya masihara tutajimaliza wenyewe. Hili gawio liachieni ndani, sio kama wanataka *interest* hawa, liachieni mtaji ukue muwape *support* hawa watu.

Mhe. Mwenyekiti, tumeona matawi sasa hivi Dar es Salaam yapo, Pemba wameongeza, hapa Mpirani juzi matunda yake tumeyaona. Leo mnakuja kuchukua gawio lazima tuwape *support* watu. Taa huwashi nje unawasha ndani ya nyumba, *sadaka inaanza nyumbani*.

Huu mtaji wenu nyinyi Wizara ya Fedha mngeuacha kwanza mtaji ukapata kukua. Kuna mabenki mangapi wanapiga vita hii benki, hii benki inafanya kazi katika mazingira mazito. Juma Amour leo Mwenyezi Mungu amemjaalia afya njema maradhi ameyapata benki. Ndio ukweli Mhe. Mohamed Aboud Mohamed ulivyo, hili halitaki tochi, yule jamaa alikuwa mzima na afya yake maradhi ameyapata benki baada ya kuiinua, benki ilikuwa imeshauzwa hii ikishakwenda zake basi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nizungumzie katika eneo la Bandari. Mhe. Mwenyekiti, eneo hili bado wafanyabiashara na biashara itazidi kuendelea kufa kwa kutokuwa na umakini na ufuatiliaji. Leo tokea kuanza Shirika la Bandari hatujaweka kitu chochote kipya, makontena hayatoki, *cranes* hazifanyi kazi, sijui nini kinachofanyika, leo tunamtafuta mchawi. Kama hamuwezi tafuteni mwekezaji asilimia wagawane, Shirika la Bandari linaoza kule. Makontena hayapatikani wakati meli zinapita zikafika Chumbe, kufika Zanzibar foleni wanarudi. Kama Wizara imekuwa mzigo, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ndio imekuwa mzigo. Imefika wakati leo hakuna kinachoendelea kule bandarini mpaka leo. *PBZ* wapo tayari kuwakopesha hawa nendeni kakopeni, msiwasumbue watu, watu wanakwenda na wakati wa leo. Iwe mtu ana biashara yake anataka kuchukua mzigo wake kwa wakati hawezi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ninamuomba Mhe. Waziri wasaidie Bandari ya Dar es Salaam inafanya kazi masaa 24, huku hakuna kinachofanyika, ikifika saa 12:00 jioni watu wameshafunga virago wanaondoka. Bandari yetu ndogo tutafanya vipi kazi namna hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, nije suala jengine Wizara ya Fedha wamekuwa wakisimamia Mfuko wa Barabara. Leo ni aibu Bandari ya Malindi kwenda kutupwa makalbi katikati ya barabara. Nimepiga kelele nitaendelea kupiga mpaka leo. Wazungu wanakuja na uchafu uliowekwa pale ni aibu kwetu ule. Barabara wameitwisha mzigo ambao si wake.

Mhe. Mwenyekiti, tunalipigia kelele siku zote suala hili, barabara mizigo mizito isipite, leo pamewekwa makalbi barabara inaumia haijui kusema. Tatizo nini na taa hamna pale mtu akija akijikwaa, Mwenyezi Mungu atuepushie mbali. Mimi nitaendelea kupiga kelele kama utaacha sawa, tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije barabara yangu ya Jambiani. Nilikuwa nikiipigia kelele siku zote tokea naingia ndani humu, na nitaendelea kuipigia kelele mpaka utakapofika wakati wa kuondoka humu ndani. Kule kuna wawekezaji wa mahoteli mengi, kuna wawekezaji wathamini wale. Kuna mahoteli zaidi ya kumi kodi ngapi zinalipwa barabara ile, Serikali ikashindwe, haielekei.

Mhe. Mwenyekiti, ulipokuwa ukichangia nilikuwa nakusikiliza ukilia na suala la *ZIPA* kuwa wanachelewesha miradi, lakini katika watu wanaofanya kazi *ZIPA* ni haki yao kusifiwa. Sio wale wenye maamuzi, mimi nilikuwa na mradi wangu nikauona matokeo yake. Sio wale *ZIPA*, yule Bwana Salum na Bwana Sharif wanafanya kazi ki- *lillah*, urasimu upo katika wizara nyengine ikiwemo Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati; utalia, utakiona cha mtema kuni! Bwana Salum na Bwana Sharif wanafanya kazi wale sana. Mimi nilikuwa na mradi nikiufuatilia pale basi niliona matatizo niliyoyakuta.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nije *ZSSF*. Mhe. Mwenyekiti, imefika wakati sasa hivi *ZSSF* iwakopeshe wateja wake, tuangalie kama kule Bara watoe fedha za magari, nyumba na kadhalika. Wateja wao si wanaangalia mtaji wao uko vipi, Bara wenzetu wanafanya vitu kama hivyo, naomba liangaliwe hili.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo, nafikiri tusubiri jawabu za Mhe. Waziri zitakapokuja ili tumuidhinishie. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote sina budi na mimi nichukue fursa hii nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema tukaweza kukutana hapa jioni hii. Pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe Mwenyekiti kwa kunipa na mimi nafasi niweze kusema machache juu ya hotuba hii ya Waziri wa Fedha.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nianze kwa kumpongeza Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wao wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya. Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze mchango wangu katika ukurasa wa 35 ambapo kunaonekana kuna Bodi ya Ukusanyaji wa Mapato.

Mhe. Mwenyekiti, mimi bado niiombe Serikali kwamba lazima iweke mkakati maalumu wa kuongeza mapato, kwani inaonekana tunatumia sana lakini tunaingiza kidogo. Hivyo Mhe. Mwenyekiti, hii inakuwa ni kazi ngumu sana, kwa sababu unataka kutumia lakini mapato yanakuwa kidogo. Kwa hivyo, ni lazima Serikali ile mipango yake mizuri ambayo inaonekana imeipanga ya kuongeza vyanzo vya mapato, basi lazima ihakikishe vyanzo hivi Serikali inaongeza juhudi ya kuona tunafanikiwa katika kuongeza mapato hayo.

Mhe. Mwenyekiti, vyanzo vingi vimetajwa ikiwemo Ujenzi wa Bandari, Uvuvi wa Bahari Kuu, kuimarisha utalii wenye uhakika na viwanda vidogo vidogo ambavyo vitaweza kuisaidia Serikali kuongeza mapato lakini pia wananchi wetu kuweza kupata ajira. Mhe. Mwenyekiti, mimi niombe azma hiyo ya Serikali basi ijitahidi ili tuweze kufanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na ukusanyaji huu wa mapato lakini bado niiombe Serikali izibe mianya ya uvujaji wa mapato ya Serikali. Mhe. Mwenyekiti, jambo hili bado lipo, mapato ya Serikali yanavuja sana. Kwa hali hii kama Serikali haikujikita katika kudhibiti uvujaji huu wa mapato basi hatuwezi kupiga hatua kubwa ya maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, pia nizungumzie kuhusu ukaguzi wa mahesabu yetu katika mawizara. Mhe. Mwenyekiti, ukaguzi haufanywi kwa wakati muafaka ambao unatakiwa *CAG* aweze kufanya ukaguzi huo.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuchelewa katika kufanya ukaguzi kunamsababishia *CAG* na yeye kuwa na kazi nzito ambayo mrundikano wa kazi utaonekana kwake kuna msongamano mkubwa wa mawizara ambao unataka kufanyiwa mahesabu. Na kazi ya kupiga mahesabu ni kazi kubwa ambayo inataka utulivu, inataka muda wa kutosha ili aweze kufanya naye kazi yake kwa uhakika. Vyenginevyo tunaweza tukamuona kama hawajibiki vizuri, kwa sababu inabidi aripue tu hiyo si vizuri. Kwa hivyo, muda ambao tunapangiwa wa mawizara kuweza kukaguliwa basi ni lazima tujiweke tayari katika muda huo.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Mfuko wa Barabara. Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wamesema hapa kuhusu mfuko huu. Kwa kweli mfuko huu pamoja na uchakavu wa vyombo lakini nilitaka kujua katika mwaka wa fedha uliopita uliweza kutengeneza barabara ngapi za mijini na vijijini; ambazo zinaonekana zinahitaji matengenezo madogo madogo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia tunapoendelea kuchelewa kuzifanyia matengenezo madogo madogo hizi barabara zetu, hiyo huwa inasababisha kufikia barabara hizo kukosa kupitika kabisa.
Mhe. Mwenyekiti, yapo matengenezo makubwa ambayo yatahitaji fedha nyingi, lakini yapo matengenezo madogo madogo ambayo yanaweza kuhitaji fedha kidogo ambazo tunaweza kuzimiliki. Hili tuliangalie yale madogo madogo yanayoweza kufanyika basi tutatue tusichanganye makubwa na madogo yakakutana kwa wakati mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe walipiga kelele sana hapa wakati wa kupitisha bajeti ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, kwa sababu kama kazi za kuweka *zebra* ambapo sehemu zile zenye mikusanyiko ya watu wengi *zebra* imefutika, masuala kama haya tunaweza kuyafanya, hayo tuyafanye. Pia kuweka alama zile katika matuta ambapo

matuta unapita hayaonekani mtu anavamia tu, kwa hivyo mambo madogo madogo kama haya tunaweza kuyafanya. Sasa Serikali ichukue hatua ya kuyafanya haya madogo madogo ili yasije yakaungana na yale makubwa ikawa mzigo mkubwa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee na mchango wangu katika ukurasa wa 41 ambapo kuna Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi *(ZIPA).* Mhe. Mwenyekiti, mamlaka hii ina jukumu kubwa la kushajihisha wawekezaji ndani na nje, lakini naomba mamlaka hii kuwa makini na wawekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa tukishuhudia wawekezaji wengine wakiitia hasara Serikali kwa kuacha madeni makubwa katika Serikali na kwa wananchi ambao wanahangaika kujitafutia riziki, lakini wawekezaji wamekuwa wakiwadhulumu fedha zao baada ya kupeleka miradi mbali mbali katika maeneo yao.

Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa na wafanyabiashara wengi ambao wamekosa fedha zao. Mimi nitoe mfano hapa kuna haya mahoteli *My Blue, Venta Club, Go Inn* na nyingi nyenginezo. Mhe. Mwenyekiti, wafanyabiashara hawa wamedhulumiwa, yaani wamepeleka bidhaa zao nyingi na mtaji wa kinyonge unaeleweka. Leo wamekosa kulipwa fedha zao na wawekezaji hao wametoweka. Mhe. Mwenyekiti, Serikali imechukua juhudi gani ya kuona wafanyabiashara wetu hawa wanaweza kupatiwa fedha zao ili wakajikwamua wakaendelea na miradi yao.

Mhe. Mwenyekiti, pia Serikali katika bajeti iliyopita ilitueleza kuhusu kuboresha mapato. Wakasema wana mpango wa kufungua benki *Airport* ili fedha za *visa* ziweze kuingia moja kwa moja. Je, azma hiyo ya Serikali imefikia wapi.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa mimi mchango wangu utakuwa mfupi niiombe tu Serikali kupunguza matumizi yasiyokuwa ya lazima ili tuweze kuwahudumia wananchi wetu katika kuwatatulia changamoto zinazowakabili wananchi na mengi mengineyo yenye kuleta faraja kwa wananchi wetu. Kwa mfano, kuweza kupata elimu bora, afya bora, miundombinu na mengineyo. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mahitaji yaliyokuwa hayana ulazima sana tuyapunguze ili fedha hizo basi ziweze kurudi kwa wananchi wetu na kuweza kutatua zile changamoto zinazowakabili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu ulikuwa ni mdogo lakini nasema naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia bajeti hii iliyowasilishwa na Mhe. Waziri wa Fedha, Mheshimiwa swahibu wangu Omar Yussuf Mzee.

Mhe. Mwenyekiti, Mheshimiwa huyu mimi ni rafiki yangu sana, na urafiki wangu haukuanza hapa Barazani, umeanza zamani kabla sijaitwa Mwakilishi, lakini sasa hapa tupo kazini, kwa hivyo ajue kwamba pamoja na urafiki wetu lakini kwenye kazi, kazi kwanza urafiki baadae.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nimwambie swahibu wangu Mhe. Waziri wa Fedha kwamba hii bajeti nitazuia fungu la *ZIPA*. Nataka maelezo ya kutosha ili nijue ni kwa nini wawekezaji hasa wazalendo na hata wageni wanakuwa wanasumbuliwa kupata vibali katika uwekezaji wao. Zaidi ukiangalia ile miradi yenyewe ambayo inawekewa vikwazo ni miradi ambayo tunategemea itatoa ajira kubwa sana kwa upande wa Zanzibar. Sasa hili nitalieleza baadae lakini nilikuwa natoa kama utangulizi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini swahibu wangu mwengine Mhe. Panya Ali Abdalla ametoka hapa, sasa yeye alimwambia Mhe. Waziri wa Fedha ajitahidi kusimamia kuziba mianya ya upotevu wa fedha. Sasa mimi nataka niwaambie Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi. Mhe. Waziri wa Fedha tumempa kazi ya kukusanya fedha na kutumia fedha, kuziba mianya ya fedha ni kazi yetu Baraza la Wawakilishi, lakini matokeo yake sasa hivi ile kazi ya kuziba mianya ya fedha tunamrejeshea yeye Waziri, sasa sisi kazi yetu itakuwa nini hapa.

Na hili nalisema kwa sababu mimi namshukuru Mhe. Waziri katika bajeti ya mwanzo kabisa tulilaumu sana vianzio vya mapato, upotevu wa fedha. Alitueleza kwamba naomba Waheshimiwa Wawakilishi nionesheni mianya ya fedha inavyopotea, nisaidieni, nitashirikiana na nyinyi kuhakikisha kwamba fedha hazipotei.

Juzi tu lakini hapa kulikuwa kuna harufu, tena harufu yenyewe nzuri ya upotevu wa fedha za Serikali, au matumizi mabaya ya fedha za Serikali. Sasa hawa ambao waliomwambia Mhe. Waziri wa Fedha azibe mianya ya upotevu wa

fedha wao ndio waliokataa Baraza la Wawakilishi lisiende kuchunguza ubadhirifu huu. Halafu leo kazi hii tumwambie Mhe. Waziri wa Fedha, mimi nadhani hatumtendei haki. Kwa hivyo, hilo nilisema nilitangulize ili tujue kwamba sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ni nini wajibu wetu ambao tulioujia hapa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze na hawa ndugu zetu wanaotusaidia kufikisha ujumbe kwa wananchi wetu katika majimbo yetu, lakini na Tanzania nzima na duniani kwa jumla. Kwa sababu sasa hivi dunia imekuwa kijiji, tunazungumza kwenye Baraza la Wawakilishi sasa hivi waliokuwepo London, waliokuwepo wapi aki-*tune* mwenyewe kupitia mitandao ya kijamii anatuona jinsi gani tunavyozungumza. Sasa nakuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha wewe ni mtu mkarimu sana, kuna mashirika unayafuta, lakini kuna shirika jengine hivi karibuni umeliunda, Shirika la *ZBC*.

Mhe. Mwenyekiti, shirika hili bado linahitaji kulelewa kwa nyenzo na vitendea kazi, lakini kitu maalumu ambacho ninachokuomba hapa Mhe. Waziri angalau hawa wanaotusaidia kurusha haya matangazo yetu hapa kesho kutwa Ramadhani inakuja. Mhe. Mohammed Haji Khalid hapa mchana alipokuwa akizungumza anasema "Ukiona kilemba kimeroa shuka sijui iko hali gani". Sasa ukiona yeye Mhe. Mohammed Haji Khalid Mwakilishi anaomba apatiwe afueni kama Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi. Je, hawa wenzetu wapo hali gani? Sasa nilimwambia Mhe. Mohammed kwamba hapa Unguja kwa bahati huku watu hawavai shuka. Sasa kama kilemba kimeroa kwa Unguja, hapa shuka haivaliwi lakini najua Mhe. Waziri umeshajua nini ambacho kitakachoroa.

Kwa hivyo, ndugu zetu hawa wanaotusaidia kurusha matangazo kwa kweli utafute namna ya kuwaangalia. Kwa sababu posho yao hawa inachukua miezi sita ndio kulipwa, kesho kutwa Ramadhani, sikukuu na nini. Kwa hivyo, naomba sana, fanya mpango wako maalumu kwa maelekezo kwamba fungu hili hebu wasaidieni hawa waliokaa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kipindi chote hichi. Sasa hilo ndio la mwanzo.

Jengine Mhe.Mwenyekiti, nilikuwa naomba sana ndugu zetu wa *ZRB. ZRB* ndio chombo ambacho kinachosimamia makusanyo ya fedha na tukaweza kulipwa mishahara, tukaweza kutoa huduma mbali mbali katika nchi yetu. Sasa kuna baadhi ya wafanyabiashara wamejaribu kutufuata na kutulalamikia. Sasa ninamuomba Kamishna kupitia kwako Mhe. Waziri wa Fedha kwa *ZRB*.

Kwanza wamelalamika kidogo wenye vituo vya petroli, kwamba wanasema ile ada ambayo au kodi inayochukuliwa na *ZRB* ni kubwa kidogo. Sasa mimi nilikuwa naomba kwa sababu wamenijia wawili, lakini ninajua ni mtandao mzima. Hebu angelijaribu kukaa nao, wana mapendekezo yao, na mimi nilivyoyasikia ni mazuri. Kwa sababu wao wamesema kwamba ukiona kimya kingi kina mshindo. Kwa hivyo, ina maana kwamba ile kodi ambayo munawakata pengine faida wanapata ndogo, wengine sasa wanasababisha kuchakachua mafuta wakachanganya na mafuta ya taa.

Sasa hili sitaki nilizungumze sana kwa sababu kama nilivyosema nakuomba Mhe. Waziri uzungumze na Kamishna wa *ZRB* akae na wawekezaji wa vituo vya petroli asikilize hichi kilio chao, lakini kuna kituo cha petroli *specific* ninakitaja ambacho kipo Mwanakwerekwe. Juzi nilikwenda kutia mafuta pale, nilipokwenda pale tena nilikwenda kutia mafuta kama kwa bahati mbaya, kwa sababu nilikuwa ninaelekea kile cha mbele lakini nikaja nikaingia pale.

Kitu ambacho alichonieleza, Mheshimiwa naomba mutusaidie nyinyi ndio munaotunga sheria. Mimi hapa pana vituo vitatu vya petroli vipo pamoja. Leo hapa ile njia ya Mwanakwerekwe, kuna sehemu ilikuwa kuna *gape* imekatwa katikati ya barabara ya kuingilia kwenye kituo cha petroli. Wenzetu wa *UUB* wamekwenda wamekiziba pale. Halafu sio hivyo tu, wakaweka na kituo cha daladala pale. Kwa hivyo, ile sehemu ya kuingilia katika kituo chake cha petroli, ndio sehemu iliyowekwa daladala halafu ile njia imezibwa. (*Makofi*).

Kwa hivyo, ina maana kama ni sawa sawa kwamba unampiganisha ngumi, mmoja umemfunga mikono. Sasa wale ndio walipa kodi wenyewe, mtu pale amewekeza analipa wafanyakazi mishahara na kulipa kodi zote, lakini mumemtengenezea mazingira ya kwamba biashara yake asifanye vizuri. Sasa nilikuwa naomba Kamishna wa *ZRB* angejaribu kutembelea kile kituo cha katikati, baina ya cha mwanzo pale Mwanakwerekwe, kile cha katikati halafu kile cha mwisho. Sasa pale palipowekwa kituo cha daladala, tunaomba awatafute wale wanaohusika na vituo vya daladala, lakini vile vile azungumze na watu *UUB* waondoe ile *block* yao waliyoiweka pale ili zipate gari kupita na kuingia na yeye aweze kufanya biashara sawa sawa na wenzake, vyenginevyo ndani ya miezi sita huko mbele itabidi afunge kituo na wale vijana wetu pale watakosa ajira.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nilikuwa namuomba Mhe. Waziri, kuna wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki waliokuwepo Zanzibar. Wao hawa tuna taarifa kwamba kuna fedha za malipo zililetwa hapa lakini baadae zikarudishwa Tanzania Bara. Hebu hili Mhe. Waziri kutokana na muda sitaki nilifafanue lakini ninafikiri ukizungumza na watendaji wako, watajaribu kukueleza, tena kuna wengine wameshakuwa marehemu tumeletewa *documents* zao hapa, kwamba fedha zao zilikuja lakini tunashangaa ilikuwaje walishindwa kupatikana mpaka fedha zile zikarudi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini jengine nilikuwa ninataka kuzungumza hoja ambayo ninamuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Nazungumza hoja hii ili wanisikie kwa sababu hapa Barazani tunazungumza na serikali. Serikali tunazungumza Kiongozi Mkuu ni Makamu wa Pili wa Rais. Juzi tulizungumza na Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, namuomba pia naye anisikilize Mhe. Jaku Hashim Ayoub acha kuzungumza naye, kuna hoja ninaileta.

Juzi tulizungumza sana kuhusu Mamlaka ya Uwanja wa Ndege na tukazungumza kadhia ya mtu ambaye ule uwanja ameufanya kama wa baba yake. Tulitegemea vituko vile angekuwa ameshaanza kuondoa. Vimeanza upya. Leo lile geti la kuingia pale la kuingilia limefungwa unaambiwa gari yako upitishe huko, hata kama kuna mvua, kwanza uroe ndio uingie. Leo juzi tunazungumza nini, leo munatufanyia kitu gani. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, jengine pale kama nilivyosema kwamba yule hatumjui kama ni meneja wa uwanja wa ndege au meneja wa Kampuni ya *Aerotek*. Leo katika lile anga la *Aerotek,* mimi ninasema anga la SMZ lakini yeye amelifanya kama anga la kwake. Kuna ndege ambazo zinatoka Afrika Kusini, ndege mbili zinakuja kufanyiwa matengenezo, amezizuia ndege zile zisije. Sasa afanye kazi moja, na tulisema hapa serikali yule mtu aulizwe, anataka kufanya kazi yake ya kuendesha anga au anataka kufanya kazi ya Mkurugenzi wa Mamlaka.

Leo kwa ubinafsi wake, kwa chuki zake na wale ambao aliowakodisha, ameamua kuzuia ndege mbili ambazo zinakuja kwenye matengenezo. Sasa mimi ninashangaa, hii serikali watu wanaifanya kama, yaani imekuwa kama shamba la bibi, kila mtu anajifanyia anavyotaka. Sasa mimi ninadhani Mhe. Mwenyekiti, nadhani siku moja hapa tuje tufanye kile kitendo ambacho labda tutaonekana sote wabaya huko. Tufanye maamuzi magumu ya kukataa bajeti ya aina yoyote, alau serikali iweze kutusikia. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, tunazungumza juzi, leo mtu anafanya vile vile. Halafu yeye kitu kikubwa anasema awali anadaiwa. Sasa kama anadaiwa si wanadaiana wao wenyewe kwa wenyewe. Yeye mwenyewe hilo anga la *Aerotek* anadaiwa na *ZRB* pesa chungu nzima hajalipa. Sasa Mhe. Mwenyekiti, yaani sisi tumekuwa, yaani imekuwa kama mbuzi unampigia gitaa nda! nda! nda! yeye huku anakula majani. *(Kicheko/Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, tunaomba pale uwanja wa ndege awekwe mtu ambaye atakayeweza ku-*manage* uwanja mapato yakapatikana. Leo hizo ndege mbili tunajua zikitua hapa zitalipa kiasi gani, anazizuia kwa ubinafsi tu. Sasa hili nilisema Mhe. Mwenyekiti, niliseme na ingawa tumempa kazi Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, tunajua kazi ile anayojua na hii *package* nyengine niliyoizungumza leo, naomba aingize katika hiyo *package* ile ya juzi na hii aingize. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba vile vile katika suala zima la wenzetu hawa *ZIPA* kama nilivyosema. Mradi ambao niliosema kuwa nitazuia fungu la *ZIPA*. Mhe. Mwenyekiti, hili bora nizuie, Mhe. Waziri nije nizuie ule mshahara wako, ndipo utakapolifanyia kazi kwa vizuri. Nimelizungumza katika bajeti kuu ya serikali, tupewe sababu gani ya mwekezaji anayejenga Chelezo Mangapwani mpaka leo ameshindwa kupewa kibali na *ZIPA*.

Sisi tunavyojua taratibu za kawaida, *assessment* ya mazingira ifanyike, ninafikiri Mhe. Makame Mshimba Mbarouk amefanya kazi kubwa akakusanya Waziri, watu wa *ZIPA* na mwekezaji, watu wa mazingira. Tatizo lilikuwa ni moja kwamba itapatikana *certificate* ya mazingira basi mradi ule uta-*take off, certificate* ya mazingira ipo lakini mpaka leo tunashindwa kutoa kibali hichi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kama nilivyosema wewe ni swahibu wangu sana na Mkurugenzi wa *ZIPA* ni swahibu sana na wewe mwenyewe unajua, lakini hapa kama nilivyosema tupo kazini.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa ninataka kuzungumzia kadhia ya wale maafisa wa *TRA* walio-*escort* makontena Zanzibar. Mhe. Waziri juzi tulizungumza kwa kauli kubwa, kwa kauli kali sana. Tunataka tupate maelezo umeshawaamua warejeshwe au bado wapo wanakuja kufanya *inspection* hapa. Hili naliomba, katika vikao vyenu vya kero za Muungano, muwaeleze watu wa *TRA* kwamba Zanzibar kuna serikali kamili, huku kuna uongozi kamili, huku kuna Rais na hayo mapato yanayokusanywa Zanzibar hayaendi pahala popote, yanakusanywa hapa Zanzibar. Kwa hivyo, kama tutafanya uzembe wa kukwepa kodi tukawaachia watu wanavyotaka, huo utakuwa ni uzembe wetu.

Sasa leo inakuwaje maafisa watoke Tanzania Bara wa *TRA* waje ku-*escort* mzigo hapa, yaani hapa hakuna uongozi? Mimi nafikiri hili ni jambo ambalo halipendezi hata kidogo.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa ninataka nizungumzie suala la misamaha. Nilizungumza sana katika bajeti ya mwanzo kabisa kwamba misamaha ya saruji ambayo inayokwenda katika sehemu za uwekezaji. Mhe. Waziri leo ninajua utatoa majumuisho, lakini sijui kama utaweza kupata hizo takwimu, tujue ndani ya miaka miwili saruji tani ngapi imetolewa msamaha na zilikwenda katika uwekezaji gani na gani. Hili vile vile ninaweza kidogo nikaja nikarusha vumbi ili nipate hii takwimu, kwa sababu kuna taarifa ambayo sio rasmi, lakini tunajaribu kuendelea kuzifuatilia kwamba kuna saruji inatoka, kwamba inaambiwa imetolewa msamaha lakini baadae inarudi madukani. Na hili ninafikiri kama litakuwepo litapunguza mapato ya nchi.

Chengine Mhe. Mwenyekiti, kuna kitengo chako Mhe. Waziri, kuna kitengo ambacho umekizaa wewe, umekilea wewe, sasa hivi hakina mwenyewe. Mhe. Mwenyekiti, wahasibu wote wapo chini ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, wote wa wizara, na wanapangiwa kazi na utaratibu wote unasimamiwa na Mhasibu Mkuu wa Serikali, lakini kuna kitengo cha *procurement*.

Mhe. Mwenyekiti, kitengo hichi, kwanza taasisi hii ni mpya na ilipoanza kuna wataalamu ambao Wizara yako wa Fedha iliwapeleka Tanzania Bara, ninafikiri kama watano kama sikosei, muliwapeleka kwenda kujifunza masuala ya *procurement*, baadae wale baada ya kurudi mukaanza kuwasambaza katika maeneo mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hawa hawawajibiki kwa Waziri wa Fedha, hawa wanawajibika kwa kila wizara. Sasa hapa kuna tatizo Mheshimiwa, kwa sababu hawa ni watu wa *procurement*, kama mutawaacha.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan Juma umebakiza dakika 3.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Tatu Mheshimiwa aah! Sasa ninafupisha maneno naomba hawa watu wa *procument* uwarejeshe katika vitengo vyako, wawe chini ya usimamizi wa taasisi yako, yaani uwatafutie Mkurugenzi ambaye atakayekuwa anawasimamia. Kwa sababu hawa Wahasibu tunajua ni Mhasibu Mkuu lakini hawa watu wa *procurement* huwezi ukawaacha wakasambaratika kila mmoja akawa katika wizara yake.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nitaomba nitakuwa ninasema neno moja moja. Sasa hili lakini utakuja kumpatisha tabu Mhe. Waziri katika vifungu kwa sababu itabidi nije nipate ufafanuzi. Sasa nakuja ili kumaliza hizo dakika ulizonipa.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba tu kwamba haya maeneo huru ya kiuchumi kwa wakezaji wazalendo, kuna masharti gani. Kwa sababu kuna mwekezaji mmoja anasema anataka kuanzisha kiwanda cha vibiriti lakini vile vile alikuwa anajaribu kuangalia serikali itakuja kumlinda vipi pale atakapoanza uzalishaji, lakini vile vile upatikanaji wa yale maeneo masharti yake yako vipi.

Kuna viwanda kama vitatu lakini nitataja hicho kimoja tu cha vibiriti. Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri kuna madeni haya ya vikosi vya SMZ. Wale vikosi vyengine waliambiwa wao walipe katika bajeti zao, lakini KVZ wao waliambiwa mzigo huu waubebe Wizara ya Fedha ili kuweza kulipa madeni yale ambayo walikuwa wanadaiwa.

Sasa hili pia nilikuwa naomba ulichukue ulifanyie kazi lakini vile vile suala la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii tunawapongeza kwa kujenga Kiwanja cha Watoto cha Kariokoo, lakini mnara mbona mpaka leo umesita. Tulikuwa tunaomba na ule mradi wa ujenzi wa nyumba za mkopo nafuu, tulikuwa tunaomba tu, pamoja na kwamba hawajapata wale wafadhili wa *joint venture*, lakini alau wao wenyewe wangeanza japo *block* moja au japo nyumba tatu nne, wakaanza mimi ninaamini wako wawekezaji na wajaribu kutafuta namna ya kuuza *shares*. Mimi ninafikiri

sisi wengine tutanunua *shares* na tutawashawishi watu wengine waje wanunue *shares* ili Shirika liweze kufanya kazi vizuri. (*Makofi*).

Jengine Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Bima hapa nilikuwa ninataka nipate maelezo, kwa sababu katika fedha ambazo walizokusanya, fedha walizozitenga kwa ajili ya miradi ya maendeleo, wametumia asilimia 40 tu. Sasa mimi hapa ninataka nije nipate maelezo kwa nini wametumia fedha za maendeleo asilimia 40 tu na asilimia 60 hawakuweza kutumia.

Mhe. Mwenyekiti, lakini na Chuo cha Chwaka hapa wamesema kwamba wanatoa mafunzo ya ujasiriamali. Mhe. Waziri hapa nilikuwa kidogo ninataka uje unisaidie ufafanuzi, kwa sababu wajasiriamali katika maeneo yetu wapo wengi, tujue mfumo wao kama je, tunawapeleka kule Chuo cha Chwaka kwenda kusoma au wao wanakuja kutoa taaluma wao, watakuja majimboni kwetu kuja kutoa mafunzo ya ujasiriamali.

Vile vile Chuo hichi kila siku kinakua na kupanuka, sasa kwa taarifa nilizokuwa nazo, wale walimu waliopo pale ninafikiri wana kiwango cha juu kabisa, wana *masters*. Sasa kwa kuwa kila siku kile chuo kinataka kuboreshwa. Je, kuna mpango gani, sijaona katika kitabu kwamba labda kuna bajeti ambayo ya kuweza kuwasomesha walimu ngazi ya *PhD*, na wapo ambao wanaotaka hiyo fursa lakini inaonesha humu katika bajeti Mhe. Waziri naona kama itakuwa hujatenga hilo fungu.

Halafu Mfuko wa Barabara vile vile nitataka maelezo. Wametumia fedha karibu asilimia 59 tu, kuna fedha karibu asilimia 41 hazikutumika katika Mfuko wa Barabara, wakati sisi tuna barabara zetu nyingi ambazo zinahitaji ukarabati. Sasa nilikuwa namuomba Mhe. Waziri kupitia Mkurugenzi wa Mfuko wa Barabara. Kuna barabara ambayo tunaishukuru serikali kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ya Kwa-Abass Hussein, Shaurimoyo inayokwenda Mboriborini mpaka Kilimahewa. Barabara ile Mhe. Mwenyekiti, tulisaidia kujengewa ile sehemu ambayo iliyokuwa korofi.

Sasa kupitia Mfuko huu wa Barabara, kwa kuwa nimeziona pesa zimebakia, naomba ile sehemu iliyobakia basi hizi fedha wazipeleke kule Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara watukamilishie. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, mji ili uwe jiji na Zanzibar inaitwa jiji, lazima barabara zote za *feeder roads* zote ziwe na lami.

Mhe. Mwenyekiti, ninafikiri baada ya hayo ili nisikuchoshe nilikuwa ninataka tu kusema hayo, lakini zaidi kama nilivyosema kuna baadhi ya maeneo nitakuja kuzuia mafungu, lakini ninaamini kwa Mhe. Waziri ninavyomjua makini atalifuatilia kwa kina ajue nini tatizo, atakuja kunijibu pengine hata hiyo buti sitawahi kupiga.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nitakuja kuunga mkono baada ya maelezo ya kina na mwanana ya swahibu wangu Mhe. Waziri wa Fedha. Ninakushukuru sana. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hamza. Mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mhe. Mahmoud Thabit Kombo na baada ya hapo nitamkaribisha Mhe. Waziri wa Fedha aweze kuja kujibu masuala ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameyauliza na kutaka maelekezo.Ahsante.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni hii ya leo. Naomba kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa kitabu chake kizuri chenye taarifa za kutosha lakini pia kuna vitu kidogo vimejificha ficha ambavyo katika mchango wangu, nitaomba ufafanuzi ili wananchi tunaowawakilisha nao waweze kujua.

Pili naomba nimpongeze mtendaji mkuu wa wizara hii Katibu Mkuu pamoja na watendaji wengine wote, hao waliokuwepo kwenye mashirika, Benki ya Watu wa Zanzibar, *ZRB*, Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi, Mamlaka ya Mapato Tanzania, pamoja na Bodi na mashirika, kama vile Shirika la Bima na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, wote ninawapongeza kwa kazi nzuri waliyoifanya. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, naomba katika kuchangia Mhe. Waziri kwanza kabisa yeye ana *experience* kubwa sana. Yeye ni *very senior civil servant*, amefanya kazi kwenye serikali kwa muda mrefu sana, anayaelewa haya mambo vizuri sana na Mwenyezi Mungu pia kamjaalia alikuwa ni Naibu Waziri wa Fedha kwenye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambapo kule alikuwa ana-*handle trillions of budget*. Kwa sababu wenzetu bajeti yao ni kubwa mno, wao wenzetu uzalishaji wao na matumizi yao ni makubwa.

Na yeye Mhe. Waziri alipata *experience* kubwa sana ya huko, lakini pia mtendaji kwa wizara hii, yeye bahati nzuri ameshakuwepo kwenye *tax collection*, ameingia kwenye *private sector*, ameingia kwenye *business sector*, halafu akarudi tena serikalini. Kwa hivyo, pia anakuja na *experience* ya kutosha.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, suala langu la mwanzo kabisa ninalotaka kusisitiza hapa, *mali bila daftari hupotea bila ya habari*. Hili suala la *Assets Register* la serikali, daftari hili la kudumu la mali zote. Ninakumbuka mimi linazungumziwa tokea ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005-2010, lakini mpaka leo bado hatukuona chochote kilichokamilika. Namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa alizungumzie angalau kwa *summary* mali yenu mimi niliyeko huku nyuma pamoja na wananchi, naona kwamba nyinyi mali munayo lakini mumeikalia na hamujui. Serikali ina mali ya kutosha lakini hakuna utaratibu wa kuifahamu mali yake.

Juzi Mhe. Mwenyekiti, tulicheza foliti kidogo hapa na Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, lakini bahati mbaya ameshaondoka kidogo, lakini ninaamini atarudi baadae na tulikuwa tunazungumza hapa hapa. Niliuliza kipengele kimoja tu cha *ZANTEL*, ilikuwa ni *shares* za *ZANTEL* ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ilinyanyuka serikali nzima ku-*defend*. Wakati kile nilichokuwa ninakiuliza mimi si kwa faida yangu mimi, ni kwa faida ya wananchi wa Zanzibar, na kwa faida ya serikali yenyewe ikiwa na mali yake. (*Makofi*).

Sasa leo nikaambiwa siku hiyo kama *hansard* zitakuwa zinasema sahihi, nikaambiwa nisubiri siku itakayokuja Wizara ya Fedha.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atwambie hili suala la *Assets Register*. Makampuni binafsi wao huwa na *cord number* wanafanya na wanaweka *bar cord*, na siku hizi mambo ya *electronic* yanakuwa yote *registered* na yanajulikana. *Asset* ikitoka inajulikana, *asset* ikiingia inajulikana na *asset* ikishakwisha muda wake inataka kuuzwa pia inajulikana. Kwa hivyo, angekuja akasema *asset register* hii imefikia wapi na ningependa kujua hizi *shares* zetu za Zantel thamani yake ni kiasi gani, hii asilimia 18 inayozungumziwa. Maana wanakopa mapesa kila pahala, lakini hizi asilimia 18 sasa kutokana na *balance sheet* ya mwisho au *official audited account* za Zantel ni kiasi gani kasma yetu, serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wananchi *shares* zao mule ndani ni mamilioni au mabilioni mangapi.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, naomba nielekee sehemu ya *revenue* leo zaidi kuliko matumizi. Mhe. Waziri hakuliweka wazi suala la *deficit*. Katika bajeti hii nzima Mawaziri wote watasimama kuanzia mwanzo mpaka mwisho na wote wataulizwa, mbona hili halijatimia na hili halijatimia. Jibu litakuwa mara nyingi la kisanii, lakini jibu halisi ni kwamba pesa hakuna na kuna upungufu. *General deficit* ya vitabu vyote ama hiki kitabu kikuu inaonesha kama ni asilimia 40. Namuomba Mhe. Waziri akija aliweke wazi, *deficit* yetu ni kiasi gani.

La tatu, *deficit* yetu katika hizo fedha za nje tunazokwenda kukopa na kuomba, kwa sababu hata wao pia wamepunguza kukopesha na wamepunguza kuombwa ama kutoa kile wanachoombwa, na kule pia *deficit* yetu. Ameeleza asilimia lakini hakuna *deficit* inayoonesha *clear list* kwamba *deficit* yetu sisi ni kiasi gani, lakini bajeti nzima ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwenye bilioni 709 kuna *deficit* ya asilimi 40. Sasa katika *deficit* hiyo vipi sisi tutatarajia kutimiza haya malengo yetu ya maendeleo tuliyojiwekea, ni ngumu kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nijaribu kutoa rai na ushauri kwa Mhe. Waziri ambapo yeye atatupa maelekezo yake, baada ya kumpongeza kwamba ni hodari na mtendaji wake ni *genius* katika wizara hii wanaweza kuja na mambo haya yafuatayo.

La kwanza kabisa Mhe. Mwenyekiti, hakuna *department*. Juzi niliuliza kwenye swali asubuhi hapa na Mhe. Waziri alinijibu vizuri sana, kwamba amelipokea na litashughulikiwa, lakini naomba hili litekelezwe haraka sana. Hakuna *department* ambayo *dedicated* ina ma-*genius* wa kubuni mapato. Hapa ukisoma idara zote, kuna Idara ya Usimamizi na Utunzaji wa Mapato na Udhibiti wa Rasilimali za Umma, katika ukurasa wa 5 inasema hivi:

"Jukumu la kusimamia, kutunza na kudhibiti rasiliamali", lakini hakuna jukumu la kuzalisha au kubuni uzalishaji wa mapato.

Ukienda katika idara hii ya kabla yake, hata katika majukumu makuu ya Wizara ya Fedha katika ukurasa wa 3 limo, kusimamia mapato ya serikali yakiwemo ya ndani na yale kutoka nje. Kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za

umma ikiwemo uratibu wa deni la Taifa. Kusimamia mali za serikali pamoja na mashirika ya umma, kutoa huduma za kiuhasibu serikalini, kusimamia sekta ya fedha nchini na maendeleo yake na kutoa huduma za utawala, kiutumishi na idara zake.

Kwa hivyo, mimi naomba aidha katika majukumu haya liongezwe jukumu maalum la kubuni, *innovation;* bila ya *innovation* ya kuzalisha *revenue* basi Mhe. Waziri kila siku tutakuwa tunakuja humu ndani tunapiga blaa blaa, tunakula fedha za wananchi halafu tunanyanyuka tunatoka, wizara zote zitakuwa na *deficit* na kila wizara moja ina *deficit* kwenye *average* asilimia 40.

Mhe. Mwenyekiti, katika wizara ambayo imepata fedha kidogo si haba za kutosha ni Wizara ya Fedha, wako kwenye kati ya 60 na 80 asilimia wanapanga humo humo na idara zake. Sasa hapa inaonesha dhahiri kwamba wao ni wasimamiaji wakuu, na kwa sababu vitu vingi viko *centralized* kwao. Siku hizi hata ukitaka kulipia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati vitu vyao vyengine unapitia Wizara ya Fedha, ukitaka kulipa vitu vya wizara nyengine kama ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo au wizara nyengine yoyote, risiti na mfumo wa risiti zinaandikwa humu, wanachapisha takriban risiti 20, 000 zote zimo katika mfumo wa *centralized*. Ilifanyika katika mfumo wa *centralized* kwa sababu ilikuwa ni kudhibiti ili mapato yetu yasivuje, kwa sababu huko nyuma kulikuwa na uvujaji wa mapato, kwa hivyo ndio tukaachana na ile *system* ya *decentralized* kila mmoja anaweka hesabu zake tukaenda kwenye *centralized system*.

La pili Mhe. Mwenyekiti, ni muhimu sana katika mashirika binafsi ama kampuni binafsi, *projection* zote zinazowekewa za *revenue* zinakuwa kubwa. Mara nyingi makampuni ama mashirika binafsi *projection* zake wanafikia asilimia 50 tu, na wakifikia asilimia 50 pia wanapongezwa. Sisi utakuta wengine wanafikia asilimia 80 au 97, au 98 tunawawekea *projection* ndogo na mara nyingi tunawaachia wao wenyewe walete maoni yao Wizara ya Fedha, wanakuwa wanaulizwa. Je, mwaka huu mnatarajia kukusanya kiasi gani. Alaa! tusiwaulize mwaka huu mnatarajia kukusanya kiasi gani, tunawawekea *target* kutokana na bajeti yao waliyoomba, kutokana na hizo *ceiling* zilizowekwa, mwaka huu mtatarajiwa kukusanya kiasi fulani, kila idara ya serikali, kila *department* na kila wizara iwekewe mfumo huo.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri ningependa kupata kauli yako je, mnao mpango wa kuwawekea *projection,* wawekeeni juu zaidi hata kama wakifikia asilimia 50 au 60 tutawapongeza katika hizo watakazofikia, lakini sio kwa *deficit* kiasi kikubwa namna hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nataka kuzungumzia kidogo haya mashirika yenye fedha nyingi sana, ambayo wenzetu Tanzania Bara wanayatumia vizuri sana na sisi Zanzibar bado hatujaamka tumelala. Tutazungumzia zaidi *ZSSF* kwa sababu ile ni *reserve* ambayo inakusanya mapato kutoka kwa wananchi kama *contribution* zao, lakini fedha zile zinaendelea kubakia za wananchi mpaka hapo watakapostaafu.

Vile vile napenda kuizungumzia benki yetu *PBZ* na pia eneo la *petrol* na *ZRB*. Mhe. Mwenyekiti, utagundua mara nyingi sana hawa *ZSSF* na *PBZ* pesa zao za *reserve*, mara nyingi wanakuwa wanaweka katika *treasure bill* ama *treasure bond* au wataalamu huwa wanaita *TB* wenyewe, sio *tuberculosis* hapana, *TB* yaani *Treasure Bond* zinawekwa na hizi huwa zinanunuliwa *BOT*. Swali langu liko hapa, yale ni mashirika ambayo watu wanachangia kwa jasho lao moja kwa moja, nia yake ni kukuza uchumi na kuwakuza wale wachangiaji ili wawe wengi zaidi kwa sababu wale ndio *customers* ama wateja wao waweze kuchangia zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa leo tunapochukua ile *reserve* yote tukaiweka kwenye *treasure bond*, tunasema kwamba ile *low risk*, hakuna *risk* yoyote katika kuweka *treasure bond*. *Interest rent* yake tunayoipata katika *treasure bond* ni ndogo kuliko zile fedha zilizozungushwa katika uchumi. Mhe. Mwenyekiti, nitampa mfano Mhe. Waziri kwa kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti. Wenzetu tuwachukulie mfano *NSSF*, sasa hivi *NSSF* nusu ya fedha zao kule kwa Dk. Dau wanaweka kwenye *treasure bond*, lakini na nusu ya fedha zao wanazizungusha sasa hivi kujenga majumba na hizi nyumba nyingi ni *low cost houses*, kwa sababu gani na pia hawazitumii zile fedha za wananchi, wanatumia zile fedha kama dhamana katika benki ili kupata mkopo mkubwa zaidi wa kujenga majumba.

Mhe. Mwenyekiti, juzi *NSSF* wamefungua nyumba karibu 1200. Kwa hivyo na sisi hapa Zanzibar tuna tatizo leo la makaazi. Tatizo hilo lipo miongoni mwa hao wachangiaji wana *ZSSF* ambao takriban kila mwananchi pamoja na mimi tunazo kadi zetu za *ZSSF*. Tatizo hilo pia lipo kwa upande wa serikali kutoa makaazi mazuri kwa wananchi wake, lipo hilo tatizo na ardhi maeneo yapo, kama maeneo ya Tunguu na maeneo mengine mbali mbali. *ZSSF*

Mwenyezi Mungu keshawajaalia bahati wana ardhi nzuri sana hapa Mbweni, kwa sababu walirithi ama walinunua kutoka *Zanzibar Insurance* hizi nyumba hapa Mbweni, nyuma yake kuna ardhi kubwa sana. Pia wana ardhi nzuri sana Tunguu.

Mhe. Mwenyekiti, badala ya kuhangaika kwa ajili ya makaazi leo fedha zile badala ya kukaa katika *treasure bond* kule Bara, zinafaidisha uchumi wa Bara zaidi na wakati mchangiaji ni kutoka Zanzibar ni *ZSSF*, mchangiaji ni *member* wa *ZSSF* na sio *member* wa *NSSF*. Hata wale wanaofanya kazi katika Mashirika ya Muungano, uchangiaji wao unakwenda *NSSF* hauji *ZSSF*.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ninachokuomba hizi fedha, mara nyingi ukizungumza watu wa *ZSSF* wanakiri kwamba mikono yao imebanwa hawaruhusiki kisheria. Sasa kama hawaruhusiki kisheria basi zile sheria ziletwe hapa Barazani, ili tuzi-*modify* na hawa kwa viwanja vyao walivyokuwa navyo wanaweza kujenga maghorofa manne tu Tunguu na kila ghorofa liwe na ghorofa 25. 25 mara 4 ni 100. Kila *floor* katika hizo hizo *floor* 100 zikiwa na sehemu 4 zimegawana.

Leo Zanzibar tayari ina nyumba mia 400, nyumba zenye vyumba viwili hadi vitatu, *self container* 400. Mhe. Mwenyekiti, tutakuwa na shida ya makaazi tena. *DIASPORA* yetu hiyo tunayoizungumzia, kuna idara maalum imeanzishwa ya *DIASPORA* ambayo iko Ikulu. *DIASPORA* wote wale wanataka kuwanunulia nyumba wazazi wao, wanataka kuwanunulia nyumba ndugu zao, wanataka kuwanunulia nyumba wazee wao. Wanashindwa siku hizi kuleta pesa kwa sababu wengine walikuwa wanapigiwa picha za viwanja lakini matofali hakuna.

Mhe. Mwenyekiti, *DIASPORA* wale wale leo kwa pesa hizo hizo ndogo ndogo wanazochangishana na kupata kama kipato chao wataweza kununua. Mimi naamini kwamba tunaweza kuuza nusu ya majumba hayo ya ghorofa 200 kabla hata hazijamalizika. Kwa hivyo, fedha zao hawa *ZSSF* zitakuwa ni katika dhamana nzuri, benki ya *PBZ* watawakopesha na benki yetu ya *PBZ* sasa hivi *Alhamdulillah,* sasa hivi Mwenyezi Mungu katujaalia ina *reserve* ya kutosha na ingepewa dhamana nzuri kwa *ZSSF* kukopa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sipingi pale Kariakoo ni jambo zuri sana, lakini pia tuangalie uzalishaji wake, Kariakoo itazalisha kiasi gani. Ningependa sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa, aniambie ile Kariakoo tunatarajia itakuwa inazalisha kiasi gani kwa mwaka, kwa sababu hali zetu tunajijua maskini. Mtoto wa kimaskini akienda skukuuni anapewa shilingi 1,000 anaambiwa hiyo hiyo kachori, badia utanunulia hiyo hiyo na pale anatarajia kuingia kwa kiingilio hicho hicho.

Je, mtoto huyu na yeye tutamfaidisha vipi. Namuomba Mhe. Waziri akija aniambie tu kwamba tunatarajia kiasi gani tutapata pale Kariakoo, na pili atwambie kwenye mnara ule na pale patakavyojengwa na mambo yote mazuri ya pale, tunatarajia kiasi gani tutatengeneza.

Mhe. Mwenyekiti, suala la nne namwambia Mhe. Waziri kwenye nyumba za makaazi, mimi naweza kumpa yeye *projection* kwamba atauza asilimia 50 ya nyumba hizo kabla hazijamalizika. Wawakilishi humu humu, kuanzia Makamu wa Rais serikali kule mbele mpaka sisi tutanunua nyumba.

Mhe. Mwenyekiti, sitaki kukwambia mengi lakini *NSSF* mimi nimenunua nyumba kwao na bei ni nafuu sio ghali. Katika mpango huo huo, kwa sababu nilikuwa ni mchangiaji wao, nina kadi ya *NSSF* na sheria hainikatazi.

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kumalizia

Mhe. Mwenyekiti: Malizia Mhe. Mjumbe.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Nina muda wa kutosha, si ni mpaka saa mbili kasorobo.

Mhe. Mwenyekiti: Hapana. Mhe. Waziri anataka kufanya majumuisho sasa na zimebakia dakika tatu tu za kwako.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mengine nitamuandikia *Inshaallah* kwa sababu ndio hapa yanakuja yale mambo ya urafiki, ushemegi na kile kitu, nitamwandikia tu haina tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia mimi naomba hili suala la petroli tuliangalie tena. Serikali ikikaa inafikiria kwamba kila tukiweka kodi kubwa katika mafuta, maana yake *one of the high taxed* ni mafuta, ile kasma ya serikali na bei ya mafuta halisi pamoja na faida anayopata yule mletaji mafuta. Sisi tupo *among the highest percentage wide*, atalieleza Waziri hili. Sisi tunafikiria kila tukiweka kasma ya serikali kubwa ndio serikali itaweza kufidia ile *deficit.* Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani hilo ni kosa, kila tukienda kwenye *volume* kubwa ya mafuta ndio *tax* itapatikana zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi Mzanzibari yeyote kabla hajawasha gari lake au pikipiki yake, basi anafikiri mara mbili kutokana na bei ya mafuta. Hata akiwa na safari yake ya kwenda shamba leo ni tofauti, kesho tofauti na kesho kutwa ni tofauti, basi anaiambia familia yake, ngojeni tutakwenda keshokutwa sote kwa pamoja, tunajaribu ku- *narrow down*. Pahala peke yake ambapo mtu mwenye vespa ananunua mafuta mpaka ya shilingi 500 ni Zanzibar, yote kwa sababu ya ughali.

Mhe. Mwenyekiti, bei ya mafuta sasa hivi duniani kidogo inashuka na sisi tungeweza kidogo hii kasma ya serikali na wale wanaoleta mafuta tukawabana ili waweze kushusha. Mhe. Mwenyekiti, naamini mimi kwamba serikali itajikuta inakusanya pesa nyingi zaidi kwenye *tax* hiyo ya mafuta kwa *volume*, kwa sababu mwananchi hatabiriki zaidi na mafuta ndio yanayochangia moja kwa moja maendeleo na uzalishaji. Kwa hivyo, tukipunguza bei kidogo, tusiogope kwenda tofauti na wenzetu. Tukipunguza bei kidogo mafuta hapa yakawa rahisi zaidi basi watu watatoka huko kuja kununua mafuta hapa hapa na serikali itakusanya *tax* mara tano zaidi kuliko inayokusanya sasa.

La mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, *TVZ* kuna tatizo gani kuficha *impress rent* kwa miradi maalum ya Zanzibar ambayo ni *low risk*, kuna tatizo gani. Je, namuuliza Mhe. Waziri atakapokuja, je *BOT* imetubana kiasi hicho hata kwenye hii miradi midogo midogo hatuwezi kushusha ile *impress rent* kwa kuangalia ile miradi. Kila siku sisi tutakuwa tunawategemea wawekezaji wa nje na wakati wawekezaji wa ndani wapo kina Bakhressa wamezaliwa hapa hapa Unguja, kina Bakhressa leo wana bajeti kubwa kuliko Serikali ya Mapinduzi nzima ya Zanzibar. TV yake tu peke yake ni sawa sawa na wizara nne, *AZAM TV* aliyofungua kwa bajeti yake ni sawa sawa na wizara nne za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba wawekezaji wapo na wamezaliwa hapa hapa, hebu tuangalie hii miradi ambayo ni *low risk*, ipo miradi anaijua Mhe. Waziri. Vipi hawa hatuwezi kuwapunguzia *impress rent*, ili fedha zile za benki yetu na za wananchi wa Zanzibar *PBZ* ziweze kuzunguka zikaweza kuzalisha faida kubwa zaidi, itakuwa faida kwa benki na faida kwa serikali, na serikali watakuwa hawana haja ya kwenda *Exim Bank* China wala popote, watakuja kukopa hapa hapa kwenye benki yetu, kwa sababu benki yetu itakuwa na uwezo mkubwa wa kuwakopesha serikali.

Mhe. Mwenyekiti, vyenginevyo tukienda hivi basi kila siku sisi tutakuwa kwenye mikopo na madeni yetu yatakuwa yanaendelea kujaa na ku-*pile up*. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na *Inshaallah* nitaunga mkono hoja, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mahmoud Thabit Kombo kwa darasa zuri. Sasa nimpishe Mhe. Waziri wa Fedha aje afanye majumuisho. Mhe. Waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nianze kwa kutoa shukrani zangu za dhati, kwa Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia katika bajeti ya Wizara ya Fedha. Nataka niwathibitishie kwamba michango yao imekuwa muongozo mkubwa kwangu mimi binafsi na kwa watendaji wangu ambao wapo juu wamejaa tele. Kwa kuthibitisha tu asubuhi walionekana hawapo, bahati nzuri Wajumbe wa Baraza walikuwepo 21 na watendaji wangu walikuwepo 36.

Kwa hivyo, nakuthibitishia kwamba Wizara ya Fedha tupo macho, tunapokea michango ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi; hatuifanyii mchezo na wala hatuifanyii mzaha, tunaifanyia kazi. Wapo Wawakilishi ambao wapo karibu na mimi na wapo karibu na watendaji wangu wanaona juhudi zetu na wanaona mabadiliko na *Inshaallah* tutaendelea kufanya kazi nao kwa karibu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe waliochangia kwa maandishi ni Mjumbe mmoja, naomba nimtaje Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa na Wajumbe waliochangia kwa kusema ni 13, naomba niwataje kama kawaida yetu. Wa kwanza ni:

1. Mhe. Viwe Khamis Abdalla kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali
4. Mhe. Asha Bakari Makame
5. Mhe. Mohammed Haji Khalid
6. Mhe. Mgeni Hassan Juma
7. Mhe. Abdalla Mohammed Ali
8. Mhe. Fatma Mbarouk Said
9. Mhe. Marina Joel Thomas
10. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
11. Mhe. Panya Ali Abdalla
12. Mhe. Hamza Hassan Juma
13. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo

Hoja walizochangia Mhe. Mwenyekiti, nimezipanga na nimepata hoja katika mafungu 61. Muda ulionipa ni saa moja, nitajitahidi kama wanavyosema *manij-tahada wajada* na mimi nitajitahidi ili niweze kuwahi kwa muda.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya kwanza ilikuwa ni suala zima la usimamizi wa matumizi na mapato ya Serikali. Hili liliambatana na kuandaa mkakati maalumu wa kuongeza mapato yaani vyanzo vipya, vile vile na kuziba mianya; hoja hii imetolewa na Mhe. Viwe kwa niaba ya Kamati, Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Jaku Hashim Ayoub na Mhe. Panya Ali Abdalla.

Kwa ujumla nataka niseme kwamba hoja tumeipokea na lengo letu na juhudi zetu Waheshimiwa Wajumbe mmeziona tokea tumeingia mwaka 2010 mpaka leo umeona hatua kwa hatua tunazokwenda, lakini binaadamu ndio binaadamu, ukiziba huku anazibua huku sisi tutajitahidi kusimamia matumizi, tutajitahidi kusimamia mapato. Na kama Mhe. Panya alivyosema ametuonesha vyanzo vipya vya mapato, nataka nikuhakikishie kwamba baadhi ya vyanzo hivyo tayari tumeshaanza kuvifanyia kazi na tutaviingiza kama ni vyanzo vipya ili tuweze kupata mapato mengi zaidi.

Hoja ya pili ilikuwa ni suala zima la Afisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani hili lilitolewa na Mhe. Viwe kwa niaba ya Kamati. Nataka niseme tu kwamba hili suala lilikuwa halipo kabisa, halipo katika sheria zetu na hivi sasa nataka nilithibitishie Baraza lako Tukufu kwamba tunaifanyia marekebisho sheria ya fedha na tumeshaliongeza hili na *inshaallah* sheria hii itakapopitishwa ndani ya Baraza basi Afisi hii itaanzishwa.

Hoja ya tatu ilikuwa viwango vya pencheni havilingani na hali ya maisha. Nataka nikubaliane na Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia; Mhe. Viwe kwa niaba ya Kamati, Mhe. Asha Bakari na Waheshimiwa wengine nataka nilithibitishie Baraza lako Tukufu kwamba Serikali ikiongozwa na Dk. Ali Mohamed Shein; Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wametupa kazi hiyo sisi Wizara ya Fedha kuangalia hali gani katika bajeti ya mwakani tutakavyoweza kuinua viwango hivi vya pencheni, tunalifanya na tumeshaanza kulifanyia kazi.

Hoja nyengine ilikuwa kutoka kwa Kamati kuhakikisha ukamilishaji wa miradi ya *ZUSP* kwani *ZUSP* inaratibiwa na Wizara ya Fedha ni kweli na *ZUSP* kwa nini basi ikawa inaratibiwa na Wizara ya Fedha? Zilikuja kamati tunaita *mission team* kutoka *World Bank* wakati ule wakatembelea Manispaa; wakatembelea na Wizara iliyokuwa ikisimamia Manispaa, Tawala za Mikoa na Vikosi wakagundua kwamba kwa kweli mradi huu usimamizi wa kitaalamu hautakuwepo kwenye taasisi, ndio wakasema kama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mnataka dola milioni 38 tunakuombeni mradi huu usimamiwe na Wizara ya fedha. Sisi kama Serikali kama Wizara ya Fedha tukaona ni vyema pesa hizi zikapatikana, na ndio kwa maana tukachukua sisi dhamana ya kusimamia mradi huu.

Lilijitokeza suala kwa nini Wizara ya Fedha wanasimamia miradi mingi sisi huwa hatutaki kubeba majukumu, lakini pale tunapoona kwamba kuna haja ya kufanya hivyo inatubidi tufanye hivyo. Mradi huu una miradi minne midogo midogo ukarabati wa Jengo la Manispaa, ambao sasa hivi tunaliona pale linaendelea, ujenzi wa mitaro ambayo sampuli imeshakamilika na imeshapelekwa *World Bank* tunasubiri majibu kutoka kwao, uwekaji wa taa za barabarani nayo vile vile sampuli tayari tumeshapeleka *World Bank* tunasubiri *No Objection* na vile vile ukuta wa Forodhani nao tunasubiri *No Objection.*

Tukishapata *No Objection* hizi kutoka *World Bank* miradi hii kwa pamoja itaanza kufanya kazi, na naomba tumesubiri sana na sisi tunaendelea kuwasukuma wenzetu ili waweze kutoa *No Objection* kwa wakati tuweze kuanza hizo shughuli.

Limekuja suala la mafunzo kuhusu *PBB* katika kudhibiti matumizi ya Serikali Mhe. Viwe kwa niaba ya Kamati na Mhe. Mgeni Hassan na nadhani na Waheshimiwa wengine ni kweli nakubaliana na nyinyi tutafanya mafunzo haya kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ili kila mmoja aweze kuelewa, *PBB* itatusaidiaje katika kudhibiti matumizi ya Serikali mafunzo hayo tutayafanya tukianza na Baraza la Mapinduzi, baadae tutakuja kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na watendaji wengine wote.

Mhe. Mgeni Hassan na Mhe. Viwe na wengine walioona hili limejitokeza kwamba majina ya vifungu na matumizi yake kuna mapungufu. Tumelipokea na tayari tumeshatoa maelekezo kwa Kamishna wa Bajeti kwamba baada ya kumalizika kwa bajeti yetu hii wapitie vifungu vyetu vyote na matumizi yake ili tuweze kwenda sambamba katika bajeti ijayo tuwe tuna vifungu ambavyo vitaweza kufahamika pamoja na matumizi yake.

Urasimu ndani ya Taasisi za Serikali unazorotesha uwekezaji. Mhe. Viwe kwa niaba ya Kamati na Waheshimiwa wengine wamelieleza hili tumelipokea. Mhe. Jaku alisema kwamba *ZIPA* hawana urasimu, urasimu upo katika taasisi nyengine za Serikali na akasema hasa ardhi, Serikali tupo tutalipokea na tutalifanyia kazi kwa pamoja tuweze kuondosha huu urasimu ili kutoa nafasi kwa wawekezaji waweze kuwekeza basi kwa wakati.

Uendelezaji wa maeneo huru na kuwaelimisha wananchi juu ya dhana nzima ya maeneo huru. Nia ipo Mhe. Viwe Khamis, Mhe. Makame Mshimba, Mhe. Asha Bakari na Waheshimiwa wengine nia ya kuendeleza maeneo huru ipo, na tumekubaliana kwamba tutaanza kuyaendeleza kwa awamu na katika bajeti inayokuja tumekusudia kuanza kuyaendeleza kwa kuyawekea sehemu kwa sehemu ya miundombinu.

Wafanyabiashara kulipa kodi kwa wakati Mhe. Viwe, Mhe. Makame Mshimba, Mhe. Raza na Waheshimiwa wengine wote nasema kwamba hii ndiyo sheria. Sheria inawataka wafanyabiashara walipe kodi kwa wakati stahiki, vyenginevyo kuna adhabu na nitawaona sana ndugu zangu wa *ZRB* kama kutakuwa kuna mfanyabiashara amechelewa kulipa kodi kwa wakati basi watumie nafasi ya sheria kuwaadhibu kwa kuwalipisha *penalt*, hii itawasaidia sana kuweza kuwashtua, maana yake tumekuwa tukishtua mara kwa mara hasa katika siku za walipa kodi.

Mimi binafsi nilikuwa nawasisitiza wafanyabiashara walipe kodi kwa wakati, lakini wafanyabiashara baadhi yetu wengine ni masugu lazima tukubali, kwa hivyo lazima twende sambamba na Sheria hili tutalilisimamia.

Mashine za utozaji wa risiti kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali. Nataka niseme Mhe. Viwe, Mhe. Asha Bakari, Mhe. Mohammed Ali *process* imeshaanza katika bajeti, kama mtakumbuka nilisema kwamba mashine hizi zitanunuliwa na Wizara ya Biashara kwa thamani ya shilingi bilioni 2.5, tayari *process* imeshaanza, tumeunda Kamati ya pamoja, na baada ya *process* hiyo tutatoa tangazo la wale ambao wanataka kuchukua tenda wachukue tena ili watuletee mashine hizo kulingana na *specification* ambazo tutakazotoa.

Lengo letu tunataka mwakani ukianza, na nataka niwaambie wafanyabiashara kwamba yeyote atakayekuwa hatumii mashine hizi na ametakiwa kutumia basi atakuwa anafanya kosa na itabidi aadhibiwe kwa mujibu wa sheria.

PBZ kuongezewa mtaji tumefikia wapi Mhe. Viwe, Mhe. Mshimba na Mhe. Jaku na wengine, nataka niseme tu tumeanza *process* ya mazungumzo. *PBZ* wana pesa zao, ni za Serikali kwa kweli wanazozipata kutokana na faida wanayoipata kila mwaka, safari hii wamepata zaidi ya bilioni saba, na gawio ni dogo sana gawio milioni 440 au 500 tu hiyo ndio gawio ambalo linakwenda Serikalini katika kuchangia bajeti ya Serikali. Tunachotaka ni kwamba *PBZ* zile faida ambazo wanazipata kwanza wafikirie kuingiza tena kama kujaliza mtaji, lakini tunafanya mazungumzo, tumeshakaa vikao viwili na hivi punde tu tulikuwa tufanye kikao bahati nzuri Katibu wao na *MD* wakawa hali zao si nzuri, kwa hivyo kikao nimekiahirisha mpaka tumalize bajeti. Tutafanya muendelezo kuweza kuona jinsi tunaweza tukai- *capitalize PBZ* kwa msingi huu ambao waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi, lakini na wao wenyewe wafikirie faida yao kuirudisha tena kama ni mtaji ndani ya mtaji walionao.

Elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa uwekaji wa Bima mali zao. Mhe. Viwe kupitia Kamati na Waheshimiwa wengine kweli hili ni jambo zuri sana kwa sababu wananchi wengi tunalidharau, lakini unapokuja kupata ajali ndio unapofikiria sasa ningekuwa nina Bima basi sasa hivi Bima ndio angekuwa muokozi wangu, unaweza kukuta wengi wa Wawakilishi tuliomo humu ndani nikikuulizeni nani ameitilia bima nyumba yake pengine unaweza kupata labda wawili au watatu, lakini unapokuja kupata ajali ya kuunguliwa na nyumba umeshaijenga kwa milioni mia mbili pale mzee huna kitu zaidi ya jivu tu utakalokuwa nalo, lakini unaweza kuweka thamani ya nyumba yako kila mwaka ukalipa laki tano tu Bima ile inaweza kukuokoa pale unapopata majanga pamoja na Bima nyengine. Kwa hivyo elimu ni muhimu, tumelipokea Mhe. Viwe na Waheshimiwa wengine tutalifanyia kazi.

Uhakiki mali kuwa na nguvu na kupatiwa nyenzo tumelipokea Mhe. Viwe, Mhe. Mshimba Idara yetu ya Uhakiki Mali tutaipatia nyenzo za kutosha, tumewatengea pesa kwa ajili ya kununua pikipiki saba ili wataalamu wao waweze kufika kule ambako wanatakiwa kwenda kuhakiki mali.

Waheshimiwa wengi sana Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, Mhe. Asha Bakari, Mhe. Mohammed Ali naelewa na Waheshimiwa wengine mnataka kujua lini meli yetu itakuja na itawasili Zanzibar, meli mpya inayotengenezwa, nataka niseme kama ifuatavyo.

Meli hii tumeijenga kwa dola milioni 30.6 sawa sawa na Bilioni 50 za Kitanzania, meli hii *Capacity* yake ni abiria 1,200 na itachukua mzigo wa tani 200. Meli hii inalipwa kwa *installment* tano, kila *installment* tunalipa dola milioni 6.12, tayari tumeshalipa *installment* mbili bado *installment* tatu.

Meli hii inatarajiwa kumalizika na kuanza kuondoka wenyewe kutoka Korea ya Kusini Mwezi wa Februari mwaka 2015 na itakuja wenyewe mpaka Zanzibar na itawasili Zanzibar kama mambo hayatabadilika mwezi wa Aprili, tunatarajia kuipokea meli yetu mwaka 2015, tumuombe mungu sote tuwe hai tuipokee meli yetu na jina la Meli ni *MV Mapinduzi Zanzibar* (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti wengi wametaka kuelewa kadhia ya makontena na wengi wametaka kujua je wafanyabiashara wetu watakapokwenda Tanzania Bara hawatapata usumbufu tena.

Mhe. Makame Mshimba, Mhe. Mahmoud Mussa, Mhe. Raza, Mhe. Mohammed Ali, Mhe. Hamza Hassan na Waheshimiwa wengine, nataka niseme tu ile haikuwa kadhia ilikuwa ni kukosa taratibu za utendaji, kama kungefuatwa taratibu za utendaji basi nadhani lile suala lingekuwa halipo. Wale vijana ambao wamekuja tumeshawarudisha tumewaambia kwa sababu taratibu zimekosewa na tumewataka *TRA* Zanzibar waendelee na kazi ile na wanaendelea nayo.

Mhe. Viwe Khamis, Mhe. Makame Mshimba, Mhe. Fatma Mbarouk, Mhe. Marina Joel, Mhe. Panya Ali na Mhe. Hamza Hassan wametaka kuelewa barabara mbovu mfuko wa barabara fedha zipo inakuwaje. Barabara zifanyiwe matengenezo haraka ili athari isiwe kubwa, uchakavu wa vifaa, mfuko ununue vifaa vya ujenzi. Nataka niseme kama ifuatavyo; Mfuko wa Barabara haujengi barabara mfuko wa barabara unasimamia pesa kwa ajili ya ujenzi wa barabara, ujenzi wa barabara unajengwa na Idara ya Barabara, tatizo liliopo kwenye Idara ya Barabara limeelezwa idara ile ina vifaa chakavu na tayari tumeshapata orodha ya vifaa ambavyo wanavyovihitajia na tayari Serikali imeshatoa idhini tuwatafutie vifaa hivyo vyenye thamani ya dola milioni 7.

Wizara yangu inafanya kazi hiyo sasa hivi ili kuiwezesha Idara ile kuwa na vifaa zaidi ili kuweza kutekeleza majukumu yao, fedha za kutengeneza barabara zipo lakini Idara ya barabara inashindwa kwa sababu ya uchache wa vifaa na uchakavu wa vifaa vyao, lakini mfuko wa barabara vile vile umetenga fedha kidogo kwa ajili ya kukarabati vifaa vile vya Idara ya barabara, kwa hivyo hatua hizo zote tunakwenda nazo pamoja na sasa hivi tumewataka wenzetu wa Idara ya barabara watoe tenda kwa taasisi nyengine ili kuharakisha utengenezaji wa hizi barabara, ambapo fedha zilizopo ziweze kutumika, nimesoma hapa kiasi gani cha fedha bado zipo chini ya Mfuko wa Barabara.

Mhe. Makame Mshimba umesema kwamba kuna haja ya Semina ya kuelimisha shughuli mbali mbali zinazotekelezwa na *ZIPA.* Mimi nakubaliana na wewe kabisa, lazima tuifahamu *ZIPA* inafanya shughuli gani hasa kwetu sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, tutafanya hivyo Mungu akitujaalia, tutatafuta pesa chini ya idara ya *ZIPA* ili tuweze kupata mafunzo hayo na tuweze kuelewa wenzetu hawa wanafanya nini na wanatafuta nini na wanapata nini kila mwaka.

Mhe. Makame Mshimba, Mhe. Mohammed Haji Khalid, na Mhe. Jaku Hashim *ZSSF* iwakopeshe wanachama wake na wale watakaomaliza ajira zao walipwe mafao yao ili wajiendeleze, wawaangalie wateja wao kuwapatia mikopo.

Nasema hivi Mhe. Mwenyekiti, tulikotoka siko tuliko, tumetoka mbali sana na *ZSSF*, sasa hivi *ZSSF* imekua sasa hivi *ZSSF* sheria yake ile imepitwa na wakati wameanza kutoa mapendekezo tumeshaifanyia marekebisho wizarani pale, sasa hivi ipo kwa Makatibu Wakuu, itatoa nafasi hiyo aidha kuwakopesha au kuchukua dhamana ya mkopo kwa wanachama wake na vile vile inaangalia jinsi gani ya kuweza kutumia sehemu ya fedha za *ZSSF* sio fedha za kutumiwa kama benki, fedha hizi ni kwa ajili ya kukusaidia wewe wakati unapozeeka.

Kwa hivyo ZSSF inaangalia kama utakosa ajira kwa kipindi inaangalia kuweza kukuwezesha sehemu ya mafao uliyoweka ili iweze kukusaidia sio yote, kwa hivyo tunachokisukuma sasa hivi Kamati ya Makatibu Wakuu itakapokuwa, halafu mutuidhinishie tuweze kuitekeleza hiyo watakuwa wanawachukulia dhamana. *ZSSF* itachukua dhamana kupitia Mabenki, wewe mwanachama wao utachukua mkopo wa benki utajenga nyumba yako, utachukua mkopo wa gari, utanunua gari yako wao watakuchukulia dhamana.

Kuanzishwa Benki ya akinamama tumefikia wapi, Mhe. Makame Mshimba suala hili nimelieleza hata katika bajeti yangu shemeji yangu utakuwa unanionea kila siku nikisimama unaniuliza benki ya akinamama.

Nakubaliana na wewe kuna umuhimu wa kuanzishwa benki ya akinamama lakini nataka nikwambieni Waheshimiwa Wajumbe hili litakuwa jina tu, maana yake kuna dhana kwamba tukianzisha Benki ya akinamama mikopo hii itakuwa asilimia moja, asilimia mbili riba hii itakuwa ni jina tu haitakuwa tofauti na benki nyengine za kibiashara, *the interest rate* zinakuwa *governed* na Benki Kuu, haitakuwa tofauti na benki nyengine, mtakuwa mna jina wanawake mna benki yetu, lakini wanaume tutakuwemo ndani tutaruhusiwa kuweka fedha zetu humo ndani, tutaruhusiwa wanaume kukopa humo ndani, kwa hivyo hili litakuwa jina tu. Kwa wakati huu lakini kama nilivyosema katika majumuisho ya bajeti ya taifa kwamba tumeanza mchakato huu bahati mbaya Katibu Mkuu tuliyeanza naye amehamishiwa Wizara nyengine, Katibu Mkuu aliyekuja ni mpya lakini tayari tumeshaandaa mkakati na Katibu Mkuu mpya kwamba ana- *go through* zile *files* zote na *minutes* zote, tukimaliza kikao chetu cha bajeti tutaandaa kikao chetu cha pamoja kuendeleza hili, na tumeshakubaliana kwamba tutachukua zile *SACOSS* zilizoko na wanawake na wanaume, wanaotaka kununua *shares* katika benki hii wataruhusiwa, sio wanawake peke yao.

Mimi nina *shares* katika benki ya Wanawake wa Tanzania, kwa hivyo na benki hii ya wanawake nayo nitanunua *shares*.

Kwa hivyo tusubirini kidogo maana yake kujenga benki ni *process* ya miaka sio miezi, hata ile Benki ya wanawake wa Tanzania imechukua zaidi ya miaka mitano, kwa hivyo sisi tuachieni, tupeni nafasi hii tutafikia pahala pazuri tutaanza kutoa nafasi kwa wanaotaka kununua *shares* halafu tuikuze benki yetu hii.

Kama nilivyoeleza kitika kikao cha majumuisho tusingependa tuanzie na benki, tutaanzia na *community bank* ya wanawake, kwa sababu mtaji wa *community bank* ni mdogo kuanzia ukilinganisha na mtaji wa kuanzia na benki kamili, kwa hivyo tutaanza hiyo halafu tutaikuza wenyewe baadae itakuwa.

Mhe. Jaku Hashim na Mhe. Mohammedraza mmezungumzia sana kuhusu habari ya msamaha wa bidhaa na usimamizi mzuri ili wafaidike walengwa. Hili tumeshazungumza na Mhe. Waziri wa Biashara na kesho ni tarehe 27 ule msamaha tulioutoa unamalizika wa Mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Tumekubaliana na watu wa *TRA* watuletee makampuni yote ambayo yamefaidika na misamaha na bidhaa ambazo wamezileta, hivi sasa tumeshachukua bei kwenye soko ni kiasi gani Mhe. Mazrui na timu yake watafuata mpaka kwa mlaji tuweze kuona, na mfanyabiashara yeyote ambaye itakuwa hajakidhi vigezo hivi msahama ule tutamuandikia aurejeshe, huu msamaha lazima uende kwa walengwa katika mwezi mtukufu wa Ramadhani, nimeshakubaliana na mwenzangu Mhe. Mazrui tutaifanya kazi hiyo kwa nguvu zetu zote katika kipindi hiki cha mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Ushauri unaotolewa na Baraza la Wawakilishi. Anatushukuru sana Mhe. Asha Bakari kwamba Wizara yangu inalifanyia kazi, na nataka nikuhakikishieni Waheshimiwa nyote kwamba sina sababu kwa nini tusiufanyie kazi.

Tutaendelea kuifanyia kazi na pale ambapo mtakapoona bado hatujafanyia kazi kama mfano Mhe. Hamza, Mhe. Hamza kila wakati ananikumbusha na anajua fika kama tuna kazi mimi na yeye lakini ananikumbusha, basi mpaka tutakapokamilisha najua atakuwa hanikumbushi tena. Na nyinyi msione tabu kutukumbusha, lengo letu ni kufanya kazi kwa kushirikiana na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao ni waajiriwa wa wananchi.

Mhe. Asha Bakari vile vile amesema suala la vifaa chakavu vilivyoko katika mawizara viuzwe, pamoja na magari ili kuweka mazingira mazuri katika maofisi yetu. Zoezi limeshaanza, tumeviorodhesha vifaa chakavu katika mawizara yote, zoezi la kuuza vifaa chakavu, ukisikiliza Redio Zanzibar tunatoa matangazo, huwa tunafanya zoezi la kuuza vifaa chakavu siku ya Jumamosi. Tumeshauza vya Wizara ya Kilimo, tumeshauza vya Wizara ya Fedha, tena kwa mnada. Tumeshauza vya Ofisi ya Rais Ikulu, tumeshauza vya Wizara ya Ardhi na tumeshauza vya Manispaa kwa mnada. Ukifika pale una nguvu unaingia unanunua. Kwa hivyo hilo zoezi litaendelea mpaka tumalize Wizara zote na Serikali nzima.

Serikali imetoa muongozo na mimi nimeuafiki muongozo huo ni mzuri tumepewa Wizara ya Fedha, kwamba fedha zote za magari tutakazouza magari chakavu tununulie magari mapya. Halafu tuyagawe kwenye taasisi ambazo hawana magari. Na wale ambao tuliouza matrekta yao na vyombo vizito tuangalie kama zinatosha na wao tuwanunulie trekta zao tuwarejeshee trekta zao. Kwa hivyo hilo zoezi muongozo mzuri wameshatupa serikali na leo nimekaa na wataalamu wangu tumekubaliana kwamba; Kamishna wangu ameweka orodha kiasi gani tumeshavuna mpaka sasa hivi katika zoezi hili ili baadae tuanze kufanya zoezi la kununua magari mengine.

Mhe. Asha Bakari amesema Serikali itumie uwezo wa taasisi zetu katika kudhibiti matumizi ya seriakali hasa kutumia kumbi zetu. Ujenzi mdogo mdogo kutumia taasisi zetu vikosi vyetu, *furniture* kuitumia *Trade School*, magari kupelekwa karakana za SMZ wazo ni zuri. Nasema tena wazo ni zuri lakini kuna matatizo ya msingi lazima na haya tuwe tunayaangalia.
Kwanza kuna ufanisi, lakini la pili kuna udokozi lazima na hayo tuweze kuyaangalia. Hatutaki tumshutumu mtu au taasisi gani ina udokozi, lakini haya kwa ujumla wake lazima tuweze kuyaangalia.

La tatu, unapopeleka kwenye taasisi za serikali ni sawa lakini mzunguko wa uchumi unakuwa haupo, ukipeleka katika taasisi za serikali mzunguko haupo na kama mzunguko wa kiuchumi haupo kodi huna. Kwa hivyo haya yote tunayaangalia kwa ujumla wake, hatusemi kwamba tutapeleka lakini tunasema sisi kama ni serikali tunatakiwa tufanye na taasisi za serikali na taasisi za sekta binafsi ili mzunguko wa kiuchumi uwepo na kodi iweze kupatikana. Kwa hivyo tumelichukua hilo wazo na tunalifanyia kazi.

Mhe. Mohammed Haji Khalid amezungumza *very interesting story* hapa. Katika Idara za Wizara ya Fedha hakuna hata Idara moja iliyopata chini ya asilimia 70 akasema tena kwa Kiingereza *charity begins at home*. Na mimi nakubaliana naye kwamba *charity begins at home*, lakini kuna sababu za msingi Waheshimiwa wengi mmesema hapa kwamba Wizara ya Fedha ni moyo ukiutoa moyo mwili hauendi, lakini nikitoa mkono mwili unafanya kazi, nikiondoa mguu mwili unafanya kazi, lakini jamani nataka muangalie hizi pesa zote ambazo mulizoipa Wizara ya Fedha sio zote ambazo zinatumiwa na Wizara ya Fedha, hizi nyengine tunatumia serikali nzima.

Nitataja mfano tu, kwanza marekebisho ya mshahara bilioni 17 sikutumia mimi tumezitumia sote serikali nzima. Risiti tulizochapisha kwa ajili ya kutafutia mapato sikuzitumia mimi, hizi tumetumia sote serikali nzima. Nimeeleza nimemnunulia Mdhibiti kompyuta kwa ajili ya serikali yetu nzima, kuna mambo mengi humu ndani, lakini ninachotaka kukisema chengine ni kwamba tumelinganisha vilinganisho tofauti. Mimi Wizara ya Fedha ninapokuja hapa ninakuja na bajeti ya kutekeleza miezi 11, Wizara nyengine imekuja na bajeti iliyotekelezwa miezi 9 nitakupeni mfano mmoja tu.

Wizara ya Afya, Mhe. Jaku Hashim Ayoub amehoji sana Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu, sina *data* za Wizara ya Elimu lakini sura itaonekana kama hiyo ya Wizara ya Afya. Wizara ya Afya walipokuja na bajeti yao ilikuwa wamekuja na bajeti ya kutekeleza miezi 9. Na bajeti yao ya *OC* Wizara ya Afya ilikuwa ni 5.7 *billions*. Miezi 9 ya utekelezaji wamepatiwa karibu bilioni 3.7 lakini leo hii Wizara ya Afya wamepatiwa zaidi ya bilioni sita tayari, zaidi ya bajeti yao wameshapatiwa ya *OC*. Kwa hivyo tunapolinganisha tunalinganisha vipindi tofauti.

Mimi nimekuja na bajeti ya miezi 11, wale wengine wamekuja na bajeti ya miezi 9, 9. Labda pengine Mzee Rama sijui kama na yeye kaja na bajeti ya miezi 11, kama kaja nayo miezi 11 labda mimi na Mzee Rama tutakuwa tumekuja na bajeti ya miezi 11. Sasa tunapolinganisha tulinganishe vipindi sawia, na ndio kwa maana kwamba mimi

za kwangu umekuta zimetononeka, pengine na wengine sasa hivi ukizitafuta utakuta pengine zimeshatononeka. Ile 25, 30, tuliyokuwa tunazungumza pengine sasa hivi imeshakuwa kubwa, lakini mawazo yenu Waheshimiwa Wajumbe tumeyapokea na kila uchumi wetu, mapato yetu, yatakapokua tutahakikisha kwamba taasisi zetu zote zinapata fedha kwa wakati na fedha za kutosha.

ZIPA kuchukua muda mrefu hadi kutoa kibali kwa wawekezaji cha kuwekeza. Tumelipokea na tutajaribu kuzungumza nao sana, ingawa Mhe. Jaku naye amelizungumza kwamba wanaoodhoofisha ni taasisi nyengine sio *ZIPA*, tutaliangalia kwa ujumla wake kama serikali.

Mhe. Mgeni umeeleza kwamba kuwa na *centre of exellency,* tumelipokea lakini tunasema tulifanyie kazi zaidi ili tuweze kuona na tutakushirikisha katika kutupatia mawazo yako ili tuweze kuona kwamba twende vipi katika suala hili. Suala tumeliona ni zuri lakini tulifanyie kazi zaidi ili tutakapokwenda tuwe tuna uhakika tunakwenda kwa mwendo gani.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali amezungumzia Shirika la Magari litafungwa lini. Nataka nimwambie Shirika la Magari limeshafungwa, Mhe. Rais ameshatoa *dessolution order* kwa mujibu wa Sheria na tayari Mhe. Rais ameshaunda Kamati ya Kusimamia Mali zote zile za mashirika haya mawili; Shirika la Magari na Shirika la Utalii, hili limeshafungwa. Na hapo hapo nataka niseme, wafanyakazi wote wa Shirika la Utalii tayari tumeshawapangia mawizara, wafanyakazi wa Shirika la Magari tayari sasa hivi wako katika zoezi la kupangiwa na wote wataendelea na kazi utumishi wao mpaka watakapofikia umri wao wa kustaafu.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa amesema sababu za msingi za kukua deni letu la Taifa. Nimesema katika bajeti yetu, kopa leo ujenge miundombinu leo, wiki iliyopita tu nimepokea barua kutoka *Exim Bank* ya China mfano mdogo tu ninakupeni wanasema kwamba *interest rate* yake sasa hivi itakuwa ni 2% badala ya 1%. Tumeshindwa kukopa jana ilipokuwa 1% tunakopa leo 2% na Bandari yetu mpya tunayotaka kujenga imeshaingia katika 2%. Kwa hivyo *cost* zinapanda, tukope leo, tusiogope kukopa leo, na sisi tunakopa hii sehemu kubwa ya madeni ni kwa ajili ya miradi yetu ya maendeleo. Na sisi tutaendelea kukopa, madhali *ratio* zetu zinaturuhusu kukopa tuendelee kukopa na wala tusiogope kukopa, madhali unalipa desturi basi.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa ameuliza katika masuala yake *who are away* kusaidia *E- Tax* sisi hatukatai kila anayetaka kutusaidia na aje, lakini unatusaidiaje, unatusaidia kwa kupiga mayowe nje, kuna utaratibu ndani ya serikali katika kuisaidia serikali *officially we have to write a letter*, lazima ueleze unataka kufanya nini ndani ya serikali, halafu hao wanaohusika nao wanakujibu mnakaa pamoja, mnaelekezana. Mimi ninawakaribisha na waje tu, kama watakosa *E-Tax* ziko E nyengine nyingi tu. *E-Education* bado, *E-Justice* bado, *E-Culture* bado, kuna E nyingi tu zipo hapo, kwa hivyo wache waje.

Mhe. Fatma Mbarouk ulitaka kujua fedha za ruzuku na mikopo zimemsaidiaje mwanamke. Hizi ni fedha ambazo zinakwenda moja kwa moja katika miradi ya maendeleo. Mimi ninasema *with due respect* zinamsaidia sana mwanamke kuliko hata mwanamme. Kwa mfano tukipeleka pesa katika maji, tunaelewa *culture* za Kiafrika mwanamke ndiye anayekwenda kuchota maji, ukipata maji mwanamke umeshamsaidia badala ya kwenda kuchota maji, bomba liko jirani pale, *culture* zetu tunazielewa. Mwanamke ndiye mkulima, ukijenga barabara anakuwa na *access to the market* anapata pesa nyingi zaidi. Kwa hivyo zimemsaidia sana mwanamke hizi pesa na wala usitaharuki, pesa hizi zinamsaidia na tutaendelea miradi tutakayoielekeza ni ile ambayo mwanamke inamsaidia.

Mhe. Fatma Mbarouk ametaka kuelewa kirefu cha MPAMITA, Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania. Unajua Watanzania sisi tunapenda sana kufupisha fupisha mambo, sijui MKUKUBI, MKUKUTA, MKUZA na hii MPAMITA.

Mhe. Fatma vile vile ametaka kujua Shirika la Magari bado linaweza kujiendesha kwa faida. Hapa nataka niseme Mhe. Fatma, nataka uunge mkono kwa sababu tayari *order* ya *dessolution* imeshatolewa na Mhe. Rais. Shirika lolote lile kama linatumia milioni 50 likatengeneza faida ya milioni tano hilo sio Shirika, lazima liondoke. Shirika lolote lile ambalo haliwezi tena kushindana ndani ya soko lazima litakufa tu. Shirika la Magari limekufa, sasa hivi pale alikuwa anaweka baiskeli za watu, vyarahani vya watu, yeye mwenyewe nyenzo za kununua hana, tumeliachia liondoke.

Shirika la Utalii halikadhalika *private sector* ime-*take lead* sasa hivi katika kuleta watalii, kwa hivyo yeye tumemwambia ondoka, *after all, we; the government* hatuhitaji kufanya biashara. Sisi ni *facilitator*, tunatakiwa ku-*facilitate* na ku-*regulate private sector* iweze kufanya biashara. Wewe ukifanya kila kitu uuze malai, uuze sijui nini *private sector* itafanya kazi gani. Mimi nimefurahishwa sana na uamuzi wa serikali kwamba Mashirika haya 2 kuyafunga ili sekta binafsi kuchukua nafasi. Na wanafanya vizuri sekta binafsi ukiziangalia zinafanya vizuri sana. Kwa hivyo tuwapongeze, hali yetu ni nzuri.

Mhe. Fatma Mbarouk ameuliza ni kiasi gani majengo ya Ofisi yamezingatia watu wenye ulemavu. Unajua kuna mambo mengine Mhe. Mwenyekiti, ukijibiwa hapa, hapa nikikujibu hupati ule utamu na ladha uende kwenye yale majengo. Mimi nimetembelea jengo moja ambalo ni la Ofisi jipya tumeshalifungua jengo la Mwanasheria Mkuu, ukiingia mule ndani hata uwe na ulemavu wa kiasi gani kuna sehemu ya kupandia wale walemavu halafu ndani kuna *lift* unakwenda juu na *lift* wamejitahidi sana, na hivyo hivyo jengo la Katiba. Tumetoa maelekezo kupitia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban yupo, hawa ndio wasimamizi wakuu wa majengo ya serikali wanahakikisha kwamba linakua na *facilities* zote kwa ajili ya ndugu zetu walemavu.

Hata ukienda Chuo chetu Dakhalia Chuo cha Chwaka, nenda kaingalie Dakhalia ya Chuo cha Chwaka mimi nimekwenda, kuna vyoo vya walemavu, wamejitahidi sana, sasa hivi tumebadilika kwa sababu gani, walemavu ni watoto wetu, ndugu zetu, kaka zetu, baba zetu, dada zetu kwa nini na wao tusiwape *access* ya kuingia katika majengo ya serikali. Kwa hivyo hilo tumelifanya vizuri sana, na ninapenda na wewe ungetembelea ukaona mwenyewe, *seeing is believing;* kuona ni kuamini.

Mhe. Marina Joel Thomas, sababu za kupelekea *ZIFA* kuchanganywa na *SUZA*, kuna ripoti kubwa sana. Hivi vyuo vilifanyiwa ripoti wakati huo Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban alikuwa Waziri wa Elimu. Kuna Kamati iliundwa ikatembea Chuo kimoja kimoja lakini sababu ya msingi tulitaka kuikuza zaidi ili University yetu iwe ni imara zaidi. Chuo Kikuu imara lakini *concern* hii ya *ZIFA* kuunganishwa na Chuo Kikuu nadhani imesikika sana na sasa hivi tunasubiri maelekezo zaidi kutoka serikalini. Bado Chuo kile tunacho sisi hatujashindwa kukilea, lakini tunasubiri muongozo hata kama kitachukuliwa na Chuo Kikuu kiende vipi. Unaweza ukachukuliwa na Chuo Kikuu ukawa chini ya *umbrella* ya Chuo lakini *you are independent* kwa mambo yako mwenyewe ya kufanya kazi. Kwa hivyo bado tunasubiri maelekezo zaidi, lakini na mimi ninakubaliana na wewe hichi Chuo kimefanya kazi nzuri na kinaendelea vizuri.

Mhe. Viwe, Mhe. Marina mawakala wa Bima malipo yao yanachelewa, nimeongea na mawakala, kila nikizunguka Mikoani mimi ninakutana na mawakala wa Bima na ninawasikiliza sana, hili ni moja ya tatizo lao wanalolalamikia. Bahati nzuri tumetangaza Bodi ya Bima juzi tu, Bodi tutaizindua siku ya tarehe 5 na nimeshawambia wenzangu kwamba moja ambayo nitayozungumza ni yale malalamiko ambayo nataka niwape *challenge* Bodi mpya ili yaweze kuyasimamia. Kwa hivyo tumelipokea na tutalifanyia kazi.

Umeeleza kwamba ni sababu gani zinazopelekea Mashirika ya Umma kabisa nimezieleza kwa mfano hayo Mashirika yetu mawili. Fedha ziingizwe kwa wakati Mawizarani ili waweze kutekeleza majukumu yao, hiyo ndio *interest* yetu sisi Wizara ya Fedha na serikali nzima, lakini nimeeleza kwamba tatizo kubwa tulilonalo sisi tunakwenda na *cash budget*, unakusanya, unagawa.

Kwa hivyo tutakapofanikisha kuwa na bajeti yenye fedha ambazo kulingana na mahitaji yetu nadhani kutakuwa hakuna matatizo, lakini sasa hivi tunajitahidi sana tuviingize kwa wakati, tutakapochelewa wenzetu wanatustahmilia hivyo hivyo tunakwenda kulingana na hali yetu.

Mhe. Jaku suala lako la Wizara ya Afya nimeshalijibu vile vile.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri una nusu saa ya kumalizia.

Mhe. Waziri wa Fedha: Sawa nitajitahidi nitakaoshindwa tena itabidi niwasikilize baadae. Mhe. Jaku gawio waachiwe *PBZ* nimelieleza sio kubwa sana kulingana na mapato yao faida wanayoipata.

Mhe. Panya ukaguzi wa matumizi ya serikali ufanywe kwa wakati ninakubaliana na wewe kabisa na tutawasisitiza wenzetu wahasibu pamoja na ma-*auditors* waweze kukagua hesabu zao na kufunga kwa wakati.

ZIPA iwe makini na wawekezaji wale ambao wajanja wajanja wale, hili nadhani *ZIPA* wameshapata *experience* ya kutosha sasa watalisimamia, kwa sababu kuna wawekezaji wajanja wajanja lakini na sisi tunataka kuwafunga katika baadhi ya sheria zetu ili watakapoondoka wasiwaachie madeni.

Mhe. Panya umezungumzia kufungua benki *airport* ili fedha za *visa* kuingia moja kwa moja, tayari ukienda sasa unakuta watu wanafunga vifaa pale na tunatarajia wakati wowote katika mwezi wa Julai watakuwa wanapeleka moja kwa moja kutakuwa hakuna matatizo. Kuna vifaa ya *POS* pale vitakuwepo na mtu anakwenda na *visa card* yake tu aliyekuwa hana *visa card* yule ndiye atakayelipa fedha taslim.

Shirika la *ZBC* lisaidiwe Mhe. Hamza swahibu yangu, nimelipokea na umenitaka hapa niwambie *ZRB* wakae na waingizaji wa mafuta wenye vituo, nimelipokea na nitawataka wafanye hivyo. Suala *East Africa* malipo yao hili ni jipya kwetu lakini tutalifuatilia. Nimewasiliana na wenzangu watendaji wakuu wanasema hili kwetu ni jipya na siku zote sisi tunataka mapato yaje tu tuwagaie watu wetu, lakini tunalifuatilia kule Dar es Salaam kuna kitengo kuna Mkuu Maalum kule kazi yake amepewa hili.

Muwekezaji wa chelezo usizuie shilingi yangu kwenye chelezo, nakuomba tutafanya kikao kama nilivyokwambia na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati tumeshakubaliana tunamaliza hapa tutakaa mimi na yeye tuone tuna mambo 2 tutayaongelea; Moja ya kule Paje na la pili tunazungumza hili la chelezo mimi na Mhe. Waziri wa Ardhi, tukijumuisha na watendaji wetu; Mipango miji, Mkurugenzi wa Ardhi na *ZIPA* tuone tunakwama wapi.

Wakati mwengine tunakwama kwa sababu tunazungumza mmoja mmoja, kila mmoja anazungumza peke yake mtakwama. Kwa hivyo tutalifanya tushakubaliana na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Watendaji wa *procurement* acha niwaangalie na hili nimelipokea. Wawekezaji wazalendo masharti yao yako vipi. Masharti ni yale yale yaliyomo katika sheria ya *investment*, isipokuwa huyu kidogo mzalendo anaweza akaanza kuwekeza hata kwa kiwango kidogo tu, sio lazima awe kiwango kikubwa. Kwa hivyo, wache waje tuta-*facilitate*, tutawapa nafasi na wao waweze kuwekeza.

Mhe. Mwenyekiti, hayo madeni ya vikosi yameshakuja ndani ya ofisi yetu tunayafanyia kazi.

Bima kwa nini wametumia asilimia 40 Mhe. Hamza Hassan Juma anauliza, walipanga fedha nyingi lakini wametumia asilimia 40 tu za maendeleo. Ni kweli walipanga kujenga na ofisi yao Pemba lakini kiwanja walichopewa baada ya kufanyiwa *soil test* wakagundua kina matatizo na wakahofia kwamba isije ikawa ni tatizo kama lile ambalo tulilolipata sisi. Kwa hivyo, sasa hivi wataendelea na ujenzi wao katika mwaka huu wa fedha.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo usizuie shilingi yangu daftari la kudumu linaendelea wizara tano tumemaliza, wizara tatu tunaingia mwaka huu katika kufanya daftari la kudumu lazima uwe mstahamilivu, ni kwamba tunaorodhesha kitu kimoja kimoja tutafanya mambo matatu kwa mpigo. Unaorodhesha *item* moja moja unaipa namba, unaipa na thamani, ni zoezi kubwa sana. Unaorodhesha hapa wizara hii kuna *glass* na *glass* hizi ziko ngapi, na unazipa namba halafu unazipa thamani na *you can imagine glass* tofauti thamani zake ni tofauti, na sisi hatuna *uniformity* katika manunuzi ndani ya serikali. Wizara hii ina kompyuta aina hii, wizara hii kompyuta aina hii zote ni bei tofauti. Kwa hivyo, nakuomba, tumepanga baina ya mwaka huu na mwakani; miaka hii mitatu tutakuwa tumeshamaliza *asset* zote za serikali kuziorodhesha na tunakwenda vizuri *inshaallah* tumuombe Mungu.

Hili umeniuliza, mimi ninachokijua tokea nilipokuwa huku najua *shares* za serikali kwa *ZANTEL* ni 18 *percent*. Sasa kama tuna *shares* ambazo zimepungua bado sijapata hiyo taarifa, nikipata taarifa ya mambo mengine yoyote nitakwambia, lakini *share* mpaka katika kikao cha mwisho, *share* yetu ndani ya *ZANTEL* ni asilimia 18.

Pia umezungumzia *deficit*, *deficit* yetu katika mapato yetu ya ndani na *deficit* yetu katika mapato yetu ya nje. Mhe. Mwenyekiti, ukichukulia *estimate* ni sahihi unavyosema, tulikisia kupata kiwango fulani hatukukipata kwa hivyo kama unachukulia ni *estimate* ile ndio *deficit*, lakini ile *estimate* inawezekana kwamba tumei-*estimate* kwa makosa, tumeipeleka *on the higher side.* Wakati mwengine unaweza ukafanya uka-*estimate* kitu kwa ku-*anticipate* kwamba hiki kitu kitakamilika kianze kunipa mapato, na hakijakamilika. Mfano, mzuri nitakupa *the E-government* na *ZANTEL*. Ni kwamba tume-*estimate* pale kupata 1.4 bilioni katika kuwapa nafasi *ZANTEL* watumie ili wauze sisi tuweze kupata, lakini bahati mbaya ule mlolongo wa ndani ya *ZANTEL* ulikuwa haujakamilika, ile *process* yote haijakamilika *from our estimate 1.4 billion* tumepata nini?

Mhe. Mwenyekiti, wakati mwengine kunakuwa kuna tatizo hilo, kwa hiyo ukichukulia *from estimate* kwa kile ambacho tulichovuna ni sahihi kabisa, tumekuwa na *deficit* katika maeneo yote; katika eneo la ndani na katika eneo la nje. Eneo la fedha za nje kuna maeneo mengine sisi wenyewe tumeyapeleka mbele kwa mfano *Airport terminal, Airport terminal* kutokana na matatizo ule uwanja tumeusimamisha sisi wenyewe SMZ zaidi ya mwaka mmoja na mfadhili naye amezuia fedha, kwa sababu tumeusimamisha. Kwa hivyo, ile hatukuipata, ingekuwa uwanja unaendelea zile pesa dola 7.4 milioni zingeweza kuja.

Vile vile umezungumzia suala la *innovation* liongezwe katika majukumu ya wizara. Sina tatizo nalo tutaliangalia na wataalamu tutaweza tukalitafutia pahala tutali-*cooperate* kila idara iwekewe malengo ya ukusanyaji wa mapato. Wasi wasi wangu mmoja tu kama haya ambayo wanayoweka wenyewe hayakusanywi, haya wanayoweka wenyewe tunaambiwa leteni tutakusanya, hayakusanywi. Kwa hiyo, nikiwapangia mimi malengo hawataweza kuyafikia, kwa sababu mimi malengo nitakayowapangia nitawapangia kutokana na mahitaji yangu, nahitaji bilioni 10 nitazigawa bilioni 10 kila pahala ili niweze kuzipata bilioni 10. Sasa haya ambayo ya kwao acha tuangalie nitawaomba wenzangu wa *ZRB* tukishirikiana na Idara yetu ya Sera na Utafiti pale ofisini tuweze kuona tunafanyaje katika hili ili tuweze kufikia malengo yetu ya ukusanyaji. *What can you do?* Tutafanya kitu kidogo ili tuweze kuona kuna matatizo gani huko, na hasa katika haya mawizara ndio matatizo makubwa sana tutaangalia tutafanya nini.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu Kariakoo umezungumza suala zuri sana *investment*, fedha za *ZSSF* kuziwekeza na kuziweka katika kijiji. Mimi nasema sio *ZSSF* peke yake hata nyinyi ukiwa na fedha zako ukiweka benki na ukiwa na fedha zako ukizizungusha kwenye biashara, basi kwenye biashara utapata faida kubwa zaidi kuliko hata ukiweka benki.

Kule benki unaiweka kwa sababu ni *risk* tu umeweka pale una pesa yako ya ziada umeweka pale siku unapotaka kwenda kuchukua angalau kufanya mambo yako mengine unapata kwenda kuchukua na kufanya mambo yako mengine.

Ukifanya miradi ambayo *risk* yake ni ndogo tumezungumzia miradi ya *real estate risk* yake ni ndogo sana, lakini nataka nikuhakikishie Mhe. Mahmoud Thabit Kombo; mtoto wa Muasisi, tumeshawaelekeza *ZSSF* katika kuelekea katika miradi hii, na sasa hivi kama unavyosema katika hotuba wanataka kuwekeza katika miradi ya nyumba. Kariakoo itazalisha kiasi gani kwa mwaka? Unajua ni kweli sisi kama serikali lazima tu-*compromise*, sisi kama serikali lazima tupime, serikali sio kila kitu inataka ipate faida tu mengine ile *social* ile inaisaidia serikali kuiweka juu, hatupati faida Wizara ya Afya sisi.

Sasa ukimwambia serikali kama hupati waondoe Wizara ya Afya wewe si serikali, hatupati faida sisi Wizara ya Elimu, ukiwaambia serikali waiondoe Wizara ya Elimu hii sio serikali, lakini ile *social*, unatengeneza wataalamu wazuri Zanzibar unapata sifa Zanzibar kwamba nina wataalamu wazuri.

Tunaye *Professor* Mbarawa pale Waziri ni sifa kwa Zanzibar, kuna *Professor* Idrissa Ahmada Rai ni sifa kwa Zanzibar, ndio maana ya kufundisha. Unapata hapa tiba unakwenda unapata tiba nzuri ni sifa kwa Zanzibar, watu wetu wanakwenda, ile *social* watu wanakuwa na imani na serikali yao, kuna mambo mengine sawa sawa na uwanja wetu wa Kariakoo. Sidhani kama uwanja wa Kariakoo kwamba utapata faida kubwa zaidi, lakini ile watoto wetu wana pahala ambapo wanakutana, mimi na wewe Mahmoud tuna pahala tunakutana, watoto wetu wakakutane wapi?

Kwa hivyo, kuna mambo mengine bwana Mahmoud lazima serikali iingie hata kama itapata hasara, iingie tu kwa sababu inatazama ile *social impact* yake na ndio uwanja wa Kariakoo, lakini kwa kukusaidia uwanja ule *capacity* yake ni kuingiza watu 15,000 kwa mpigo. Nimewaambia wenzangu kwamba lazima tuwe tuna *POS (Point of Sales*) tusiende watu na *cash* wakatoa *cash* pale, uwanja ule utaliwa, lazima kuwe kuna *POS* ambayo mtu ananunua kadi yake ana-*swap* anaingia ndani pesa zinakwenda moja kwa moja kwenye *account*. Tunataka kuweka malipo ya kileo, huu mpango wa kwamba lete hela nitie aah, tunataka kuanza mapema pale na tumeshazungumza na watu wa *ZSSF* pale tunataka kuanza mapema.

Tupunguze bei ya mafuta kidogo ili tuuze sana, nakubaliana na wewe kabisa katika hili na mimi nimewaambia watu wa mafuta waje na *option*, waniletee *option* yao niangalie halafu niangalie hiyo *volume* itakuwa kwa kiasi gani. Mimi nazungumzika hamna matatizo kabisa linazungumzika. Kwa hivyo, hili tutazungumza nao tukiona kwamba ni

sahihi kwamba tukipunguza kodi kidogo *volume* itakuwa kubwa sawa. Vile vile ili tuuze *volume* kubwa lazima tuangalie *capacity* ya uwekaji.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk amezungumza juzi hapa akasema kwamba wako wawekezaji wazalendo wanataka kuweka *storage capacity*, na mimi ninawa-*encourage,* Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tuwa-*encourage* hawa wazalendo waweke *storage* tutauza ndani, tutauza Comoro, tutauza Seychelles, waweke *storage* basi. Meli ya mafuta tunayo na tunataka tujenge nyengine mpya meli ya mafuta.

Mhe. Mahmoud amesema kuna tatizo gani kushusha riba kwa kuangalia miradi midogo midogo. Benki zote zimepewa uwezo na *BoT* kwa mkopaji mkubwa wanaweza waka-*negotiate* riba. *BoT* anatoa zile *standards* za riba lakini wao wanaweza waka-*negotiate.* Wapo mbona wanapata *interest* sio kubwa sana kama zile nyengine. Kwa hivyo, hili lipo.

Mhe. Mwenyekiti, muda ulionipa naona nimeutumia vizuri nimekubakishia dakika fulani fulani, kwa heshima kubwa kwa wale ambao sikufanikiwa kujibu hoja zao ni kwa sababu tu ya muda sio kwa sababu sijataka kukujibuni. Nakuheshimuni sana na nakupendeni sana.

Naomba sana niwashukuru watendaji wangu walionisaidia katika kufanikisha shughuli zetu hizi. Vile vile kama kawaida yangu nimshukuru mke wangu na familia yangu kwa kunisaidia kuniwezesha kuwepo hapa, siku zote, nawashukuru sana. Ahsanteni sana, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Fedha kwanza nakushukuru kwa kujali muda, lakini vile vile kwa kuweza kutoa majibu ambayo yana matumaini, na tunakuombea Mwenyezi Mungu akujaalie uweze kutimiza hizo ndoto ambazo umeziweka, na vile vile uweze kutimiza yale ambayo umeahidi kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo, tunakutakia kila la kheri.

Waheshimiwa Wajumbe kwa sasa hivi akidi yetu haitimii kuweza kuwahoji kwa ajili ya kama mumeikubali hoja ya Mhe. Waziri wa Fedha, kwa hiyo tutafanya kama tulivyofanya kwa Wizara ya Ardhi ili tutahojiana kesho, ili hiyo hiyo kesho sasa tutakuja kufanya majumuisho katika kamati.

Kwa hiyo, baada ya kusema hayo machache sasa naona zimebakia dakika 10, kwa hiyo naakhirisha kikao chetu hadi kufikia kesho saa 3:00 asubuhi.

(Saa 1:33 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 27/06/2014 saa 3:00 asubuhi)